

**13 SEPTEMBER, 2022**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 13 Septemba, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya  
Afrika Mashariki Uliimbwa**

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Akson) Alisoma Dua*

**KIAPO CHA UAMINIFU**

Mheshimiwa Mbunge afuataye aliapa kiapo cha uaminifu:-

Mhe. Tamima Haji Abass

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Taarifa inatolewa chini ya Kanuni ya 39(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020.

Katika Mkutano wa Saba wa Bunge (Mkutano wa baketi) Bunge lilipitisha Miswada miwili ya sheria kama ifuatavyo; kwanza Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali wa Mwaka 2022 (*The Appropriation Bill of 2022*) na pia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022 (*The Finance Bill of 2022*).

Kwa taarifa hii napenda kuliarifu Bunge hili tukufu kuwa tayari miswada hiyo miwili imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa sheria za nchi na sasa zinaitwa Sheria ya Matumizi ya Fedha Na. 4 ya Mwaka 2022 (*The Appropriation Act No. 4 of 2022*) nay a pili ni Sheria ya Fedha Na. 5 ya mwaka 2022 (*The Finance Act No. 5 of 2022*). (Makofi)

**13 SEPTEMBER, 2022**

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo sheria hizi zimeshaanza kazi. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):**

Maelezo ya Waziri Mkuu Kuhusu Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022 *(The Disaster Management Bill, 2022)*.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2022 *(The Disaster Management Bill, 2022)*.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Majumuisho ya Majibu ya Serikali na Mpango kazi wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):**

Taarifa ya Majumuisho ya Majibu ya Serikali na Mpango kazi wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

13 SEPTEMBER, 2022

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali. Tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwawa, sasa aulize swali lake.

Na. 1

**Ukarabati Hospitali ya Wilaya Mpwawa**

**MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa Hospitali ya Wilaya ya Mpwawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Jimbo la Mpwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga Shilingi bilioni 16.55 kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa wa hospitali kongwe za Halmashauri 19 kote nchini. Hospitali ya Halmashauri ya Mpwawa ni miongoni mwa Hospitali hizo ambapo imetengewa Shilingi milioni 900 kwa ajili ya kazi hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Natany Malima, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na jibu zuri la Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza ni kwamba, pamoja na uchakavu wa hospitali hii, lakini hatuna gari la wagonjwa: Je, ni lini Serikali italeti gari la kubebea wagonjwa (*ambulance*)?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Ni lini Waziri atafanya ziara katika hospitali hii ya Wilaya ya Mpwawa ili ajionee hali halisi ya hospitali ile? Ahsante.

**13 SEPTEMBER, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka huu wa fedha atapata gari la wagonjwa kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya katika Halmashauri ya Mpwapwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nilifanya ziara mwezi wa Nne mwaka huu katika Hospitali ya Mpwapwa, lakini nipo tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kufanya ziara tena kuona namna ya kuboresha huduma pale. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nini mpango wa Serikali kupeleka vifaa tiba kwenye zahanati zilizokamilishwa kwa nguvu za wananchi hasa katika Vijiji vya Mundarara, Loremeta, Gelai Lumbwa, vilivyopo katika Wilaya ya Logindo, Mkoa wa Arusha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka huu wa fedha Serikali imetenga Shilingi bilioni 69.95 kwa ajili ya kupeleka vifaa tiba katika vituo 530 zikiwemo hizi zahanati ambazo zimejengwa kwa nguvu za wananchi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Alaudin Hasham Salim, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Abubakari Asenga.

Na. 2

**Hitaji la Hospitali Mpya ya Wilaya – Ulanga**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA K.n.y. MHE. ALAUDIN H. SALIM** aliuliza:-

**13 SEPTEMBER, 2022**

Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali mpya ya Wilaya ya Ulanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alaudin Hasham Salim, Mbunge wa Jimbo la Ulanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga ina Hospitali ya Wilaya Ulanga ambayo ni kongwe na chakavu. Serikali itafanya tathmini ya hospitali hiyo ili kufanya maamuzi ya kuikarabati katika bajeti ya mwaka 2023/2024 au kuweka mpango wa kujenga hospitali mpya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri au Wilaya katika Jimbo la Kilombero unaenda kwa kusuasua: Je, Serikali inawahakikishia nini wananchi wa Jimbo la Kilombero kwamba hospitali hiyo ya Halmashauri itakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asenga ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kilombero kuhakikisha anatumia fedha za Serikali zilizoletwa kwa ajili ya kujenga hospitali hiyo, na hospitali hiyo ikamilike kwa wakati kama mpango kazi ulivyo. Nasi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutafuatilia kuona utekelezaji huo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya swali la nyongeza. Hospitali ya Wilaya ya Kilwa maarufu kama Kinyonga iliyopo Kilwa Kivinje ni chakavu, lakini imeidhinishiwa fedha shilingi milioni 900: Lini Serikali itapeleka fedha hizo ili ukarabati ufanyike?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

13 SEPTEMBER, 2022

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Kassinga, Mbunge wa Kilwa Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hospitali chakavu kama hospitali ya Wilaya ya Kilwa maarufu "Kinyonga", imetengewa Shilingi milioni 900 na katika mwaka huu wa fedha Serikali inaendelea kutafuta fedha ili tupeleke katika hospitali hiyo kwa ajili ya ukarabati. Ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mathayo David, swali la nyongeza.

**MHE. MATHAYO D. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Vudee na Kata ya Mshewa katika Jimbo la Same Magharibi, ni miongoni mwa Kata za kujengewa vituo vya afya vya kimkakati: Je, ni lini Serikali itajenga vituo vya afya katika Kata ya Vudee na Kata ya Mshewa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mathayo David Mathayo, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mbunge kwamba Serikali iliainisha kata zote za kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya na tutakwenda kujenga vituo vya afya hivyo kwa awamu ikiwemo kata hizi za kimkakati katika Jimbo la Same Magharibi. Ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wilaya ya Biharamulo, tuna ujenzi wa hospitali ya Wilaya pale, lakini ujenzi ule umekwama kwa muda mrefu kwa sababu ya pesa iliyorudishwa Shilingi milioni 204. Hii fedha nimeisema mbele ya Rais akiwa Biharamulo tarehe 8 Juni, na TAMISEMI wakaahidi kwamba wanakwenda kuifuatilia: Ni lini sasa fedha hii italetwa ili tuweze kukamilisha kwa sababu kila kitu kiko tayari pale isipokuwa fedha hii? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa, Mbunge wa Jimbo la Biharamulo, kama ifuatavyo:-

**13 SEPTEMBER, 2022**

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Mbunge amefuatilia sana suala ya fedha hizi na ameshauliza hapa. Tulikubaliana na Hazina kwa maana ya Wizara ya Fedha, fedha zile ziweze kurejeshwa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafuatilia sisi na Wizara ya Fedha, tuhakikishe fedha zinakwenda kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Kabla sijamwita wa tatu, Waheshimiwa Wabunge hao wachache waliouliza maswali ya nyongeza wamejitahidi, lakini inabidi yapunguzwe. Nenda moja kwa moja kwenye swali, usianze na hadithi kwanza halafu ndiyo uulize swali ili kutoa fursa kwa Wabunge wengi kuuliza maswali.

Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Halmashauri ya Mji wa Bunda, imeanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri kwenye Kata ya *Bunda Store*, na Serikali ilitenga Shilingi milioni 500: Kuna mkakati gani wa kutenga fedha kila mwaka wa fedha ili ile hospitali iweze kukamilika haraka? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, dhamira ya Serikali ni kuendelea kutenga fedha kila mwaka wa fedha, ndiyo maana tulipeleka Shilingi milioni 500 na kila mwaka wa fedha tutatenga Shilingi milioni 500 au zaidi kuhakikisha Hospitali ya Mji wa Bunda pia inakamilika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo, sasa aulize swali lake.

Na. 3

### **Kuigawa Kata ya Katumba – Nsimbo**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaigawa Kata ya Katumba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

13 SEPTEMBER, 2022

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe Mbunge wa Jimbo la Nsimbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhitaji wa kuigawa Kata ya Katumba kutokana na ukubwa wake na idadi kubwa ya watu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuwepo kwa maeneo mengi ya utawala ambayo bado hayana miundombinu muhimu ya kiutawala na ya huduma za jamii, Serikali kwa sasa imeweka kipaumbele zaidi katika kujenga miundombinu hiyo ili kutoa huduma bora kwa wananchi badala ya kuanzisha maeneo mapya ya utawala.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo inashauriwa kukamilisha hatua za maombi na kuwa na subira katika kipindi hiki mpaka hapo Serikali itakapoona inaweza kuigawa Kata hiyo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anna Lupembe, swali la nyongeza.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri, lakini kwa kuwa mtendaji ni mmoja na watendaji wa vijiji wako wawili tu, kata ni kubwa, ina vijiji 16: Ni lini Serikali itaongeza watendaji kwa ajili ya kata hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kutokana na mazingira magumu ya kata hiyo, vijiji 16 na mazingira magumu: Ni lini Mtendaji wa Kata ya Katumba anaweza kupata usafiri kwa ajili ya kufanya kazi kwa ufanisi zaidi? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua kwamba kata hii ni kubwa, ina vijiji 16 na inahitaji nguvu zaidi kwa watendaji wa kata kuhakikisha kwamba wanatoa huduma na pia watendaji wa vijiji. Naomba nilichukue jambo hili, tutalifanyia kazi na



**13 SEPTEMBER, 2022**

nitawasiliana naye kuhakikisha kwamba kata hii inaongezewa nguvu ya watendaji. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mahitaji makubwa ya wananchi ni kupata vitongoji vipya na vijiji vipya; na kwa kuwa mchakato huu haueleweki sana kwao, sisi tunalalamikiwa: Je, Serikali ina utaratibu gani sasa wa kugawa vijiji na vitongoji na mitaa ili kurahisisha huduma kwa wananchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna mahitaji ya kugawa vijiji, vitongoji, kata na mara nyingine hata Halmashauri katika nchi yetu, lakini kama nilivyotangulia kujibu kwenye maswali ya msingi kwamba kipaumbele chetu sasa Serikali ni kuboresha kwanza miundombinu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu ni kwamba wananchi wanafanya vikao vyao vya Halmashauri za Kijiji na kwenda DCC na RCC na baadaye kuwasilisha maombi Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwa hiyo, namwombe Mheshimiwa Mbunge waanze taratibu hizo za kisheria wakati tukisubiri maamuzi ya Serikali kuja kugawa maeneo mengine ya kiutawala. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kata ya Rungwe Mpya iliyoko Jimbo la Kasulu Vijijini ina idadi kubwa ya watu wengi sana: Je, ni lini Serikali itakubali kuigawa kata hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu la nyongeza la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itagawa kata hizo baada ya kuwa tayari imeshaboresha miundombinu kwenye

**13 SEPTEMBER, 2022**

maeneo ya utawala yaliyopo sasa. Tuna kata nyingi na vijiji ambavyo bado vinahitaji uboreshaji. Kwa hiyo, baada ya hapo tutakwenda pia kutazama Kata hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Peter Getere, swali la nyongeza. Mheshimiwa Neema Mwandabili, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Mlowo ni moja kati ya kata kubwa sana katika Mkoa wetu wa Songwe: Ni hatua zipi Serikali imefikia katika mchakato wa kuigawa kata hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kata ya Mlowo ni moja ya kata kubwa, lakini utaratibu ni kwamba, endeleeni na taratibu za kuwasilisha maombi kwa mujibu wa taratibu za ugawaji wa maeneo ya utawala. Hata hivyo kipaumbele kwa sasa ni kuhakikisha tunaboresha miundombinu kwenye kata zilizopo kabla hatujakwenda kugawa kata hizi nyingine. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaelekea Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 4

### **Kikosi Kazi Kuratibu Mikataba ya Mazingira**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuunda Kikosi Kazi kuratibu Mikataba ya mazingira na mabadiliko ya Tabianchi kati ya Tanzania Bara na Zanzibar?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

**13 SEPTEMBER, 2022**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Kusini Pemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuliariifu Bunge lako Tukufu kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama wa mikataba mbalimbali ya Kimataifa ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira ambayo inaratibiwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, utaratibu unaotumika katika kuratibu masuala ya mikataba ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni wa kushirikiana katika majadiliano ya pamoja na kushiriki katika mikutano ya Kimataifa na utekelezaji wa Mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikishirikiana kwa karibu na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kutekeleza program na miradi mbalimbali ya hifadhi na usimamizi wa mazingira inayotekelezwa chini ya mikataba husika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa mashirikiano haya hayapo kisheria: Je, Serikali haioni haja ya kuwa na utaratibu wa kisheria ili kuwezesha ushiriki wa Zanzibar kuwa bora zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Je, mpaka kufikia Julai, 2022, Zanzibar imenufaika na miradi gani ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kusini Pemba, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, kama ifuatavyo:-

**13 SEPTEMBER, 2022**

Mheshimiwa Spika, ushirikiano na majadiliano ambayo huwa tunafanya yanayohusiana na mikataba ya Kimataifa, ya mazingira na kukabiliana na mazingira ya tabia ya nchi, ni ya kisheria. Maana yake, yako kisheria. Hata ukienda ukisoma Katiba ya Jamhuri kwenye fungu lile la *Foreign Affairs* utakuta kumeelezwa namna ambavyo inatakiwa tushirikiane kwenye mahusiano yanayohusu masuala ya mikataba ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hata ukienda kwenye sheria yetu ya mazingira, imeeleza, Waziri anayehusika na mazingira kwa upande wa Jamhuri ya Muungano, basi anatakiwa akae na ashirikiane na Waziri anayehusika na mazingira kwa upande wa Zanzibar. Kwa hiyo, majadiliano haya hasa mikataba ya Kimataifa yanakuwa yapo kisheria zaidi.

Mheshimiwa Spika, ipo miradi ambayo imetekelezwa na inaonekana. Kwa mfano, kuna ujenzi wa kuta ama kingo za kuzuia maji Wete kule Sepwese, hiyo ipo; pia kuna miradi ya kurejesha ardhi iliyoathirika na mabadiliko ya tabia ya nchi, hii iko maeneo ya Kiuyu, Shumba Viamboni, Shumba Mjini, Maziwa Ng'ombe maeneo mingine miradi hii ipo na imepita.

Mheshimiwa Spika, pia upo mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi maeneo ya Kaskazini A, Unguja katika Mkoa wa Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Charles Kajege.

Na. 5

### **Fedha za VAT Zilizorudishwa kwa Wanaodai Serikali**

**MHE. CHARLES M. KAJEJE K.n.y. MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza:-

Je, ni fedha kiasi gani zimerudishwa kwa wadai wa VAT wanaoidai Serikali kuishia mwaka wa fedha 2021/2022?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

**13 SEPTEMBER, 2022**

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2021/2022, jumla ya Shilingi bilioni 916.68 zililipwa kwa wadai wa VAT, sawa na ufanisi wa asilimia 431.7 ikilinganishwa na bajeti iliyotengwa. Ufanisi huu umetokana na hatua iliyochukuliwa na Serikali ya kuhakiki maombi ya wadai kwa kuzingatia viashiria hatarishi badala ya utaratibu wa awali wa kuhakiki maombi yote kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo umeongeza kasi ya uhakiki na ulipaji wa madai ya marejesho ya VAT na kupunguza ucheleweshwaji kwa kuwa uhakiki unafanyika kwa wakati. Hatua na mafanikio hayo yanalenga kuchochea ukuaji wa uchumi, uwekezaji na kulinda mitaji ya wawekezaji na wafanyabiashara hapa nchini. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naipongeza Serikali kwa kuanza kufanya malipo hayo. Je, ni lini Serikali itakamilisha malipo ya madai yaliyosalia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Charles Kajege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhakiki na kupitia madeni yote ambayo maombi yao yameletwa. Mara tu utakapokamilika uhakiki huo, Serikali itaendelea kulipo kwa madeni yote yaliyosalia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali yako kwa Mheshimiwa Wabunge. Samahani unaswali lingine, Mheshimiwa Toufiq Salim Turkey, Mbunge wa Mpendae, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Ramadhani Ramadhani.

Na. 6

**Kudhibiti Mfumuko wa Bei Nchini**

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN K.n.y. MHE. TOUFIQ SALIM TURKY**  
aliuliza:-

**13 SEPTEMBER, 2022**

Je, Serikali ina mpango gani juu ya mfumuko wa bei unaoendelea nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Toufiq Salim Turkey, Mbunge wa Mpendae, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2021/2022, mfumuko wa bei uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.0 ikilinganishwa na asilimia 3.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/2021. Pamoja na ongezeko hili, mfumuko wa bei umeendelea kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja na upo ndani ya lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki la asilimia 8.0 na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika la kati ya asilimia 3.0 hadi 7.0.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mikakati mbalimbali ikiwemo: kuimarisha sekta za uzalisha ili kuongeza upatikanaji wa bidhaa unaoendana na mahitaji; kutoa ruzuku kwa ajili ya kupunguza bei ya nishati ya mafuta kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa mwezi ambapo shilingi bilioni 500 zimetengwa; kutoa ruzuku ya pembejeo za mbegu na mbolea na kutoa unafuu wa kodi katika uagizaji wa baadhi ya bidhaa muhimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua nyingine katika suala hili ikiwemo: kuruhusu watu wenye uwezo wa kuleta mafuta kwa bei nafuu; kuanzisha mfuko wa kuhimili ukali wa bei za mafuta baada ya bei za mafuta kutulia katika soko la dunia; kuanzisha hifadhi ya mafuta ya kimkakati na kuanzisha upokeaji wa mafuta katika ghala moja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, swali la nyongeza.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ingawa, Mheshimiwa Naibu Waziri amejiibu vizuri kwenye swali la msingi, lakini naomba niulize swali la nyongeza. Serikali imeshafanya jitihada za makusudi kwenye kupunguza ukali kwenye bidhaa ya mafuta. Je, Serikali haioni haja ya kufanya jitihada hizo hizo ili kupunguza ukali kwenye bidhaa za vyakula?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

**13 SEPTEMBER, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ramadhan, Mbunge wa Chake Chake, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi kwamba tayari Serikali imeshotoa ruzuku kwa upande wa mbolea na tayari Serikali imeshusha kodi ya uingizaji wa mafuta ya kula. Kwa hiyo, Serikali imeshachukua hatua ya kupunguza ukali wa mfumuko wa bei za mafuta.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ussi Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini naomba niulize swali la nyongeza. Serikali imekuwa na majibu mazuri sana kuhusu mfumuko wa bei, lakini uhalisia ulivyo nje katika mitaa na vijiji, hali ilivyo haiko hivyo ambavyo Serikali imekuwa ikijibu. Je, Serikali inaliambia nini Taifa letu la Tanzania juu ya mfumuko huu wa bei?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ussi Pondeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali na mipango yake ya Serikali ni kusimamia bei za bidhaa na kuona kwamba wananchi wanapata huduma zao kwa bei nafuu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, sasa aulize swai lake.

Na. 7

### **Sheria ya Kusimamia Kampuni Binafsi za Ulinzi**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza:-

Je ni lini Serikali italeta Bungeni Muswada wa Sheria ya Kampuni Binafsi za Ulinzi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mhandisi Masauni, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Athuman Almasi Maige, Mbunge Wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo kwa Sheria inayosimamia Makampuni Binafsi ya Ulinzi na kwa sasa Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mapendekezo ya kutunga Sheria ya Huduma za Sekta Binafsi ya Ulinzi umekamilika na utawasilishwa katika Baraza la Mawaziri kwa ajili ya maamuzi baada ya kupata maoni ya kina ya wadau wa pande zote mbili za Muungano juu ya rasimu ya sheria hiyo. Baada ya kukamilika kwa hatua hizo Muswada wa Sheria hiyo utaletwa Bungeni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri usiende kukaa, subiri maswali ya nyongeza hapo.

Mheshimiwa Almasi Maige.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nisikitike kwamba majibu ya Serikali hayaridhishi. Muswada huu niliuleta mimi binafsi mwaka 2016 ndiyo ukachukuliwa na Serikali. Hii mara ya tatu, Serikali inajibu hivi hivi kwamba inafanya hivi, inapeleka kwa wadau. Je, Serikali haioni kwamba miaka sita kugonjea Muswada mmoja ni muda mrefu sana?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari sasa kuruhusu mjadala kati ya mimi niliyeleka Muswada huo ili kuukwamua Muswada huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Maige kwa kanuni zetu unataka kuelewa sehemu yako ya kwanza. Umesema huridhiki na majibu, kwamba majibu si ya kweli, hayana uhalisia, ama uridhiki nayo kwa sababu umekuwa ukipewa majibu hayo hayo? Nieleweshe vizuri.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, suala kwamba Muswada huu utapelekwa kwa wadau, ulishapelekwa.

**SPIKA:** Kwa hiyo, majibu haya hayaendani na swali lako?

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Ni kweli.

**SPIKA:** Kama ndivyo basi swali lako la nyongeza na hilo la msingi tupe muda tukafuatilie kama Waziri kajibu sawa sawa ama tofauti na wewe



**13 SEPTEMBER, 2022**

unavyosema ili tukishashughulika na hiyo sehemu ya kwanza tutakupa fursa ya kuuliza tena wakati mwingine. *(Makofi)*

Sasa hapa kulikuwa na Mbunge aliyekuwa anataka kuuliza swali la nyongeza, sasa tukishaambiwa haya majibu siyo halisi hatuwezi kuweka maswali ya nyongeza. Kwa sababu maswali ya nyongeza yanatokana na majibu yaliyotolewa hapa mbele.

Kwa hiyo, tutaendelea na swali linalofuata, swali la namba saba, tutaenda kulifanyia kazi halafu majibu yatatolewa hapa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, sasa aulize swali lake.

Na. 8

### **Wafungwa Kupata Haki ya Faragha na Wenza Wao**

**MHE. BAHATI K. NDINGO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaweka mfumo utakaoruhusu wafungwa kupata haki ya faragha na wenza wao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa haki mbalimbali kwa wafungwa walioko magerezani kwa mujibu wa sheria. Haki ya faragha kwa wafungwa na wenza wao itaanza kutolewa pale ambapo mifumo ya kisheria, na miundo mbinu ya magereza itakapokidhi kutolewa kwa haki hiyo. Masuala mengine yatakayozingatiwa ni usalama, mila na desturi za Watanzania, kwani haki hiyo inatakiwa kutekelezwa kwa faragha.

**SPIKA:** Bahati Ndingo, swali la nyongeza.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nina maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza; ni mifumo ipi ya kisheria ambayo mpaka sasa haijatengenezwa?

**13 SEPTEMBER, 2022**

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mchakato huo utachukua muda gani ili wafungwa wetu waweze kupata haki ya msingi na tumpunguzie haki balozi wa afya ya akili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali yote ya nyongeza ya Mheshimiwa Bahati Ndigo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba ieleweke kwamba suala la tendo la ndoa si haki ya msingi, ni haki lakini si haki ya msingi. Haki ya msingi ambayo tunatoa kwa wafungwa, chakula malazi, mavazi kwa hiyo, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba kuna mambo ya kuzingatia ambayo yanapaswa kuzingia kwanza kabla ya kuruhusu haki hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge anapigania.

Mheshimiwa Spika, hata ukiangalia katika nchi zilizoendelea basi utaratibu huo haupo kama hivyo, kuna utaratibu ambao wale wafungwa wanapelekwa kwenda kutembelea familia, siyo inafanyika katika magereza, lakini ukitaka ifanyike magereza unahitaji kwanza uangalie miundombinu, mila zetu na desturi. Kwa sababu wakati mwingine inakuwa siyo jambo jema kwa mila zetu na desturi, kwamba kila mtu anajua sasa hawa wanakwenda kufanya tendo la ndoa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa maelezo hayo naomba Mheshimiwa Bahati aridhikena majibu yangu ya msingi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ni kwa nini Serikali isiweke utaratibu wa kuwawezesha mahabusu au wafungwa kupata fursa ya kuzungumza na familia zao angalau mara moja kila baada ya miezi mitatu, kuliko hivi sasa unaongelea kwenye nondo, unakuta hakuna usikivu wowote ule?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la namna ya kuboresha utaratibu wa kuzungumza aidha wenza wao na familia zao ni jambo ambalo linazungumzika. Kimsingi tukubaliane kwamba sasa hivi utaratibu huo upo, labda Mheshimiwa

Esther yeye haridhiki na ile *frequency* ama muda. Sasa hilo linategemea na mambo mengi, mazingira, kwa sababu masuala ya magereza yanazingatia usalama, kwamba watu walioko ndani na watu wanaokuja, ni lazima mazingira ya magereza iendelee kulindwa kiusalama ili wanaokuja wasihatarishe usalama wa magereza na wafungwa walioko ndani. Ndiyo maana utaratibu huo umewekwa kwa sasa hivi, lakini pale ambapo miundombinu itaruhusu na pengine utaratibu wa kuweza kuwaona mara kwa mara si jambo baya, lakini nadhani ni jambo linalotakiwa kuangaliwa na kutafakariwa kulingana na usalama wa magereza yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali fupi la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Magereza zetu zimekuwa na tatizo ambalo linatokana na hili swali la msingi kwamba kwa kuwa hawa watu wanakosa faragha, wengine wanafanya vitendo wenyewe kwa wenyewe mle magerezani. Je, Serikali ili kupunguza hivyo vitendo vya watu kugeuzana wenyewe kwa wenyewe magerezani, inachukua hatua gani kupunguza vitendo hivyo ambavyo vinasababisha kuwa kinyume hata na mila na desturi zetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna njia nyingi ambazo Serikali inachukua, la kwanza ni kuhakikisha tunaimarisha ulinzi katika magereza na kuimarisha ulinzi kuna njia nyingi vilevile, tuna mifumo ya *ki-intelligence* kupata taarifa kabla matukio hayajajitokeza. Pia kuna utaratibu ambao kuna askari waliopo katika magereza kuangalia mienendo na mazingira ya wafungwa katika magereza na tabia zao vilevile.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi ni kwamba kupitia Serikali ya Awamu ya Sita, kuna mikakati kabambe ya kufanya maboresho makubwa katika vyombo vyetu vya usalama. Moja ni kuhakikisha tunaimarisha na kuboresha miundombinu ya magereza ili kutenganisha kati ya wafungwa kwa mfano, kutenganisha wafungwa wenye umri fulani mpaka umri fulani, wenye historia ama rekodi ya uharifu zaidi kuliko wengine na mambo mengine, ili kutoa nafasi kwa kuweza kupeleka nguvu zaidi ya uangalizi katika maeneo ambayo yanastahili kulingana na uzito na changamoto ya mfungwa husika.

**13 SEPTEMBER, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 9

**Kudhibiti Uhalifu Nchini**

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti ongezeko la uhalifu nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi inaendelea na mikakati yake ya kudhibiti vitendo vya uhalifu hapa nchini kwa kuimarisha doria, kufanya misako na operesheni mbalimbali dhidi ya uhalifu na wahalifu, pamoja kutoa elimu kwa jamii kutokujihusisha na vitendo vya uhalifu na kufuata sheria za nchi. Kushirikisha jamii kwenye ulinzi wa maeneo yao kupitia dhana ya ulinzi shirikishi. Pia Serikali imewapeleka wakaguzi wa polisi kwenye kata na shehia ili kushughulikia uhalifu kwa kushirikiana na wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos, swali la nyongeza.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kumejitokeza suala la uhalifu ambao unafahamika kwa jina la panya *road*, je, Serikali ina mikakati ipi ya kuweza kuwaelimisha wananchi ili kuendelea kujikinga na suala hili la panya *road*?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa uhalifu huu unafanyika Zaidi kwa silaha za jadi pamoja na silaha nzito. Serikali ina mkakati gani juu ya udhibiti wa silaha hizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tauhida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na utaratibu wa elimu kwa jamii kuhusu kukabiliana na uhalifu wa aina mbalimbali ikiwemo uhalifu ambao amezungumza Mheshimiwa Mbunge. Kwanza hivi karibuni tumeweka utaratibu wa kupeleka askari katika kila kata, kuna askari ambao walihitimu mafunzo ya kuupandishwa vyeo na hawa tumewatawanya katika kata zote nchi nzima kwa ajili ya kwenda kusaidia utaratibu na mifumo ya ulinzi shirikishi katika maeneo husika pamoja na utoaji elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kama hilo halitoshi hivi karibuni tumepata maelekezo kutoka kwa Amiri Jeshi Mkuu kwamba tuhakikishe tunakamilisha ununuzi wa magari ambayo yatakwenda moja katika wilaya na utaratibu wa kupeleka mafuta uende moja kwa moja wilayani kusaidia kuimarisha vitendea kazi kwa askari wetu walio karibu na wilaya na kata zetu kwa lengo la kuandaa mipango thabiti ya elimu kwa umma kuhusiana na ulinzi shirikishi pamoja na jitihada nzima za kushirikisha wananchi katika kusaidia vyombo vyetu vya usalama hususan Jeshi la Polisi katika kudhibiti uhalifu, si katika elimu tu hata kujipanga katika kudhibiti matukio ya kiuhalifu yasijitokeze.

Mheshimiwa Spika, nimjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, baadaye Jeshi la Polisi watafanya mazungumzo na vyombo vya habari, watazungumza kutoa na kuainisha mkakati kabambe wa kupambana na waharifu ikiwemo Mkoa wa Dar es Salaam, hatua zilizofikia, mafanikio, changamoto, sababu na mipango ya kudhibiti jambo hilo lisiendelee kutokea zaidi. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine, wananchi wanaweza kupata ufafanuzi zaidi wa kina juu ya jambo hili hapo baadaye.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, jitahidi majibu yawe mafupi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kumekuwepo na ongezeko kubwa la uhalifu na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwenye mabasi yanayobeba wanafunzi wa shule za msingi na sekondari. Je, Serikali haioni ni wakati sahihi sasa kutoa maagizo kwamba mabasi haya yaendeshwe na madereva wanawake na makondakta wawe wanawake ili tunusuru ukatili wa kijinsia unaoendelea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, inawezekana ikawa ushauri wake ni moja kati ya mambo yanayoweza kusaidia, kwa hiyo tunauchukua. Hata hivyo, ziko na hatua zingine ambazo Serikali inazifanyia kazi, kwa pamoja tutajumuisha na ushauri wake ili tuweze kufanyia kazi ili matatizo kama haya yasijitokeze tena.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kuniona.

Swali langu ni kwamba je, Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo vya polisi katika Tarafa za Kipatimu, Njinjo na Mandawa Wilayani Kilwa ili kudhibiti vitendo vya uhalifu katika Wilaya ya Kilwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikiri juu ya changamoto ya upungufu wa vituo vya polisi katika kata za jimbo ambalo Mheshimiwa Mbunge ameeleza, lakini nizungumze kwa ujumla wake kwamba tuna upungufu wa vituo vya polisi tuna mpango wa kuongeza vituo vya polisi kwa miaka kumi zaidi ya mia tatu na hamsini na kitu ambavyo tunahitaji zaidi shilingi bilioni mia moja sitini na kitu.

Nataka nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mikakati ya kufanikisha mkakati huu wa ujenzi na Wabunge wengine ambao wana shida ya vituo vya polisi katika maeneo yao kwa miaka kumi, mwelekeo wa kuutekeleza mkakati huo katika kipindi kifupi sana upo katika hatua nzuri. Kwa hiyo, wakae mkao wa kula, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine kwamba tuna mkakati kabambe na upo katika hatua nzuri ya kuukamilisha kabla ya muda uliopangwa ambao utatusaidia sana kupunguza changamoto za vituo vya polisi katika nchi hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ninakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

**Ujenzi wa Hosteli ya Madaktari Watarajali - Hospitali ya Mkoa wa Ruvuma**

**MHE. MARIAM M. NYOKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha jengo la hosteli ya madaktari watarajali katika Hospitali ya Mkoa wa Ruvuma lililoanza kujengwa mwaka 2014/2015?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummu Mwalimu majibu.

**WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni moja katika mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la hosteli ya madaktari watarajali (*interns*) katika Hospitali ya Mkoa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa hosteli hii utaendelea mara tu fedha hizi zitakapokuwa zimetolewa na tunatarajia ujenzi huu utakamilika ifikapo Juni, 2023.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka swali la nyogeza.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, naomba niulize swali langu lingine la nyongeza.

Kwa kuwa mazingira ya nje ya majengo ya hospitali hii ya Mkoa wa Ruvuma sio rafiki hasa kwa watumishi na wagonjwa kwa kipindi cha mvua; je, Serikali ina mpango gani wa kuweka *paving* pamoja na kujenga mifereji ya maji ya mvua katika hospitali hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka kwa swali lake zuri, lakini kwa kufatilia maendeleo ya utoaji huduma katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuboresha hospitali zote za rufaa za mikoa kwa kuwa ni kiungo muhimu cha utoaji huduma kati ya ngazi ya msingi na huduma za rufaa za juu. Kwa hiyo,

**13 SEPTEMBER, 2022**

tumepokea changamoto ya mazingira ya nje ambayo hayavutii na nikuahidi kwamba najua pia kuna suala la barabara tutawasiliana na *TARURA* ili pia kuweza kuweka lami katika barabara ambayo inaelekea kwenye hospitali ya rufaa ya mkoa.

Mheshimiwa Spika, suala la *tent* hilo ni jambo ambalo tutalifanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Hospitali ya Mkoa wa Simiyu haina wodi za kulaza wagonjwa, wodi ya wanaume, wanawake na watoto; je, ni lini Serikali itajenga wodi hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Esther Midimu kwa swali lake la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti yetu ya 2022/2023 tumetenga fedha kwa ajili ya kuongeza wodi za kulaza wagonjwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu na baada ya Bunge mimi mwenyewe nitakwenda Simiyu pamoja na Mheshimiwa Esther Midimu ili kuhakikisha kwamba ujenzi unaanza haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri asante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 11

### **Ujenzi wa Uwanja wa Mpira-Dodoma**

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS** aliuliza:-

Je, ni lini ahadi ya ujenzi wa uwanja wa mpira Dodoma iliyotolewa na Mfalme wa Morocco itatekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Pauline Gekul majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-



**13 SEPTEMBER, 2022**

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana na kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefuatilia utekelezaji wa ahadi ya ujenzi wa uwanja wa mpira Dodoma iliyotolewa na Mfalme wa Morocco. Mawasiliano kuhusu utekelezaji wa mradi huo baina ya Serikali ya Tanzania na Morocco bado yanaendelea. Vilevile katika kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa Serikali imedhamiria kutafuta fedha kutoka katika vyanzo mbalimbali vikiwemo sekta binafsi na wabia wa maendeleo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba ujenzi wa uwanja wa kisasa wa michezo na shughuli za Serikali kwa Makao Makuu ya Dodoma haukwepeki. *(Makofi)*

Je, Serikali pamoja na majibu ya kusema kutafuta wabia, wadau mbalimbali wa michezo, kwa nini Serikali isiwe na *commitment* kwamba mwakani katika bajeti tunatenga fedha ili ujenzi huo uanze, ukitilia maanani uwanja hauwezi kujengwa kwa mwaka mmoja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani hukusikia ile sehemu ya kwanza. Anasema yaani hilo jambo la kujenga uwanja huo mkubwa wa kisasa hapa Dodoma kwa kuwa ni Makao Makuu haukwepeki. Kwa hiyo, Serikali badala ya kusubiri yule Mfalme wa Morocco atimize ahadi yake Serikali ijipange kama vile. Sasa wewe umjibu yeye anataka mwakani kwenye bajeti muanze kuweka Serikali ili ile ahadi ije iwakute njiani ndio swali lake. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru.

**SPIKA:** Pole nilikuwa nakueleweshia lile swali lake linahusu nini naona ulikuwa unaonekana hujamsikia sasa nikawa nakusaidia, kwa hiyo sasa jibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Innocent kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekwisha kujipanga na ndio maana tumeshafanya upembuzi yakinifu kujua kwamba huu uwanja tunaujenga wapi, lakini kwa gharama gani. Huu uwanja unahitaji zaidi ya shilingi bilioni 420 na

Serikali tuko kwenye hizo hatua pamoja na maongezi yanayoendelea lakini ndani ya Serikali tunaendelea kutafuta fedha.

Mheshimiwa Spika, nihakikishie Bunge hili tukufu huu uwanja pia ni ahadi ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 na lazima tutaujenga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza kabisa nataka nimpongeze Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa uzinduzi wa uwanja mzuri kule Ruangwa. Sambamba na pongezi hizo nataka niipongeze vilevile timu ya Namungo ambayo ilicheza na ikashinda vizuri sana kwenye ule uwanja wa nyumbani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali langu; je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza juhudi za wananchi katika kuhakikisha kwamba uwanja ule unakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, na sisi Serikali pia tumeendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuonesha mfano katika suala zima la michezo na kuendeleza miundombinu ya michezo, lakini pia wenzetu wa Ruangwa pamoja na halmashauri yao.

Mheshimiwa Spika, sisi Serikali tumeendelea kuunga mkono jitihada za wadau mbalimbali kuhakikisha pia accessories za michezo kama nyasi bandia, lakini pia vifaa vya michezo kodi inapunguzwa. Sisi tutaendelea kushirikiana na halmashauri na watu binafsi kuhakikisha kwamba tunatengeneza mazingira rahisi ya uwekezaji katika michezo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwenye Bunge la Bajeti lililopita tulipitisha bajeti ya shilingi bilioni 10 kuweka nyasi bandia kwenye viwanja vya michezo nchini; je,

**13 SEPTEMBER, 2022**

Serikali imefikia hatua gani kwenye kuweka nyasi bandia kwenye viwanja vyetu kwa sababu ligi inaendelea na bado viwanja haviridhishi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi kuweza kujibu swali la Mheshimiwa Festo Sanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika bajeti iliyopita ya Bunge tulipitisha zaidi ya shilingi bilioni 10 kuhakikisha kwamba tunaboresha viwanja vya Arusha, Mwanza, Tanga, Dodoma, Mbeya na viwanja vyetu vikuu vya Mkapu ambavyo sasa vinatumika na vya Uhuru.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara tumeshaanza mchakato kuhakikisha kwamba mwaka huu wa fedha haupiti bila hizi fedha kutumika. Kwa hiyo, Wizara kupitia kitengo chetu cha manunuzi wameshaanza mchakato na tumeendelea kusisitiza kwamba jambo hili la kuboresha viwanja hivi iweze kuanza mapema ili hivi viwanja viweze kutumika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suleiman Haroub.

**MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu ya nyongeza kwa kifupi.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba nilithibitishie Bunge lako tukufu na Watanzania kwa ujumla kwamba viwanja hivi ambavyo Mheshimiwa Sanga amevizungumza havitawekwa tu nyasi bandia na nyasi za kawaida, tutakwenda kuweka viti vya kisasa kabisa. Pia viwanja hivi tunakwenda kuvitengeneza kwa namna ambavyo tunaweza kuvitumia kimataifa na mchakato huu wa ujenzi utanza mwaka huu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Suleiman Haroub Suleiman, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi sasa aulize swali lake.

Na. 12

**Vigezo vya Wachezaji Taifa Stars**

**MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN** aliuliza:-

Je, ni vigezo gani vinatumika kuchagua wachezaji wa timu ya Taifa (*Taifa Stars*)?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nikushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Haroub Suleiman, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jukumu la kusimamia timu zote za Taifa ni la Serikali kwa kushirikiana na Vyama na Mashirikisho ya Michezo. Kwa mujibu wa Kamati ya Ufundi ya *TFF* vigezo vinavyotumika kuchagua wachezaji wa *Taifa Stars* ni kama ifuatavyo; mchezaji awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mchezaji anayecheza katika kluba ya ligi za juu, mchezaji anayepata nafasi na kucheza kwenye kluba husika (*playing time*), mchezaji awe na ufanisi mzuri wa kucheza (*good performance*), awe na vigezo katika nafasi anayocheza (*fitting the positional profile*), pamoja na kuwa na nidhamu ya kiuchezaji na nidhamu katika maisha ya kawaida.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suleiman Haroub Suleiman, swali la nyongeza.

**MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majawabu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, timu ya *Taifa Stars* ni timu ya Tanzania na Tanzania ina ligi kuu mbili kwa maana ya kwamba Ligi Kuu ya Zanzibar na Ligi Kuu ya Tanzania Bara. Sasa je, kwenye kuchagua wachezaji kwenye kutafuta wachezaji kuunda timu ya Taifa hauoni haja au hauoni sababu kwamba sasa kocha wa timu ya Taifa kuweza kudhuru ligi zote mbili ili kupata wachezaji wazuri?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; zamani kulikuwa kuna ligi kuu ya Muungano kwa maana ya *Super Cup* ligi ile iliweza kutoa timu bora na timu nyingi ambazo zilishiriki ligi ile iliweza wachezaji wa timu ya *Taifa Stars*. Sasa je, Serikali ina mkakati gani kuweza kurudisha kombe hili? Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kunipa nafasi nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Suleiman kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Suleiman amependa kufahamu kwamba katika kuandaa timu za Taifa; je, si vyema timu hizi zikaandaliwa kwa kufatilia ligi zote mbili za *TFF* pamoja na *ZFF*.

Mheshimiwa Spika, hili ni dhahiri kwamba tunapochagua wachezaji wa timu ya Taifa kocha hakatazwi kwenda popote kwenye hizi ligi ndani ya Taifa letu na hili limekuwa likifanyika ndio maana wachezaji katika timu yetu ya Taifa wanatoka pia kwa upande wa Zanzibar pamoja na upande wa Bara. *(Makofi)*

Kwa hiyo hili tutaendelea kuimarisha tukishirikiana na *ZFF* pamoja na *TFF* ili kuhakikisha kwamba tunapata wachezaji wazuri na hata katika benchi la ufundi tumekuwa tukiwahusisha wenzetu wa Zanzibar kuhakikisha pia wanatoa mchango na wanakuwa sehemu ya ligi yetu na timu yetu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili amependa kufahamu tulikuwa na ligi ya Muungano sasa anapenda kufahamu ni ligi hii itarudishwa? Nijibu hili kwamba jambo hili sisi kama Wizara pia tumeliona. Tumekuwa sasa na mazungumzo kati ya *BMT*, *TFF* pamoja na *ZFF* kuhakikisha kwamba ligi hii inarudishwa.

Mheshimiwa Spika, mwanzoni ilisitishwa kwa sababu Zanzibar ilipata *associate membership* kwa *CAF* wakawa wanapeleka timu zao mbili na huku Bara pia wakawa wanapeleka pia timu zao mbili. Lakini kwa afya ya Muungano wetu, kwa afya ya mashirikiano tuliyonayo kama Taifa tumekubaliana na kamati imeshaundwa ligi hii itarudishwa hivi karibuni tunaangalia tu tathmini na gharama kwamba gharama zitakuwaje, lakini itarudishwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abbas Tarimba swali fupi.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri anasema moja ya kigezo cha wachezaji kuteuliwa katika timu ya Taifa ni kupata muda wa kutosha kwa maana ya *play time* katika ligi za juu kwa maana ya *premier na first division*. Wachezaji wa Tanzania wanapata vipi nafasi kiasi hicho wakati ligi zetu zimejaa wageni walio wengi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo majibu.

**13 SEPTEMBER, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kunipa nafasi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tarimba Abbas kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba hili ni la msingi, lakini sisi tuna *limitation* ya usajili wa wachezaji wa nje katika timu. Hata wanapocheza wanapoingia uwanjani kocha anazingatia pia kuna uwakilishi wa vijana wetu katika mechi hiyo ya siku hiyo. Tutaendelea kulizingatia na tutaendeleo kushauri *TFF* wahakikishe pamoja na kwamba wamesajili wachezaji kutoka nje kwa *limit* ile ambayo tumewapa kupitia *BMT* vijana wetu wanapata nafasi wacheze waoneshe vipaji vyao, asante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Mheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Profesa Patrick Aloyce Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 13

### **Ruzuku ya Pembejeo kwa zao la Kahawa**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itarejesha utoaji wa ruzuku ya pembejeo za dawa kwa wakulima wa kahawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukua kwa teknolojia ambako kumewezeshwa kugunduliwa kwa miche chotara ya kahawa ambayo ina ukinzani na magonjwa makuu ya kahawa ya kutu ya majani na Chole Buni, Serikali inaendelea kutekeleza mkakati wa kuzalisha miche bora ya kahawa milioni 20 yenye ukinzani mkubwa wa magonjwa na ambayo hutolewa kwa ruzuku kupitia Taasisi ya Utafiti *TaCRI* na Bodi ya Kahawa Tanzania.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini pamoja na majibu hayo ni ukweli usiofichika kwamba changamoto kubwa kwa uzalishaji wa kahawa ni hayo magonjwa uliyoyataja na mbegu zilizozalishwa bado hazijaweza kupambana na hayo magonjwa mia kwa mia.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuanzisha mfuko wa maendeleo ya kahawa ili wakulima waweze kupata pesa za kununua pembejeo wapambane na magonjwa haya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili je, kwa kuwa tumehamasisha sana uzalishaji wa kahawa, Serikali haioni pia ni muhimu kuanzisha programu za kuboresha mifereji ya asili ili wakulima waweze kupata maji ya kumwagilia kahawa zao? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Profesa Patrick Aloyce Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza sisi tunaona Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo ambao tumeutamka katika bajeti yetu unatosha kwa ajili ya kushughulikia mazao yote. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba zao la kahawa pia ni kati ya mazao ambayo yanashughulikiwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo na hivi sasa utaratibu ambao unaendelea ni kutenga kila shilingi mia moja kwenye zao la kahawa aina ya robusta na shilingi mia mbili kwa arabica kwa ajili ya kuchangia katika mfuko huu, kwa hiyo mwisho wa siku pia utakwenda kuhudumia zao la kahama.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza sisi tunaoa Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo ambao tumeutamka katika bajeti yetu unatosha kwa ajili ya kushughulikia mazao yote, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba zao la kahawa pia ni kati ya mazao ambayo yatashughulikiwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo, hivi sasa utaratibu ambao unaendelea ni kutenga kila Shilingi 100 kwenye zao la kahawa aina ya robusta na Shilingi 200 kwa arabica kwa ajili ya kuchangia katika mfuko huu. Kwa hiyo, mwisho wa siku pia, utakwenda kuhudumia zao la kahawa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mifereji, nakubaliana na wewe Profesa nami nimefika katika baadhi ya mashamba katioka Mkoa wa Kilimanjaro, hilo tumelichukua tunaendelea kulitekeleza, tutalifanyia kazi ili mwisho wa siku liweze kuleta tija kwa wakulima wetu. *(Makofi)*

**13 SEPTEMBER, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Swali langu ni fupi. Je, Serikali itatumia mkakati gani na ni lini itanza kugawa hizo mbegu mnazosema tutagawiwa za ruzuku za miche ya kahawa kwa sababu muda unakwenda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kimei, Mbunge, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, zoezi la ugawaji wa miche chotara linaendelea na tumeshagawa katika Mikoa ya Kagera, Mbeya, Songwe pamoja na Mkoa wa Kilimanjaro, pia hata Mheshimiwa Ndakidemi ni shahidi katika eneo lako miche hii imeshagawiwa. Zoezi ambalo tunaenda nalo ni kuhakikisha kwamba, tunazalisha kwa wingi ifikie miche Milioni 20 ili tuweze kubadilisha ile mibuni iliyokaa muda mrefu tui-replace na hii mipya ili kuondokana na changamoto ambayo wakulima wengi wanaipata.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Je, Serikali haioni kwamba, umefika wakati sasa wa kuwekeza kwenye uzalishaji wa mazao ya choroko na dengi kwa kutoa pembejeo na mafunzo kwa wakulima badala ya ambavyo sasa Serikali imewekeza zaidi kwenye kusimamia mauzo badala ya kusimamia uzalishaji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kasalali Mageni, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Kasalali kwa namna ambavyo amekuwa akiyasimamia mazao haya, hii ni hoja yake ambayo amekuwa akiisema mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie mbele ya Bunge hili ya kwamba, tutaendelea kuyapa kipaumbele mazao yote, katika maoni na ushauri ambao Mheshimiwa Mbunge ameusema tumeupokea tutakwenda kuufanyia kazi ili mwisho wa siku wakulima wa choroko na dengi pia walime kwa tija na masoko ya uhakika wayapate pia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhata, swali la nyongeza.



**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, msimu wa korosho unaanza mwezi wa Kumi. Je, Serikali haioni haja ya kuweka bei dira kwa zao la korosho kama ilivyo mazao mengine kama pamba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Yahya Mhata, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha wadau tulichokifanya katika Manispaa ya Songea, katika kikao hiki mwongozo uliotolewa na ambao pia Serikali tunausimamia ni kwamba, utaratibu wa zamani wa bei ya korosho utaendelea ambapo ni utaratibu ule wa kulaza sanduku na baada ya hapo bei itakwenda kutangazwa ili mwisho wa siku wakulima waweze kuipata bei yao katika ufunguzi wa sanduku lile. Kwa hiyo, yale ambayo tulikubaliana na wadau na Waheshimiwa Wabunge pia walikuwepo ndiyo sehemu ya utekelezaji ambao Serikali tutausimamia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 14

### **Kushirikiana na Sekta Binafsi katika Kilimo cha Umwagiliaji**

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE** aliuliza:-

Je, ni kwa nini Serikali ishirikishe sekta binafsi katika kilimo cha umwagiliaji ili kutimiza Ajenda 1030?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Mwijage, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika utekelezaji wa miradi yake mbalimbali katika sekta ya kilimo, imeendelea kushirikiana bega kwa bega na sekta binafsi. Kwa muktadha huo, katika miradi ya umwagiliaji ambayo Serikali inatekeleza kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea kuishirikisha sekta binafsi katika hatua mbalimbali za miradi hiyo ili kufikia malengo ya Agenda 10/30. Aidha, katika mwaka 2022/2023 Serikali imepanga kukarabati na kujenga

miundombinu ya umwagiliaji katika eneo la hekta 95,000, ambapo jumla ya kandarasi 55 zimetolewa kwa sekta binafsi. Mpaka hivi sasa jumla ya mikataba 21 ya Wakandarasi imesainiwa na Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Mwijage, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na kwamba, sasa Tanzania ni soko la chakula, naomba Serikali itueleze kasi ya Serikali katika kuwekeza kwenye umwagiliaji kwa kutumia sekta binafsi katika mito ambayo ina maji yasiyokauka, mito kama mabonde ya Kagera, *basin* ya Viktoria, Ruvuma na maziwa yetu? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Katika maelezo ya hizo hekta 95,000 zinazozungumzwa naomba Serikali inihakikishie hekta 11,000 za Mto Ngono na zenyewe zimo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Charles Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, katika Jedwali la Sita katika Kitabu cha Bajeti iliyosomwa na Waziri wa Kilimo limeelezea mabonde 22 ambayo Serikali imeamua kuyafanyia upembuzi yakinifu na usanifu ili mwisho wa siku nchi yetu kuanzia Mashariki, Magharibi, Kusini na Kaskazini yote tufanye kilimo cha umwagiliaji. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, mpaka hivi sasa ninavyozungumza tayari kazi hii imekamilika na tuko katika hatua za kuwapata Wakandarasi kwa ajili ya kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika maeneo yote hayo mabonde yale makubwa, yaani kuanzia Bonde la Ziwa Viktoria, Malagarasi, Mto Manonga, Ifakara, Idete, Mto Songwe, Rufiji *Basin* Kwenda mpaka Mkoazi maeneo yote haya tutayagusa. Lengo letu ni kufanya kilimo cha umwagiliaji na mwisho wa siku tufikie malengo ambayo tumejiwekea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu Mto Ngono, kwenye hili la Mto Ngono nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ambaye amekuwa akilisimamia sana jambo hili, katika yale mabonde 22 ambayo tunayafanyia upembuzi yakinifu na usanifu, Mto Ngono pia upo. Kwa hiyo, ekari zile 11,000

**13 SEPTEMBER, 2022**

zitakuwepo kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge suala la Mto Ngoni tumelichukulia katika umakini mkubwa sana. (Makofi/Kicheko)

**SPIKA:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Mheshimiwa Amina Daudi Hassan, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 15

### **Elimu Kuhusu Kuepuka Ndoa za Siri Nchini**

**MHE. AMINA DAUDI HASSAN** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kutoa elimu kwa Wanawake kuepuka ndoa za siri ambazo zina changamoto ya malezi ya familia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, majibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Daudi Hassan, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa ndoa ni Taasisi muhimu katika kuimarisha haki na ustawi wa familia. Hivyo, Serikali kupitia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/2018 hadi 2021/2022 eneo namba nne linalohusu malezi na mahusiano ya familia imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu malezi chanya na mahusiano ndani ya familia ili kuwa na familia inayozingatia maadili mema.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ipo kwenye hatua za mwisho za kukamilisha Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji, Usimamizi na Uratibu wa Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa na Familia ambao utasaidia kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuzingatia taratibu za ufungaji wa ndoa pamoja na kuyajengea mabaraza ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia uwezo ili kuendelea kutoa elimu katika jamii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Daudi Hassan, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA DAUDI HASSAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali moja la nyongeza.

**13 SEPTEMBER, 2022**

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali italeti marekebisho ya Sheria ya Ndoa ili iweze kupunguza changamoto ya ndoa za siri na za utotoni? (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, majibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amkina Daudi Hassan, kuhusu Sheria ya Ndoa na Marekebisho yake.

Mheshimiwa Spika, wiki ijayo Kamati ya Maendeleo ya Jamii pamoja na Kamati ya Sheria na Katiba zinaketi kikao kwa ajili ya kufanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa. Hivyo, basi tumepokea hoja yake, tunaenda kuwasilisha tujumuishe ili vijadiliwe pamoja. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sheria za ndoa, lakini kuna tatizo kubwa sana la malezi kwa watoto wetu. Kuna changamoto kubwa sasa hivi ya wazazi kuwapeleka watoto wadogo kuanzia *nursery school* mpaka sekondari katika shule za *boarding* na watoto kukosa malezi ya wazazi. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha sasa mitaala inarudishwa kwa mfano ile ya sayansikimu katika shule zetu ili watoto waweze kupata malezi na kupata elimu za kujitegemea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, majibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati la nyongezab kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumepokea hoja yako. Ni kweli, kuna kasi kubwa ya mmomonyoko wa maadili inayoendelea na inasababisha masuala mengi sana ya visa vya ukatili. Kwa sababu marekebisho ya mitaala yanaangukia sekta nyingine tumelipokea tutakwenda kukaa tulijadili kwa pamoja, tujange hoja tuone namna gani tunaweza tukafanya ili kurekebisha hiyo mitaala ikidhi na kuakisi changamoto za sasa kwa ustawi wa Taifa letu la kesho.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru sana kwa majibhu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Mheshimiwa Ng'wasi Damasi Kamani, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 16

**Mkakati wa Kuhakikisha Vijana Wanaajiriwa Nje ya Nchi**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutumia Balozi zetu kuhakikisha Vijana wengi wa Kitanzania wanaajiriwa nje ya nchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ng'wasi Damasi Kamani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mkakati maalum wa kuhakikisha kuwa vijana wa Kitanzania wenye sifa zilizowekwa wanapata fursa za ajira nje ya nchi kama ifuatavyo:-

i) Balozi zetu nje ya nchi zimeendelea kutafuta fursa za ajira mbalimbali kwenye maeneo yao ya uwakilishi kwa kuingia mikataba ya ajira nje ya nchi inayowawezesha vijana wetu kupata ajira na kuwahakikishia usalama na maslahi yao katika ajira hizo.

ii) Serikali kupitia Kanzi Data ya Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TAESA) inawawezesha vijana na wataalam mbalimbali kujiandikisha ili kuwasadia kuomba nafasi za ajira pindi zinapopatikana nje ya nchi.

iii) Wizara inafuatilia nafasi za ajira ambazo hutangazwa katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa na kuziwasilisha katika mamlaka mbalimbali ili kusaidia kuwatambua vijana ambao wanazo sifa kutoka Serikalini na Sekta Binafsi na kuwashawishi kuomba nafasi hizo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ng'wasi Damasi Kamani, swali la nyongeza.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Hivi karibuni nchi jirani ya wenzetu imeingia makubaliano na nchi za uingereza za kupeleka wataalam wa afya vijana kwa ajili ya kufanya kazi kule. Majibu ya Serikali ni mazuri, lakini matokeo yake hayaridhishi. Ni lini hasa Serikali itaona haja ya kuja na mikakati mbadala ya kuhakikisha inatumia Balozi zetu tulizonazo katika nchi zaidi ya 25 na Balozi Ndogo kwenye nchi zaidi ya 15 kuhakikisha inaongeza mawanda ya vijana kupata ajira? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mheshimiwa Rais wa nchi yetu, Mama Samia Suluhu Hassan amekuwa akifanya juhudi kubwa sana za kuhakikisha anapanua mawanda ya mahusiano ya Kimataifa kwa nchi yetu katika nchi za Kimataifa, lakini takwimu zinaonesha kwamba, vijana wachache sana wanapata nafasi za ajira kwenye nchi jirani. Serikali je, inalitambua hili? Na kama inalitambua ni lini hasa itaanza kuchukua hatua ili kuhakikisha juhudi za Mheshimiwa Rais zinapata tija ya ajira kwa vijana? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna haja ya Serikali yetu kuongeza juhudi katika kuhakikisha kwamba, vijana wetu wanapata fursa za ajira nje ya nchi. Miongoni mwa mbinu hizo ni kuhakikisha kwamba, tunaingia mikataba na nchi mbalimbali ili kuhakikisha kwamba, fursa zilizopo huko zinapatikana.

Mheshimiwa Spika, mfano hivi sasa tayari tumeshaingia mkataba na nchi ya Qatar mwezi uliopita tu ujumbe mkubwa wa Tanzania ulikwenda Doha mahsusi kwa ajili ya kufuatilia mkataba huo. Katika makubaliano yao tayari nchi ya Qatar imekubali kufungua *Visa Centre* hapa Tanzania maalum kwa ajili ya vijana wa Tanzania kwenda kufanya kazi Qatar. Pia tumeanza mazungumzo na nchi za Falme za Kiarabu na Oman na Saudi Arabia kwa ajili ya kuingia nao mkataba. Hii mikataba ni muhimu sana kwa sababu ndiyo inayotupa uhakika wa kupata hizo ajira.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kwamba, Serikali imeona kuna umuhimu mkubwa sana wa vijana wetu kupata ujuzi kabla ya kwenda kufanya kazi nje ya nchi. Hivyo basi, kupitia *TAESA* ambao ni wakala maalum wa taasisi

**13 SEPTEMBER, 2022**

ya ajira hapa Tanzania, imeanzisha kanzi data na ina *portal* maalum ili vijana waweze kujiandikisha mara zinapotokea fursa za ajira waweze kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tayari *portal* hiyo ina vijana wanaofika 40,000 na umuhimu wake ni kwamba, hao vijana kabla ya kwenda kufanya kazi nje ya nchi huwa wanapewa mafunzo maalum ili kuhakikisha kwamba, wanapokwenda huko nje hawaharibu katika kazi ambazo wamepelekewa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, sasa aulize swali lake.

Na. 17

### **Kumaliza Ujenzi wa Chuo cha VETA – Mkinga**

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA** aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa Chuo cha VETA unaoendelea Wilayani Mkinga utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Sayansi na Teknolojia, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kukamilika kwa Chuo cha VETA cha Wilaya ya Mkinga pamoja na vyuo vingine ili viweze kutoa mafunzo yatakayowawezesha vijana wetu kujajiri na kuajiriwa. Kwa sasa ujenzi wa Chuo hiki upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji ambapo ujenzi umefikia asilimia 95. Ujenzi wa Chuo hiki unatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Disemba, 2022. Hivyo, Chuo hiki kinatarajiwa kuanza kutoa mafunzo ya muda mfupi kuanzia mwezi Oktoba, 2022 na mafunzo ya muda mrefu mwezi Januari, 2023. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dunstan Kitandula, swali la nyongeza.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyozungumza chuo hiki hakina mkufunzi hata mmoja wala hakina Mkuu wa Chuo. Wakufunzi wanaotegemewa ni kutoka Chuo cha VETA Tanga ambacho na chenyewe kimeelemewa, kinategemewa chuo hichohicho cha Tanga kitoe wakufunzi kwenda Korogwe. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kuhakikisha kinapata wakufunzi ili hayo malengo ya kuanza mwezi wa Kumi yaweze kutimia? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Hivi tunavyozungumza vifaa vya ufundi havijapatikana kwenye vyuo hivi vya Mkinga wala Korogwe. Serikali ina mkakati gani wa haraka kuhakikisha vifaa hivi vinapatikana ili mafunzo yaweze kufanyika? (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba sasa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kitandula Mbunge wa Mkinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri ni kweli tuna upungufu wa walimu kwenye vyuo vyetu hivi vya VETA hivi sasa tuna Wilaya 77 zenye Vyuo vya VETA vya Wilaya pamoja na mikoa. Lakini nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 Wizara imepata kibali cha kuajiri walimu zaidi ya 514. Kwa hiyo, tayari mchakato huu wa kuajiri walimu uko kwenye hatua za mwisho na tutahakikisha sasa miongoni mwa walimu hawa 514 tunaokwenda kuwaajiri basi waweze kwenda kwenye Chuo cha Mkinga lakini pamoja na vile vyuo 25 vya Wilaya pamoja na vyuo vile vinne vya mikoa ambavyo sasa nakamilisha ujenzi wake.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la pili amezungumzia suala la vifaa vya kufundishia; ni kweli mchakato wa vifaa unaendelea kwa sababu upo kwenye bajeti 2022/2023 ambao tumeanza kuutekeleza hivi sasa na tuko katika *quarter* ya kwanza. Kwa hiyo, pindi fedha zitakapokuwa zimekaa tayari tunakwenda kununua hivyo vifaa na kuvipeleka kwenye vyuo hivi ambavyo tayari vimekamiliwa, lakini upande wa samani zote za vyuo vyote 25 viko tayari kwa ajili ya kupelekwa katika maeneo haya nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Asya Mwadini Mohammed, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.



Na. 18

**Viwanda vya Kuchakata Taka Ngumu**

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED** aliuliza:-

Je, kuna viwanda vingapi vya kuchakata taka ngumu nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asya Mwadini Mohammed, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Tanzania hadi sasa tuna jumla ya viwanda 137 vya kuchakata taka ngumu hapa nchini. Viwanda hivyo vimegawanyika katika makundi manne ambayo ni viwanda vinavyotumia taka zitokanazo na chuma viko 16; viwanda vinavyotumia taka za plastiki viko 70; viwanda vidogo vya kutengeneza mkaa mbadala kutoka kwenye mabaki ya kilimo viko 50; na tuna kiwanda kimoja cha kutengeneza mbolea aina ya mboji inayotokana na mabaki ya vyakula. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asya Mwadini, swali la nyongeza.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa mujibu wa majibu ya Mheshimiwa Waziri ni dhahiri kwamba Tanzania hakuna kiwanda kinachochakata vigae na ukizingatia vigae vingi tunaingiza kwanza chupa za pombe na mengineyo, lakini tunazalisha na hapa nchini maana yake uchafuzi wa kimazingira unaendelea. Nini mkakati wa Serikali kuanzisha kiwanda cha kuchakata vigae nchini?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; je, Serikali haioni sasa kupunguza kodi kwa bidhaa zote zinazochakatwa na taka ngumu ili kuweza kuwavutia wawekezaji waweze kuwekeza nchini lakini pia na kuyalinda mazingira yetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara majibu.

**13 SEPTEMBER, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Asya Mwadini Mohamed Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli bado hatuna viwanda vya kuchakata vigae kwa maana ya mabaki, lakini nia ya Serikali ni kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia wawekezaji ambao tunaamini wataendelea kuwekeza katika maeneo tofauti ikiwemo hili ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja, kwa hiyo tunaendelea kutafuta na kuweka kuwavutia wawekezaji katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni kweli Serikali tunaendelea kufanya juhudi na kuona namna ya kuweka vivutio maalum katika maeneo mbalimbali ikiwemo hili la kupunguza kodi katika maeneo ya uchakataji au urejeshaji taka ambazo kwa kweli zinaharibu sana mazingira hapa nchini. Kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira tunaendelea na juhudi za kuhakikisha tunatunza mazingira kwa kuvutia wawekezaji wanaopunguza taka ambazo zimezagaa mjini nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, Mbunge wa Korogwe Mjini sasa aulize swali lake.

Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, Mbunge wa Mahonda sasa aulize swali lake.

Na. 20

### **Kampuni ya Uber Kusitisha Huduma zake Nchini Tanzania**

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI** aliuliza:-

Je, Serikali imechukua hatua gani kutatua changamoto zinazoelezwa za ukiritimba zilizopelekea Kampuni ya Uber kusitisha huduma zake nchini Tanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandishi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu :-

**13 SEPTEMBER, 2022**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, Mbunge wa Mahonda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ilianza kudhibiti huduma za *taxi* mtandao mwezi Mei, 2020 kwa kutumia Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini Na. 3 ya mwaka 2019 pamoja na kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, baada ya LATRA kuanza kudhibiti eneo hili kisheria, iliweka viwango vya tozo kwa huduma za *taxi* ili kupunguza migogoro kati ya madereva na wamiliki wa mifumo ya *taxi* ambao ni pamoja na Kampuni ya Uber. Kutokana na hatua ya LATRA kuweka tozo katika huduma za *taxi* mtandao, Kampuni ya Uber iliamua kusitisha kutoa baadhi ya huduma hapa nchini mwezi Aprili, 2022.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia LATRA inaendelea na mazungumzo na Kampuni ya Uber kwa lengo la kuhakikisha inarejesha huduma za *taxi* mtandao. Ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majawabu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Uber inachangia kwa kiasi kikubwa sana ajira nyingi za vijana; je, Serikali haioni kwamba ajira ya vijana ina mchango chanya zaidi kushinda hizi tozo ndogo ambazo Serikali imeziweka?

Swali la pili; kwa kuwa Uber ni kampuni ya teknolojia na siyo kampuni ya usafiri, Uber ulimwengu mzima haina gari hata moja, inawezesha watu wenye magari kuweza kufanya biashara ya usafiri wa *taxi* kirahisi na kwa kuhuda nafuu.

Je, taasisi ya LATRA (Mdhhibiti wa Magari ya Ardhini) ni taasisi sahihi kufanya majadiliano na kampuni ya Uber? Ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante napenda kujibu mawali mawili kwa pamoja ya Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, Mbunge wa Mahonda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba Uber pamoja na mashirika mengine ambayo yalikuwa yanatoa huduma za *taxi* mtandao yanatoa ajira kubwa kwa vijana, lakini pia yanatoa huduma kwa wasafiri. Kilichopelekea kusitisha huduma kwa kampuni hii ya Uber na Bolt ilikuwa ni baada ya LATRA kuona uwezekano wa wao kupunguza kamisheni ambapo walikuwa wanatoa zaidi ya asilimia 25 na kukawa kuna malalamiko ya wamiliki wa *taxi* ambapo waliona kamisheni ile sasa hawafanyi kazi vizuri ndiyo maana wakasimama.

Kwa hiyo ilikuwa ni kuona ni namna gani wamiliki wa *taxi* watapata faida lakini wamiliki wa haya makampuni ya *taxi* mtandao watapata faida, lakini pia bila kumuumiza abiria.

Mheshimiwa Spika, tarehe 5 mpaka 8 Septemba, 2022 LATRA, wamiliki wa hizi *taxi* pamoja na wasafirishaji wengine wamekaa na wamekubaliana kupata muafaka na kabla ya mwisho wa mwezi huu Serikali itatoa taarifa maana kumekuwa na mazungumzo mazuri ili kuwa na *win win situation* kwa msafiri, mwenye *taxi* lakini na kampuni hizi ambazo zinasimamia huu usafiri wa *taxi* mtandao, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri hebu tusaidie, ni wale wenye magari ndiyo waliolalamika na kwa hivyo kwa sababu kama yeye ndiyo anayelalamika si angejiondoa tu yeye Uber ili Uber iendelee kufanya kazi kama yeye ndiye aliyelalamika? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, wenye *taxi* ndiyo ambao wanafanya usafirishaji waliona kwamba kwa kufanya ile biashara hawapati faida, na kazi ya LATRA ni kufanya *regulation* kwamba wasije wakapata hasara na hata wakisimamisha maana yake tayari hiyo huduma itakuwa imekosekana.

Kwa hiyo, wamekaa pamoja ili kuona kampuni zinazosimamia hizi *Uber* zinaendelea kufanya biashara, lakini pia wale wamiliki wa magari wanapata faida na wale wasafiri hawaumizwi na ndiyo maana bado makampuni mengine na hasa ya wazawa yameendelea kutoa hiyo huduma kwa asilimia ambazo LATRA waliona zinafaa asilimia 15 kwa maana ya kamisheni, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimetaja swali la Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, Mbunge wa Korogwe Mjini sasa litaulizwa na Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

**Hitaji la Bandari Kavu Eneo la *Old Korogwe***

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA K.n.y. MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga bandari kavu eneo la *Old Korogwe* katika Halmashauri ya Mji Korogwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, Mbunge wa Korogwe Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa bandari kavu hufanyika ili kuongeza ufanisi wa bandari zilizopo mwambao wa bahari na maziwa. Ujenzi wa bandari kavu huzingatia vigezo maalum ikiwa ni pamoja na kuondoa msongamano katika bandari iliyo karibu na bandari kavu na kusogeza huduma karibu na watumiaji wa mwisho. Aidha, kigezo kingine ni uwepo wa upembuzi yakinifu unaobainisha mahitaji ya bandari kavu husika ili kuwa na msingi wa kufanya maamuzi sahihi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo, eneo la *Old Korogwe* halijabainishwa kwa sasa kwamba linafaa kujengwa bandari kavu. Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari itafanya tathmini kuona umuhimu wa uwepo wa bandari kavu katika eneo la *Old Korogwe*. Ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru pamoja na majibu ya Serikali naomba kuuliza swali dogo moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kazi kubwa sana iliyofanywa na Serikali ya kuboresha bandari ya Tanga na kwa sababu bandari ya Tanga kuwa na eneo dogo, ujenzi wa bandari kavu kwenye eneo la Korogwe ni jambo muhimu sana. Ni lini sasa Serikali itafanya hiyo tathmini ili kuwezesha bandari kavu kwenye eneo la Mji wa Korogwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**13 SEPTEMBER, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):**  
Mheshimiwa Spika, ahsante napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kwa sasa Serikali inaboresha na imewekeza sehemu kubwa sana kuboresha bandari ya Tanga ili kuweza kupokea mizigo na kusafirisha mizigo mingi. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi tulikuwa bado eneo la Korogwe halijabainishwa kuwa eneo la kujenga bandari kavu, na ndiyo maana Serikali imesema baada ya kupata hilo wazo la Mheshimiwa Mbunge ambaye kazi yake kubwa pia ni kuishauri Serikali tumelichukua na tutafanya tathmini ili tuone kama eneo hilo litafaa kujenga bandari kavu ambayo itakuwa na tija na endelevu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali na niwashukuru sana Serikali kwa kuleta majibu ya msingi ambayo ni mafupi na yanaenda na wakati. Kwa hiyo nawashukuru sana kwa ushirikiano huo, lakini pia Wabunge waliopata fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza wale wa mwanzo mwanzo wamejitahidi sana kwa hiyo nawapongeza sana na kuwashukuru kwa kuokoa muda hawa wa mwisho kidogo ilikuwa changamoto na nikaona leo ni siku ya kwanza, kwa hiyo watu kidogo twende nao.

Lakini mtagundua katika hiki kipindi cha saa moja na nusu ya maswali muda umepita kidogo pale kwa sababu leo tulikuwa na ratiba nyingine maana ni siku ya kwanza, lakini tutajitahidi kufanya maswali 20 ndani ya saa moja na nusu, kwa hiyo, mtagundua waliopata maswali ya ziada ni wachache siku ya leo ni kwa sababu maswali ya msingi ni mengi na niwasihi Waheshimiwa Wabunge mpeleke kwa Katibu maswali ya msingi, kwa sababu maswali ya nyongeza yataendelea kuwa machache.

Kwa hiyo, mtu kama anayasubiria hayo asikasirike humu ndani akinyimwa swali na Mwenyekiti ama Spika asipompa nafasi asilalamika kwa sababu tunatarajia tupate maswali ya msingi kutoka kwenye maeneo yenu ya uwaklishi.

Ninalo tangazo la wageni walioko Bungeni hapa siku ya leo, kwanza tutaanza na wageni wa Bunge ambao ni viongozi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu yupo Dkt. John Jingu ambaye ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu karibu sana; yupo pia Ndugu Kaspar Kaspar Mmuya ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, karibuni sana. *(Makofi)*

**13 SEPTEMBER, 2022**

Waheshimiwa Wabunge hawa ndiyo wageni wa Bunge.

Lakini pia wapo wageni wa Bunge wengine ambao wako Jukwaa la Spika, kundi la kwanza la wageni hawa ni Wabunge kutoka Bunge la Uganda na hapa tutaanza na Mheshimiwa Mapuuga Mathias ambaye ni Kiongozi wa Upinzani Bungeni Uganda, karibu sana. *(Makofi)*

Lakini pia yupo Mheshimiwa Nambeshe John ambaye yeye ni *Chief Whip* wa *Opposition* Uganda, karibu sana. *(Makofi)*

Sasa nimeona niite hivyo kwa kiingereza maana inawezekana ukisema mnadhimu hajui, lakini yeye ni Mnadhimu Mkuu wa Upinzani Uganda. Lakini yupo pia Mheshimiwa Dkt. Kamara Nicholas, yeye ni Mbunge karibu sana; yupo pia Mheshimiwa Juliet Nakabuye naye ni Mbunge karibuni sana; yupo pia Mheshimiwa Lutaaya Geofrey naye ni Mbunge karibu sana; yupo pia Mheshimiwa Sebamala Richard naye ni Mbunge karibu sana; yupo pia Mheshimiwa Kabuye Frank naye ni Mbunge karibu sana; wao wameambatana na Ndugu Nakawunde Ruth ambaye ni Katibu wa msafara, karibuni sana wageni wetu kutoka Uganda wamekuja hapa kwetu kwa ajili ya kujifunza mambo mbalimbali na naamini watapata fursa ya kuonana nanyi Wabunge na mimi nitaonana nao hapo baadaye. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wa Bunge kutoka Bunge la Ghana ambao ni Mheshimiwa Andrew Amoako ambaye ni Mbunge na huyu ni Naibu Spika wa Pili na pia ni kiongozi wa msafara, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia *Mrs. Rosemary Sarkodie* ambaye huyu ni Mkuu wa Idara ya Mambo ya Mahusiano kwenye Bunge la Ghana, karibu sana; yupo pia Ndugu Esther Donkor ambaye yeye ni Katibu Tawala wa Bunge; yupo pia Ezekiel Birikorang ambaye yeye ni Msaidizi wa Bunge huko, lakini pia yupo Nathaniel Acquah ambaye yeye ni msaidizi kwenye upande wa ulinzi, karibu sana. *(Makofi)*

Karibuni sana wageni wetu lugha zetu rasmi humu ndani ni Kiswahili na Kiingereza sasa kwa sababu Kiswahili hata majirani zetu hapo Waganda kidogo wanapata changamoto, *I would like to take this opportunity to welcome the two delegations to our Parliament. We are very glad to receive you and you all welcome, I believe you will have an opportunity to meet one or two members of parliament and I will see you in the course of the day today, so good to see you.*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni tisa na hawa wanatambulishwa maalum kabisa kwa sababu ni wageni wa Mheshimiwa Mbunge ambaye ameapishwa leo.

**13 SEPTEMBER, 2022**

Wageni tisa wa Mheshimiwa Tamima Haji Abass ambao ni familia yake kutoka Kaskazini Unguja, Zanzibar wakiongozwa na mume wake Ndugu Shukrani Seif Salum, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Sasa hapo wengine mkae halafu abaki mume wa Mheshimiwa Mbunge tumuone vizuri, mume wa Mheshimiwa Mbunge haya, karibu sana shemeji yetu. *(Makofi)*

Lakini pia wapo wageni wa Wabunge mbalimbali ambao wametembelea siku ya leo Bungeni hapa kwa ajili ya kujifunza mambo mbalimbali; wageni wa Wabunge wote wasimame kwa pamoja. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao pia wachungaji 67 kutoka Chuo cha *Assemblies of God Central Bible College* kilichopo Jijini Dodoma, hawa wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wachungaji karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hawa ndiyo wageni tulionao na haya ndiyo matangazo niliyokuwa nayo. Kwa hivyo, tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

### **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

#### **Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2002 (The Disaster Management Bill, 2022)**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaenda huko nimemuona Mheshimiwa Abdullah Mwinyi amesimama.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ABULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nasimama kwa Kanuni ya 76 kuomba Mwongozo.

Mheshimiwa Spika, hapo mapema baada ya kujibiwa swali langu la msingi niliuliza maswali ya nyongeza mawili. Moja likajibiwa vizuri, lakini la pili halikujibiwa naomba Mwongozo wako.



**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Abdullah Mwinyi akiomba Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 76 akieleza kwamba alikuwa ameuliza maswali ya nyongeza mawili na anasema swali la pili halijajibiwa, limejibiwa swali moja.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu zinataka maswali yajibiwe kikamilifu. Kanuni zetu zinataka maswali yajibiwe kikamilifu sasa kwa sababu sina hakika sana kama swali lilijibiwa ama halikujibiwa ili nitoe fursa kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kulijibu hilo swali la nyongeza, basi nitaenda kutazama Taarifa Rasmi za Bunge maswali yaliyoulizwa na majibu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri ili kama hilo la pili alikuwa amelisahau basi tutampa fursa ya kulijibu wakati mwingine. Kwa hiyo, huo ndiyo Mwongozo wangu. Ahsante sana.

Sasa Katibu alikuwa ameshasoma jambo ambalo linafuata na ametueleza kwamba kinachofuata hapo ni Muswada wa Sheria na sasa nitumie fursa hii kumuita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu Mheshimiwa George Simbachawene Mwatawaguluvala. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 1 wa mwaka 2022, kama ulivyorekebisha kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho, sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote afya njema na kutuwezesha kuhudhuria Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Nane wa Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa ninamshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukubali itungwe Sheria ya Usimamizi wa Maafa nchini. Aidha, nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yao na maelekezo muhimu ambayo yamekuwa dira wakati wote katika kufanikisha azma ya Serikali ya kuwa na sheria itakayoweka mfumo imara na madhubuti wa usimamizi wa maafa.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya katika kuliongoza Bunge letu. Miongozo yenu imetuwezesha waheshimiwa Wabunge kutekeleza majukumu yetu kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, naishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb), na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb), pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi kubwa ya kuchambua na kutoa maoni na mapendekezo yaliyosaidia sana kuboresha maudhui ya Muswada huu wa Sheria inayopendekezwa kutungwa na Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kumshukuru sana msaidizi wangu Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga (Mb), Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa mchango wake mkubwa katika kufanikisha Muswada huu. *(Makofi)*

Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhiti kwa Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama (Mb) na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mheshimiwa Balazi Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb), Waziri wa Maliasili na Utalii ambao wote kwa vipindi tofauti walishiriki kikamilifu na kwa weledi mkubwa katika maandalizi ya Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana viongozi na wataalam wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu wakiongozwa na Dkt. John Jingu, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu na Naibu Katibu Mkuu, Bwana Kaspar Kaspar Mmuya kwa kufanya kazi bila kuchoka wakati wa uandaaji wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa namna ya pekee nitumie fursa hii kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi na timu yake ya wataalam kwa kufanya kazi bila kuchoka wakati wa uandaaji wa Muswada huu, na kwa namna ya pekee nimshukuru sana Mwandishi Mkuu wa Sheria Ndugu Onorius Njole kwa ushiriki wake wa moja kwa moja wakati wote na hata wakati wa Kamati tukiandaa sheria hii mpaka tunafika hatua hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naomba kuwashukuru sana wadau wote wa usimamizi wa maafa waliopata fursa ya kutoa maoni yao ambayo yalisaidia sana kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Ofisi ya Waziri Mkuu inalo jukumu la kusimamia shughuli za maafa kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2004; Mwongozo wa Taifa wa Menejimenti ya Maafa wa mwaka 2014; Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Sura ya 242 na Kanuni zake za mwaka 2017.

## 13 SEPTEMBER, 2022

Katika kipindi cha miaka saba ya utekelezaji wa sheria hiyo, kumekuwa na mafanikio mbalimbali katika usimamizi wa maafa nchini kama ifuatavyo:-

(a) Kuanzishwa kwa Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya kufuatilia mwenendo wa majanga na kuratibu dharura nchini;

(b) Kuboresha utabiri wa hali ya hewa kufikia uhakika kwa asilimia 87 ambao umewezesha kuongeza ufanisi katika tahadhari za mapema kwa majanga yanayosababishwa na hali mbaya ya hewa;

(c) Kuanzishwa kwa Baraza la Usimamizi wa Maafa Tanzania na kuratibu kufanyika kwa mikutano ya Baraza hilo;

(d) Kufanya tathmini mbalimbali kuhusu maafa na kulishauri Baraza la Usimamizi wa Maafa Tanzania juu ya hatua za kuchukuliwa;

(e) Kutoa misaada ya kibinadamu kwa waathirika wa maafa na kufanya ufuatiliaji wa ugawaji wa misaada hiyo kwa waathirika;

(f) Kusimamia maghala sita ya kikanda ya kuhifadhi misaada ya kibinadamu ikiwemo kuhakikisha uwepo wa vifaa husika na kutumika kutoa huduma za kibinadamu katika matukio ya maafa;

(g) Kufanyika kwa mikutano ya Jukwaa la Taifa la Usimamizi wa Maafa kwa lengo la kukutanisha wadau mbalimbali kutoka Serikalini na nje ya Serikali ili kujadili namna bora ya kuimarisha usimamizi wa maafa;

(h) Kuanzishwa na kujengewa uwezo kwa Kamati za Usimamizi wa Maafa za ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na Kijiji au Mtaa kupitia mafunzo, mazoezi na kuandaa mipango na mikakati;

(i) Kuelimisha, kuhamasisha na kuwawezesha wadau wa maafa juu ya kuzuia, kujiandaa, kukabili maafa na kurejesha hali baada ya maafa kutokea kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na matumizi ya vyombo vya habari; na

(j) Kuandaa *profile* inayoainisha maeneo yenye uwezekano wa kuathirika na majanga ya mafuriko na ukame.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, kumekuwa na changamoto katika utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa maafa nchini katika hatua za kuzuia, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali. Changamoto hizo zinatokana na hali ya kuongezeka kwa matukio ya majanga na kubadilika kwa

mwenendo wa majanga ya asili kama vile mafuriko, ukame, magonjwa ya mlipuko ya wanadamu ya wanyama, wadudu waharibifu wa mazao na matetemeko ya ardhi na majanga yanayotokana na shughuli za kibinadamu kama vile moto katika majengo na matukio makubwa ya ajali; kuongezeka kwa kiwango cha madhara ya maafa katika maisha, miundombinu, afya, mifumo ya kiuchumi na kijamii na teknolojia nchini; na mabadiliko ya mifumo ya kikanda na kimataifa katika kushughulikia hatari za majanga yanayovuka mipaka na huduma za kibinadamu. Kutokana na hali hii, Serikali inapendekeza itungwe Sheria Mpya ya Usimamizi wa Maafa.

Mheshimiwa Spika, sheria inayopendekezwa kutungwa inalenga kuweka mfumo wa kusimamia maafa kuanzia hatua za kuzuia na kupunguza madhara ya majanga, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali endapo maafa yanatokea kwa kuzingatia sera, sheria na miongozo. Aidha, muswada unajikita katika kuimarisha uwajibikaji wa kila sekta ya jamii pamoja na kuimarisha ushirikiano katika kutekeleza afua za usimamizi wa maafa katika ngazi zote ili kuimarisha ustahimilivu kwa maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, Sheria inayopendekezwa pamoja na mambo mengine itazingatia yafuatayo:-

(a) Kuipa Ofisi ya Waziri Mkuu jukumu la usimamizi wa maafa kupitia Divisheni ya Menejimenti ya Maafa kama ilivyoinishwa katika Hati ya Mgawanyo wa Majukumu ya Mawaziri ya tarehe 24 Januari, 2022. Hatua hii inalenga kuweka mfumo unaoweza Wizara, Taasisi za Serikali na wadau wote muhimu kushiriki katika shughuli za usimamizi wa maafa chini ya uratibu wa moja kwa moja wa Ofisi ya Waziri Mkuu.

(b) Kutenganisha majukumu ya Kamati za Usalama za Mkoa na Wilaya ambazo zinaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa Sura ya 61 ambapo muswada unakusudia kuzitambua kuwa Kamati Elekezi za Mkoa na Wilaya za Usimamizi wa Maafa na yale ya Kamati za Mikoa na Wilaya za Wataalam za Usimamizi wa Maafa zitakazoundwa kwa kuzingatia mapendekezo yaliyopo katika Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya mwaka 2022. Hivyo, muswada unapendekeza kuwa na mgawanyo wa majukumu kwa kuzingatia mfumo wa kiutendaji uliopo.

Mheshimiwa Spika, sheria inayopendekezwa imezingatia uwepo wa makubaliano ya Kikanda na Kimataifa yanayohusiana na shughuli za usimamizi wa maafa ambayo Nchi imeridhia. Makubaliano hayo ni pamoja na Mkakati wa Sendai wa Usimamizi wa Maafa wa mwaka 2015 – 2030 katika ngazi ya Kimataifa; Mpango Kazi wa Usimamizi wa Maafa wa Afrika wa mwaka 2015 – 2030 na Mkakati wa Kujiandaa na Kukabilina na Maafa wa Kikanda na Mfuko

wa Fedha wa mwaka 2016 – 2030 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, wakati wa maandalizi ya muswada huu, Serikali ilipata nafasi ya kufanya tathmini na kupitia tafiti mbalimbali za usimamizi wa maafa hapa nchini pamoja na kupata uzoefu wa nchi nyingine za ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika kama vile Uganda, Botswana, Zambia, Msumbiji, Afrika Kusini na Madagaska. Tathmini iliyofanyika imeonesha kuwa masuala ya usimamizi wa maafa katika nchi hizi yawemekwa chini ya Wizara yenye uwezo wa kuratibu sekta kwa kuwa suala la maafa ni mtambuka.

Aidha, nchi hizo zina mifumo ya utekelezaji inayojumuisha uwepo wa Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi za utendaji kuanzia ngazi ya Taifa hadi Kijiji kutegemea na aina ya muundo wa Serikali katika nchi husika. Kamati hizo zimekuwa zikihusisha ngazi ya Mawaziri, Makatibu Wakuu, wakurugenzi na maafisa waandamizi wa Serikali pamoja na waatalam katika ngazi zote za utendaji. Uzoefu kutoka nchi hizi umesaidia kuboresha mapendekezo ya mfumo wa uratibu na usimamizi wa maafa ulioainishwa katika muswada huu.

Mheshimiwa Spika, muswada ulioandaliwa umezingatia kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2004 ambayo ndiyo mwongozo wa msingi katika shughuli za usimamizi wa maafa hapa nchini. Sera hiyo imezingatia vipengele vyote vya usimamizi wa maafa ambavyo ni kuzuia na kupunguza madhara ya majanga, kujiandaa kukabili na kurejesha hali pindi maafa yanapotokea.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Maafa ambayo imezingatia masuala yaliyoainishwa katika sera kwa kuzingatia mfumo wa utendaji wa Serikali uliopo katika ngazi zote. Mfumo wa kisheria wa usimamizi wa maafa unaopendekezwa unalenga kugatua madaraka ya usimamizi, utunzaji wa rasilimali na kuzingatia mwenendo wa majanga kutokana na taarifa za tahadhari za mapema. Hatua hii itasaidia kuwa na ushiriki wa wadau wote katika hatua zote za usimamizi wa maafa kwa kuongeza uwajibikaji katika ngazi zote nchini. Aidha, mfumo utaimarisha wajibu wa sekta kutambua hatari za maafa katika maeneo yao, kutenga rasilimali za kisekta kabla ya tukio kwa ajili ya kuzuia au kupunguza madhara pamoja na kujiandaa kukabili endapo maafa yatatokea.

Mheshimiwa Spika, sheria inayopendekezwa kutungwa itaimarisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya mwaka 2020 – 2025 ambayo katika Ibara ya 107 inaelekeza Serikali kuhakikisha inasimamia vyombo vinavyoshughulika na usimamizi wa maafa katika kuchukua hatua za kuzuia, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali pindi maafa yanapotokea. Aidha, Serikali inaelekezwa kuchukua hatua za kuimarisha mifumo ya utendaji ya Wizara,

taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa; upatikanaji wa vifaa vya uokozi katika maafa makubwa; kufanya tafiti na kutoa elimu ya kuzuia na kukabiliana na maafa; upatikanaji wa matumizi ya taarifa za tahadhari za mapema; kutekeleza mikakati ya kitaifa, kikanda na kimataifa; na kujenga Kituo cha Kudumu cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa na Mawasiliano ya Dharura katika Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kutungwa na kuanza kutumika kwa Sheria hii kutakuwa na matokeo chanya yafuatayo:-

(a) Kuimarika kwa mfumo wa kitaasisi wa uratibu na usimamizi wa maafa;

(b) Kuongeza ushiriki wa wadau katika shughuli za usimamizi wa maafa, upatikanaji na ufanisi katika matumizi ya rasilimali;

(c) Kupungua kwa madhara yatokanayo na maafa kutokana na kuimarika kwa ushiriki wa sekta na uwajibikaji wa wadau katika shughuli za usimamizi wa maafa;

(d) Kuimarisha uwajibikaji wa kiutendaji wa shughuli za usimamizi wa maafa katika sekta na ngazi zote kutegemea na aina na chanzo cha janga, kiwango cha hatari na ukubwa wa madhara ya maafa;

(e) Kuimarisha uratibu wa ushirikiano kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kuhusu usimamizi wa masuala ya maafa na magonjwa ya mlipuko; na

(f) Kuongeza ufanisi wa mfumo wa tahadhari ya mapema na matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika usimamizi wa maafa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya jumla, naomba sasa kwa rufusa yako, niwasilishe Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa mwaka 2022 ambao umegawayika katika sehemu kuu tano kama ifuatavyo:-

Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi yanayojumuisha jina fupi la sheria, utaratibu wa kuainisha tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria inayopendekezwa kutungwa, mipaka ya matumizi ya sheria inayopendekezwa kutungwa na tafsiri ya baadhi ya maneno na misamiati inayotumika katika sheria inayopendekezwa.

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni tisa na hawa wanatambulishwa maalum kabisa kwasababu ni wageni wa Mheshimiwa Mbunge ambaye ameapishwa leo.

**13 SEPTEMBER, 2022**

Wageni tisa wa Mheshimiwa Tamima Haji Abass ambao ni familia yake kutoka Kaskazini Unguja, Zanzibar wakiongozwa na mume wake Ndugu Shukrani Seif Salum. Karibuni sana wageni wetu. Sasa hapo wengine mkae halafu abaki mume wa Mheshimiwa Mbunge tumuone vizuri. Eee! Mume wa Mheshimiwa Mbunge, haya!. Karibu sana shemeji yetu. *(Makofi)*

Lakini pia wapo wageni wa Wabunge mbalimbali ambao wametembelea siku ya leo Bungeni hapa kwa ajili ya kujifunza mambo mbalimbali. Wageni wa Wabunge wote wasimame kwa pamoja. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao pia wachungaji 67 kutoka Chuo cha *Assemblies of God Central Bible College* kilichopo Jijini Dodoma. Hawa wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wachungaji karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hawa ndiyo wageni tulionao na haya ndiyo matangazo niliyokuwa nayo. Kwa hivyo, tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2002  
(The Disaster Management Bill, 2022)**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijaenda huko nimemuona Mheshimiwa Abdullah Mwinyi amesimama.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ABULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nasimama kwa Kanuni ya 76 kuomba Mwongozo. Hapo mapema baada ya kujibiwa swali langu la msingi niliuliza maswali ya nyongeza mawili. Moja likajibiwa vizuri lakini la pili halikujibiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge amesimama Mheshimiwa Abdullah Mwinyi akiomba Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 76 akieleza kwamba alikuwa ameuliza maswali ya nyongeza mawili na anasema swali la pili

halijajibiwa, limejibiwa swali moja. Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni zetu zinataka maswali yajibiwe kikamilifu.

Kanuni zetu zinataka maswali yajibiwe kikamilifu. Sasa kwa sababu sina hakika sana kama swali lilijibiwa ama halikujibiwa ili nitoe fursa kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kulijibu hilo swali la nyongeza basi nitaenda kutazama Taarifa Rasmi za Bunge maswali yaliyoulizwa na majibu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri ili kama hilo la pili alikuwa amelisahau basi tutampa fursa ya kulijibu wakati mwingine. Kwa hiyo, huo ndio Mwongozo wangu. Ahsante sana.

Sasa Katibu alikuwa ameshasoma jambo ambalo linafuata na ametueleza kwamba kinachofuata hapo ni Muswada wa Sheria. Sasa nitumie fursa hii kumuita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa George Simbachawene Mwatawaguluvala. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:**

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020 naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 1 wa Mwaka 2022, kama ulivyorekebisha kwa mujibu wa jedwali la marekebisha, sasa usomwe Mara ya Pili.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote afya njema na kutuwezesha kuhudhuria kikao cha kwanza cha Mkutano wa Nane wa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa ninamshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukubali itungwe Sheria ya Usimamizi wa Maafa nchini. Aidha, nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yao na maelekezo muhimu ambayo yamekuwa dira wakati wote katika kufanikisha azma ya Serikali ya kuwa na sheria itakayoweka mfumo imara na madhubuti wa usimamizi wa maafa.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya katika kuliongoza Bunge letu. Miongozo yenu imetuwezesha waheshimiwa wabunge kutekeleza majukumu yetu kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, naishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb), na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb), pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi kubwa ya kuchambua na kutoa maoni na mapendekezo yaliyosaidia sana kuboresha



maudhui ya Muswada huu wa Sheria inayopendekezwa kutungwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kumshukuru sana msaidizi wangu Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga (Mb), Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa mchango wake mkubwa katika kufanikisha Muswada huu. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dharti kwa Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama (Mb) na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb), Waziri wa Maliasili na Utalii ambao wote kwa vipindi tofauti walishiriki kikamilifu na kwa weledi mkubwa katika maandalizi ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana viongozi na wataalam wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu wakiongozwa na Dkt. John Jingu, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu na Naibu Katibu Mkuu, Bwana Kaspar Kaspar Mmuya kwa kufanya kazi bila kuchoka wakati wa uandaaji wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa namna ya pekee nitumie fursa hii kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi na timu yake ya wataalam kwa kufanya kazi bila kuchoka wakati wa uandaaji wa Muswada huu. Na kwa namna ya pekee nimshukuru sana Mwandishi Mkuu wa Sheria Ndugu Onorius Njole kwa ushiriki wake wa moja kwa moja katika wakati wote na hata wakati wa Kamati tukiandaa sheria hii mpaka tunafika hatua hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, naomba kuwashukuru sana wadau wote wa usimamizi wa maafa waliopata fursa ya kutoa maoni yao ambayo yalisaidia sana kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Ofisi ya Waziri Mkuu inalo jukumu la kusimamia shughuli za maafa kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya Mwaka 2004, Mwongozo wa Taifa wa Menejimenti ya Maafa wa mwaka 2014, Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Sura ya 242 na Kanuni zake za mwaka 2017.

Katika kipindi cha miaka saba ya utekelezaji wa Sheria hiyo, kumekuwa na mafanikio mbalimbali katika usimamizi wa maafa nchini kama ifuatavyo:-

a) Kuanzishwa kwa Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwaajili ya kufuatilia mwenendo wa majanga na kuratibu dharura nchini,

## 13 SEPTEMBER, 2022

b) Kuboresha utabiri wa hali ya hewa kufikia uhakika kwa asilimia 87 ambao umewezesha kuongeza ufanisi katika tahadhari za mapema kwa majanga yanayosababishwa na hali mbaya ya hewa,

c) Kuanzishwa kwa Baraza la Usimamizi wa Maafa Tanzania na kuratibu kufanyika kwa mikutano ya Baraza hilo,

d) Kufanya tathmini mbalimbali kuhusu maafa na kulishauri Baraza la Usimamizi wa Maafa Tanzania juu ya hatua za kuchukuliwa,

e) Kutoa misaada ya kibinadamu kwa waathirika wa maafa na kufanya ufuatiliaji wa ugawaji wa misaada hiyo kwa waathirika,

f) Kusimamia maghala sita ya kikanda ya kuhifadhi misaada ya kibinadamu ikiwemo kuhakikisha uwepo wa vifaa husika na kutumika kutoa huduma za kibinadamu katika matukio ya maafa,

g) Kufanyika kwa mikutano ya Jukwaa la Taifa la Usimamizi wa Maafa kwa lengo la kukutanisha wadau mbalimbali kutoka serikalini na nje ya Serikali ili kujadili namna bora ya kuimarisha usimamizi wa maafa,

h) Kuanzishwa na kujengewa uwezo kwa Kamati za Usimamizi wa Maafa za ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji au Mitaa kupitia mafunzo, mazoezi na kuandaa mipango na mikakati,

i) Kuelimisha, kuhamasisha na kuwawezesha wadau wa maafa juu ya kuzuia, kujiandaa, kukabili maafa na kurejesha hali baada ya maafa kutokea kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na matumizi ya vyombo vya Habari, na

j) Kuandaa Profile inayoainisha maeneo yenye uwezekano wa kuathirika na majanga ya mafuriko na ukame.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, kumekuwa na changamoto katika utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa maafa nchini katika hatua za kuzuia, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali. Changamoto hizo zinatokana na hali ya kuongezeka kwa matukio ya majanga na kubadilika kwa mwenendo wa majanga ya asili kama vile mafuriko, ukame, magonjwa ya mlipuko ya wanadamu ya wanyama, wadudu waharibifu wa mazao na matetemeko ya ardhi na majanga yanayotokana na shughuli za kibinadamu kama vile moto katika majengo na matukio makubwa ya ajali. Pia kuongezeka kwa kiwango cha madhara ya maafa katika maisha, miundombinu, afya, mifumo ya kiuchumi na kijamii na teknolojia nchini; na mabadiliko ya mifumo ya

## 13 SEPTEMBER, 2022

Kikanda na Kimataifa katika kushughulikia hatari za majanga yanayovuka mipaka na huduma za kibinadamu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii, Serikali inapendekeza itungwe Sheria Mpya ya Usimamizi wa Maafa.

Mheshimiwa Spika, Sheria inayopendekezwa kutungwa inalenga kuweka mfumo wa usimamizi wa maafa kuanzia hatua za kuzuia na kupunguza madhara ya majanga, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali endapo maafa yatatokea kwa kuzingatia sera, sheria na miongozo. Aidha, Muswada unajikita katika kuimarisha uwajibikaji wa kila sekta ya jamii pamoja na kuimarisha ushirikiano katika kutekeleza afua za usimamizi wa maafa katika ngazi zote ili kuimarisha ustahimilivu kwa maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, Sheria inayopendekezwa pamoja na mambo mengine itazingatia yafuatayo:-

(a) Kuipa Ofisi ya Waziri Mkuu jukumu la usimamizi wa maafa kupitia Divisheni ya Menejimenti ya Maafa kama ilivyocainishwa katika Hati ya Mgawanyo wa Majukumu ya Mawaziri ya tarehe 24 Januari, 2022. Hatua hii inalenga kuweka Mfumo unaowezesha wizara, taasisi za Serikali na wadau wote muhimu kushiriki katika shughuli za usimamizi wa maafa chini ya uratibu wa moja kwa moja wa Ofisi ya Waziri Mkuu.

(b) Kutenganisha majukumu ya Kamati za Usalama za Mikoa na Wilaya ambazo zinaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa Sura ya 61; ambapo Muswada unakusudia kuzitambua kuwa Kamati Elekezi za Mikoa na Wilaya za Usimamizi wa Maafa na yale ya Kamati za Mikoa na Wilaya za Wataalam za Usimamizi wa Maafa zitakazoundwa kwa kuzingatia mapendekezo yaliyopo katika Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2022. Hivyo, Muswada unapendekeza kuwa na mgawanyo wa majukumu kwa kuzingatia mfumo wa kiutendaji uliopo.

Mheshimiwa Spika, Sheria inayopendekezwa imezingatia uwepo wa makubaliano ya Kikanda na Kimataifa yanayohusiana na shughuli za usimamizi wa maafa ambayo nchi imeridhia. Makubaliano hayo ni pamoja na Mkakati wa Sendai wa Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2015 – 2030 katika ngazi ya Kimataifa; Mpango Kazi wa Usimamizi wa Maafa wa Afrika wa Mwaka 2015 – 2030 na Mkakati wa Kujiandaa na Kukabilina na Maafa wa Kikanda na Mfuko wa Fedha wa mwaka 2016 – 2030 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, wakati wa maandalizi ya Muswada huu, Serikali ilipata nafasi ya kufanya tathmini na kupitia tafiti mbalimbali za usimamizi wa maafa hapa nchini pamoja na kupata uzoefu wa nchi nyingine za ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika; kama vile Uganda, Botswana, Zambia, Msumbiji, Afrika Kusini na Madagaska. Tathmini iliyofanyika imeonesha kuwa masuala ya usimamizi wa maafa katika nchi hizi yawemekwa chini ya Wizara yenye uwezo wa kuratibu sekta kwa kuwa suala la maafa ni mtambuka. Aidha, nchi hizo zina mifumo ya utekelezaji inayojumuisha uwepo wa Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi za utendaji kuanzia ngazi ya taifa hadi vijiji kutegemea na aina ya muundo wa Serikali katika nchi husika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na waatalam katika ngazi zote za utendaji, uzoefu kutoka nchi hizi umesaidia kuboresha mapendekezo ya mfumo wa uratibu na usimamizi wa maafa ulioainishwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Muswada ulioandaliwa umezingatia kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya Mwaka 2004 ambayo ndio mwongozo wa msingi katika shughuli za usimamizi wa maafa hapa nchini. Sera hiyo imezingatia vipengele vyote vya usimamizi wa maafa ambavyo ni kuzuia na kupunguza madhara ya majanga, kujiandaa kukabili na kurejesha hali pindi maafa yanapotokea.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Maafa ambayo imezingatia masuala yaliyoainishwa katika Sera kwa kuzingatia mfumo wa utendaji wa Serikali uliopo katika ngazi zote. Mfumo wa kisheria wa usimamizi wa maafa unaopendekezwa unalenga kugatua madaraka ya usimamizi, utunzaji wa rasilimali na kuzingatia mwenendo wa majanga kutokana na taarifa za tahadhari za mapema. Hatua hii itasaidia kuwa na ushiriki wa wadau wote katika hatua zote za usimamizi wa maafa kwa kuongeza uwajibikaji katika ngazi zote nchini. Aidha, mfumo utaimarisha wajibu wa sekta kutambua hatari za maafa katika maeneo yao, kutenga rasilimali za kisekta kabla ya tukio kwa ajili ya kuzuia au kupunguza madhara pamoja na kujiandaa kukabili endapo maafa yatatokea.

Mheshimiwa Spika, Sheria inayopendekezwa kutungwa itaimarisha utekelezaji wa Iiani ya uchaguzi ya chama tawala ya Mwaka 2020 – 2025 ambayo katika Ibara ya 107 inaelekeza Serikali kuhakikisha inasimamia vyombo vinavyoshughulika na usimamizi wa maafa katika kuchukua hatua za kuzuia, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali pindi maafa yanapotokea. Aidha, Serikali inaelekezwa kuchukua hatua za kuimarisha mifumo ya utendaji ya Wizara, taasisi na mamlaka za serikali za mitaa katika upatikanaji wa vifaa vya uokozi katika maafa makubwa. Kufanya tafiti na kutoa elimu ya kuzuia na kukabiliana na maafa; upatikanaji wa matumizi ya taarifa za tahadhari za mapema; kutekeleza mikakati ya kitaifa, kikanda na kimataifa; na kujenga kituo cha

## 13 SEPTEMBER, 2022

kudumu cha Taifa cha usimamizi wa maafa na mawasiliano ya dharura katika Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kutungwa na kuanza kutumika kwa Sheria hii kutakuwa na matokeo chanya yafuatayo:-

(a) Kuimarika kwa mfumo wa kitaasisi wa uratibu na usimamizi wa maafa;

(b) Kuongeza ushiriki wa wadau katika shughuli za usimamizi wa maafa, upatikanaji na ufanisi katika matumizi ya rasilimali;

(c) Kupungua kwa madhara yatokanayo na maafa kutokana na kuimarika kwa ushiriki wa sekta na uwajibikaji wa wadau katika shughuli za usimamizi wa maafa;

(d) Kuimarisha uwajibikaji wa kiutendaji wa shughuli za usimamizi wa maafa katika sekta na ngazi zote kutegemea na aina na chanzo cha janga, kiwango cha hatari na ukubwa wa madhara ya maafa;

(e) Kuimarisha uratibu wa ushirikiano kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kuhusu usimamizi wa masuala ya maafa na magonjwa ya mlipuko; na

(f) Kuongeza ufanisi wa mfumo wa tahadhari ya mapema na matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika usimamizi wa maafa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya jumla, naomba sasa kwa ruhusa yako, niwasilishe Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022 ambao umegawayika katika sehemu kuu tano kama ifuatavyo:-

Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi, yanayojumuisha jina fupi la Sheria, utaratibu wa kuainisha tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria inayopendekezwa kutungwa, mipaka ya matumizi ya Sheria inayopendekezwa kutungwa na tafsiri ya baadhi ya maneno na misamiati inayotumika katika Sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili inahusu mfumo wa usimamizi na uratibu wa maafa nchini. Sehemu hii inaweka mfumo wa kitaasisi wa usimamizi na uratibu wa maafa kwa kuanzisha Kamati Elekezi ya Usimamizi wa Maafa katika ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya na Kamati ya Wataalam na Usimamizi wa Maafa katika ngazi ya Taifa hadi kijiji au mtaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati zinazopekezwa kuanzishwa zitakuwa na jukumu la udhibiti wa usimamizi wa shughuli za maafa katika maeneo yao.

Sehemu hii pia inaanza jukwaa la Taifa la wadau wa usimamizi wa maafa litakalokutanisha wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya Serikali ili kujadili namna bora ya kuimarisha usimamizi wa maafa kwa ushiriki wa pamoja.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu inaweka masharti kuhusu mkakati wa Taifa wa usimamizi wa maafa na wajibu wa mtu na taasisi wakati wa shughuli za usimamizi wa maafa. Vilevile sehemu hii inaweka utaratibu wa kutangaza eneo la maafa na hatua zinazopaswa kuchukuliwa katika eneo lililotangazwa. Aidha, sehemu hii pia inaweka utaratibu utakaozingatiwa na Waziri katika kumtaarifu Rais matukio yanayolazimu kutangazwa kuwa hali ya hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne inapendekeza kuanzishwa Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za kuzuia na kupunguza madhara ya majanga, kujiandaa kukabiliana na maafa kabla hayajatokea na kurejesha hali baada ya maafa kutokea.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii inaainisha vyanzo vya fedha za mfuko unaopendekezwa kuanzishwa na kuweka utaratibu wa matumizi ya fedha za mfuko. Aidha, sehemu hii inaweka masharti ya utaratibu wa pamoja wa ukusanyaji wa misaada wakati wa maafa na ufikishwaji wa misaada hiyo kwa jamii iliyoathirika na maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano inabainisha masharti ya jumla yanayojumuisha makosa yanayohusiana na usimamizi wa masuala ya maafa na adhabu zake, kinga dhidi ya mashtaka kwa waajiriwa wa Wizara wakati wa kutekeleza shughuli za usimamizi wa maafa na mamlaka ya Waziri ya kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekezwa kufutwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Sura ya 242 na kupendekeza itungwe sheria mpya ambayo itaimarisha mfumo wa usimamizi wa maafa nchini kwa kuondoa changamoto za sheria iliyopo sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii tena kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu. Naishukuru tena Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa mchango wao mkubwa sana katika Muswada huu ambao kwa kweli ulitusumbua lakini hata hivyo kutokana na umakini wa Kamati hii tuliweza kukubaliana katika maeneo takribani yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako Tukufu kuujadili na kuupitisha Muswada huu wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022 kuwa Sheria ya Tanzania.

**13 SEPTEMBER, 2022**

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. Tunaendelea na utaratibu wetu.

Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama aje awasilishe maoni ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge.

**MHE. DKT. JOSEPH K. MHAGAMA (MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, naomba taarifa hii yote iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Muswada wa Sheria ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1)(b) cha nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kutekeleza jukumu hilo, kama ilivyo desturi, Kamati ilianza uchambuzi wake kwa kupokea na kujadili maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada ambayo yaliwasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa Boniface George Simbachawene, Mbunge, tarehe 30 Agosti, 2022.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau walioalikwa katika Mkutano wa Kupokea Maoni ya Wadau kwa maana ya *Public Hearing*, uliofanyika tarehe 31 Juni, 2022 na tarehe 01 Septemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau yaliyowasilishwa kwa njia ya mtandao. Kwa kumbukumbu za Bunge lako Tukufu, naomba niwatambue wadau waliowasilisha maoni hayo mbele ya Kamati na kwa njia ya mtandao kama ifuatavyo:-

- (1) Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania;
- (2) Benki ya Dunia;
- (3) Chama cha Wanasheria Tanganyika;
- (4) Dar es Salaam *Multi-Agency Emergency Response Team*; na

(5) Watu binafsi kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa dhati kabisa wadau wote waliowasilisha maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa yameongeza mawanda ya uchambuzi wa Kamati kuhusu maudhui ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022 ulifanyiwa uchambuzi na Kamati kwa kuhakiki na kufanya upembuzi wa maudhui, masharti, mpangilio na dhamira kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi huo, Kamati ilijielekeza katika mambo muhimu ya jumla pamoja na masharti mahsusi yaliyopatikana katika ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilifanya rejea katika nyaraka mbalimbali pamoja na uzoefu katika nchi nyingine katika suala la usimamizi wa maafa ili kufanya uchambuzi linganifu kwa maana ya *comparative analysis* kwa lengo la kuboresha masharti yaliyopendekezwa na Muswada.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya Mwaka 2004 imekuwa ndiyo nyenzo kuu ya kimkakati katika suala la usimamizi wa maafa kwa kuwa inaweka mkazo wa umuhimu wa usalama wa maisha ya watu na mali zao.

Mheshimiwa Spika, sera hiyo imebainisha mambo muhimu mbalimbali katika mkakati wa kusimamia maafa ambayo kwa ujumla wake yamejikita katika vipengele vikuu vinne vya usimamizi, menejimenti ya maafa ambavyo ni:-

1. Kuzuia;
2. Kujiandaa;
3. Kukabili; na
4. Kurejesha hali.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa mwaka 2022 unakusudia kuanzisha mfumo wa usimamizi na uratibu wa maafa kwa lengo la kujiandaa, kukabili majanga, kuchukua hatua za kupunguza madhara ya majanga pamoja na kurejesha jamii katika hali ya awali au bora baada ya maafa.

Mheshimiwa Spika, Muswada pia unakusudia kuifuta Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Sura ya 242 iliyokuwa inatumika tangu mwaka 2015. Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kwamba sheria iliyofutwa ina upungufu unaosababisha utekelezaji wake kuwa na changamoto mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-



(a) Sheria inayofutwa kukinzana na Sheria ya Baraza la Usalama wa Taifa, Sura ya 61 kwa sababu sheria zote mbili kwa pamoja kuwa na masharti ambayo yanaweka jukumu la usimamizi wa maafa kwa kamati mbili tofauti bila kuainisha mipaka ya majukumu. Kamati hizo ni Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na Wilaya kwa mujibu wa Sura ya 61 kwa upande mmoja na Kamati ya Usimamizi wa Maafa ya Mkoa na Wilaya kwa mujibu wa Sura ya 242 ambayo inafutwa na Muswada huu.

(b) Sheria inayofutwa ilianzisha Wakala wa Usimamizi wa Maafa ambayo ulipewa mamlaka ya kuwa chombo kikuu cha usimamizi na uratibu wa maafa. Hata hivyo, tangu kutungwa kwa sheria hiyo Wakala hakuwahi kuundwa. Aidha, Kamati imebaini kwamba pamoja na Wakala huo kuwepo kisheria, muundo wa sasa umeweka usimamizi wa maafa katika Idara ya Menejimenti ya Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine sheria iliyopendekezwa inaakisi Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ambayo pamoja na mambo mengine, iliweka ahadi kwamba itahakikisha Serikali inasimamia vyombo vinavyoshughulika na maafa kuwa na mpango wa utayari wa kuzuia, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali haraka pindi maafa yanapojitokeza kwa kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

(a) Kujenga na kuimarisha uwezo wa Kitaifa wa uokozi katika maafa makubwa;

(b) Kuzijengea uwezo Wizara, taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(c) Kuweka mikakati ya kushirikiana na sekta nyingine katika kuzuia na kukabiliana na maafa katika ngazi zote hususani ngazi za chini; na

(d) Kuyaainisha maeneo hatarishi na kuweka mfumo wa tahadhari ya mapema.

Mheshimiwa Spika, sheria inayopendekezwa pia inalenga kuendana na mabadiliko ya mifumo ya kikanda na Kimataifa katika kushughulikia hatari za majanga yanayovuka mipaka ya nchi ikiwemo mkakati wa Sendai wa malengo ya kupunguza athari za maafa 2015 – 2030 ulioandaliwa na Umoja wa Mataifa kwa kushirikiana na Nchi Wanachama na kuridhiwa tarehe 18 Machi, 2015 nchini Japani.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, sheria inayopendekezwa sasa inaanzisha mfumo wa kitaasisi wa usimamizi wa maafa katika sekta mtambuka na ngazi mbalimbali za uongozi wa nchi. Mfumo unaopendekezwa umezingatia muundo

## 13 SEPTEMBER, 2022

wa kitaasisi uliopo katika Serikali katika usimamizi wa maafa na hivyo basi, mfumo huo utajumuisha mambo muhimu yafuatayo:-

(a) Kuanzisha Kamati Elekezi ya Kitaifa ya Usimamizi wa Maafa inayoundwa na Mawaziri wenye dhamana na sekta mbalimbali itakayoongozwa na Waziri Mkuu;

(b) Kuzitambua Kamati za Ulinzi na Usalama za Mkoa na Wilaya kuwa Kamati Elekezi za Usimamizi wa Maafa katika ngazi hizo pamoja na Wabunge wengine ambao wameainishwa katika Muswada;

(c) Kuanzisha Kamati za Wataalam za Usimamizi wa Maafa katika ngazi mbalimbali za uongozi wa nchi kuanzia ngazi ya Taifa hadi ngazi ya vijiji na mitaa;

(d) Kuanzisha Jukwaa la Taifa la Wadau wa Usimamizi wa Maafa; na

(e) Kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi kuhusu ibara za Muswada; sehemu ya kwanza ya Muswada inaweka masharti ya utangulizi na inajumuisha jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika, mipaka ya matumizi pamoja na kutoa tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada huo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya Muswada inahusu uanzishwaji wa mfumo wa usimamizi na uratibu wa maafa nchini ambapo pamoja na mambo mengine, inaanzisha Kamati Elekezi ya Kitaifa ya Usimamizi wa Maafa inayoongozwa na Waziri Mkuu pamoja na kamati nyingine mbalimbali na kuainisha muundo wa majukumu ya kamati hizo.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika sehemu hii, Muswada unaanzisha kituo cha operesheni na mawasiliano ya dharura ambacho kitakuwa na jukumu la kufuatilia mwenendo wa majanga pamoja na kupokea na kuchambua taarifa za tahadhari kwa ajili ya usimamizi wa maafa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Sita inazungumzia mamlaka ya Waziri. Ibara ndogo ya 6(c) inaweka masharti kwamba Waziri atakuwa na mamlaka ya kuamuru matumizi ya rasilimali za mtu yeyote, idara au taasisi wakati wa usimamizi wa maafa kwa tathmini ya kamati na kwa kuzingatia ulinzi wa haki za msingi za raia kumiliki na kuhifadhi mali kwa mujibu wa Ibara ya 24(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Mamlaka hii inaweza kuleta changamoto katika utekelezaji wake. *(Makofi)*

## 13 SEPTEMBER, 2022

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano kuhusu ibara hiyo ya Muswada, Serikali imeboresha masharti hayo kwa kuondoa sharti la Waziri kuamuru kutumia mali za watu na taasisi binafsi katika kukabiliana na maafa na badala yake Waziri atakuwa na mamlaka ya kuamuru matumizi ya mali za taasisi za Umma pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kulitaarifu Bunge lako kwamba tathmini na uchambuzi wa Kamati uliofanywa katika Ibara ya 6 pia umefanyika katika Ibara ya 21 ya Muswada ambayo nayo inaweka masharti yanayoshabihiana kwa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya mtawalia kutumia rasilimali za mtu yeyote, idara au taasisi wakati wa usimamizi wa maafa. Serikali imeboresha masharti hayo pia kwa kuondoa sharti la Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kuamuru kutumia mali za watu na taasisi binafsi katika kukabiliana na maafa na badala yake watakuwa na mamlaka ya kuamuru matumizi ya mali za taasisi za Umma pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 7 ya Muswada inaanzisha Kamati Elekezi ya Kitaifa ya Usimamizi wa Maafa. Moja kati ya hoja kubwa zilizoibuliwa wakati wa uchambuzi ni idadi kubwa ya Wajumbe wa Kamati hiyo ambayo ilikuwa inajumuisha Mawaziri wenye dhamana katika sekta karibu zote.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuzingatia kwamba suala la usimamizi wa maafa ni jambo ambalo linapaswa kufanyika kwa haraka, uchache au wingi wa Wajumbe una uhusiano wa moja kwa moja na ufanisi wa kufanya maamuzi ya haraka. Kamati pia ilizingatia uzoefu unaopatikana katika nchi nyingine ikiwemo India ambako kamati inayofanana na hii ina Wajumbe wasiozidi tisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano ya kina na Kamati, Serikali iliboresha ibara hiyo kwa kupunguza idadi ya Wajumbe wanaounda Kamati Elekezi ya Kitaifa ya Usimamizi wa Maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tathmini ya idadi ya Wajumbe iliyofanywa na Kamati ya Katiba katika Ibara ya 7, pia imefanyika katika Ibara ya 9 inayoanzisha Kamati ya Wataalam wa Kitaifa, Ibara ya 15 inayoanzisha Kamati ya Wataalam ya Mkoa ya Usimamizi wa Maafa pamoja na Ibara ya 19 inayoanzisha Kamati ya Wataalam wa Jiji, Manispaa, Mji na Wilaya ya Usimamizi wa Maafa kwa muktadha wa kupunguza idadi ya Wajumbe wa Kamati hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imefanya maboresho katika ibara hizo kwa kuondoa wawakilishi na kutambua Wajumbe kutokana na nafasi zao. Aidha, maboresho yamefanyika kwa kupunguza idadi ya Wajumbe wa Kamati za Wataalam katika ngazi husika. *(Makofi)*

## 13 SEPTEMBER, 2022

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya Muswada inahusu mkakati wa Taifa wa usimamizi wa maafa na operesheni wakati wa maafa. Kimsingi sehemu hii inaainisha wajibu wa Serikali kuandaa mipango, bajeti na mikakati inayolenga kuainisha hatari za majanga yanayoweza kutokea na hatimaye kuzuia na kupunguza madhara ya majanga, kujiandaa na kukabiliana na maafa.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 31 ambayo imebainisha wajibu wa jumla, Kamati ilifanya tathimini na kubaini kwamba kuna ombwe la kukosekana masharti ya uwajibikaji kwa sheria inayopendekezwa kutoweka adhabu. Pamoja na kwamba sehemu ya tano ya Muswada inaweka masharti ya jumla ya kuweka makosa ya adhabu, bado kuna umuhimu wa Serikali kwa sehemu hii inayobainisha wajibu pia kuwa na masharti ya adhabu.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano ya kina, Serikali imezingatia maoni ya Kamati kwamba itaongeza ibara mpya itakayoweka masharti ya adhabu za jumla kwa makosa yote yanayohusiana na ukiukwaji wa masharti ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ya Muswada inaanzisha Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa, kuainisha vyanzo vya fedha vya mfuko huo na kuweka masharti yanayohusu matumizi ya fedha za mfuko ikiwemo kumtambua Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana na maafa kuwa Afisa Masuuli.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya mambo ya msingi ambayo kwa uchambuzi wa Kamati yanapaswa kuwekewa utaratibu mzuri wa kisheria ni namna bora ambavyo mfuko huu utatumika ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba fedha za mfuko zinalindwa ili zitumike kwa matumizi ya kuzuia majanga na kukabiliana na maafa tu na siyo kwa matumizi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano ya Muswada inahusu masharti ya jumla ikiwemo makosa na adhabu ambayo yanatokana na utekelezaji wa usimamizi wa maafa. Aidha, katika sehemu hii ya Muswada, Waziri mwenye dhamana na maafa amepewa mamlaka ya kutengeneza kanuni kuhusu suala lolote ambalo ni la lazima kwa madhumuni ya utekelezaji wa sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 36 inabainisha makosa na adhabu. Makosa yanayoainishwa ni pamoja na mtu kukataa kutoa ushirikiano kwa Afisa anayetekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria hii au kwa makusudi kutoa taarifa za uongo au za kupotosha wakati wa kujibu maswali yanayoulizwa na Afisa kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yake chini ya sheria hii.

**13 SEPTEMBER, 2022**

Mheshimiwa Spika, moja ya adhabu inayopendekezwa ni faini isiyopungua Shilingi milioni moja au kifungo kisichozidi mwaka mmoja au vyote. Kwa tathmini ya Kamati, adhabu ya faini isiyopungua Shilingi milioni moja haina ukomo na inaweza kutumika vibaya. Baada ya majadiliano ya kina, Serikali imezingatia tathmini ya Kamati hiyo, kupunguza adhabu hiyo na pia kuweka ukomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni na mapendekezo ya Kamati; Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa mwaka 2022 kwa lugha ya Kiswahili. Pamoja na kwamba nia ya Bunge inabaki kuona sheria zetu zinatungwa katika lugha inayoeleweka, hatuwezi kukwepa ukweli kwamba matumizi ya lugha ya Kiswahili pekee katika uandishi wa sheria unaleta changamoto hasa katika matumizi ya maneno na tafsiri. Changamoto kama hizi zinapaswa kuwa kichocheo chenye lengo la kuongeza ufanisi wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika uandishi wa sheria mbalimbali nchini ili lugha yetu iendelee kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo mahususi kuhusu elimu kwa Umma. Kamati inashauri Serikali kutoa elimu ya mara kwa mara kwa Umma kuhusu hatua za kuchukua panapotokea majanga ili kupunguza athari za maafa. Elimu hii itolewe katika Shule za Msingi na awali, maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu na yenye shughuli nyingi pamoja na kwenye vyombo mbalimbali vya habari.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maboresho ya sera. Kwa kuzingatia kwamba Sera ya Menejimenti ya Maafa ya Mwaka 2004 imekuwa ndiyo nyenzo kuu inayoweka dira ya suala zima la usimamizi wa maafa, ni vyema sera hiyo ikahuishwa ili iendane na wakati. Aidha, sera hiyo iweke mkazo kuhusu suala la ushirikishwaji na ushiriki wa sekta zote katika kukabiliana na maafa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa, Kamati inaishauri Serikali kuandaa haraka Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa, katika maandalizi ya mkakati huo kwa kadri itakavyowezekana Serikali ishirikishe makundi na wadau wote muhimu ili kuboresha mawanda ya utekelezaji wa mkakati huo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ambao katika kutekeleza majumu yao ya kikatiba walichambua kujadili na kutoa na maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mchango wao naomba majina yao yaingie katika taarifa rasmi za Bunge kama yalivyoorodheshwa.

## 13 SEPTEMBER, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba baadhi ya Wabunge ambao walikuwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria wakati wa uchambuzi wa Muswada huu, sasa ni Wajumbe wa Kamati nyingine, sina budi kuwashukuru sana kwa mchango wao ambao ni sehemu ya taarifa hii. Wajumbe hao ni Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani na Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nichukue fursa hii kuwakaribisha Wabunge walioteuliwa hivi karibuni kuwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria ambao ni Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid, Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo na Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Mheshimiwa George Boniface Simbachawene akisaidiwa na Naibu Waziri katika ofisi hiyo Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga kwa ushirikiano ambao ameupatia Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada. Aidha, nawashukuru watendaji wote chini ya ofisi hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. John Anton Jingu; Naibu Katibu Mkuu, ndugu Kaspar Kaspar Mmuya kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee niwashukuru watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge ndugu Nanelwa Mwhambi kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. Namshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, ndugu Athumani Hussein, akisaidiwa na Mkurugenzi Msaidizi, ndugu Gerald Magili kwa kusimamia utendaji wa Kamati mbalimbali za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru watumishi wa Bunge ambao wanaunda Sekretarieti ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria iliyohusika na uratibu wa vikao vya Kamati na kutoa ushauri wa kitalaam wakati wa uchambuzi wa Muswada hadi kukamilika kwa taarifa hii. Watumishi hao ni ndugu Elihaika Mtui, ndugu Yona Kirumbi, ndugu Eveline Shibandiko, ndugu Rebeca Balisidya na ndugu Daniel Zephania wakisaidiwa na ndugu Teresia Jacob. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria inalishauri Bunge, kujadili, kukubali na kupitisha Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022, pamoja na marekebisho yake kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**13 SEPTEMBER, 2022**

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.  
(Makofi)

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU  
MUSWADA WA SHERIA YA USIMAMIZI WA MAAFA NA.1 WA MWAKA 2022 - KAMA  
YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 99 (5)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria Kuhusu Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Na. 1 wa Mwaka 2022.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza katika **Kikao cha Kumi na Tatu** katika **Mkutano wa Sita** wa Bunge, siku ya Alhamis tarehe **17 Februari, 2022** kwa mujibu wa masharti ya **Kanuni ya 93 (2)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Baada ya hatua hiyo, na kwa kuzingatia masharti ya **Kanuni ya 97 (1)** ikisomwa pamoja na **Kanuni 136 (14)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ulitumia mamlaka yako kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, ili Kamati iujadili na kuufanyia uchambuzi.

**1.2 Namna Kamati ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi wa Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Miswada ya Sheria ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa **Kifungu cha 7(1) (b)** cha **Nyongeza ya Nane** ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kutekeleza jukumu hilo, kama ilivyo desturi, Kamati ilianza uchambuzi wake kwa kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada, ambayo yaliwasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Mhe. Boniface George Simbachawene (Mb) siku ya Jumanne tarehe 30 Agosti, 2022.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, kwa mujibu wa **Kanuni ya 97 (2)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau walioalikwa katika Mkutano wa Kupokea Maoni ya Wadau (*Public Hearing*) uliofanyika tarehe 31 Agosti, 2022 na tarehe 1 Septemba, 2022. Aidha, Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau yaliyowasilishwa kwa njia ya mtandao. Kwa kumbukumbu za Bunge lako tukufu, naomba niwatambue wadau waliowasilisha maoni yao mbele ya Kamati na kwa njia ya mtandao kama ifuatavyo:-

- 1) Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania (*Tanzania Red Cross Society*)
- 2) Benki ya Dunia (*The World Bank*)
- 3) Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS)
- 4) *Dar es Salaam Multiagency Emergency Response Team (DarMAERT)*
- 5) Watu binafsi kutoka maeneo mbalimbali nchini

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru kwa dhati kabisa, wadau wote waliowasilisha maoni yao, ambayo kwa kiasi kikubwa yameongeza mawanda ya Uchambuzi wa Kamati kuhusu maudhui ya Muswada huu.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

#### 2.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022 ulifanyiwa uchambuzi na Kamati kwa kuhakiki na kufanya upembuzi wa maudhui, masharti, mpangilio, na dhamira kwa ujumla. Katika uchambuzi huo, Kamati ilijielelekeza katika mambo muhimu ya jumla pamoja na masharti mahsusi yanayopatikana katika Ibara mbalimbali za Muswada. Aidha, Kamati ilifanya rejea katika nyaraka mbalimbali pamoja na uzoefu katika nchi nyingine katika suala la usimamizi wa maafa ili kufanya uchanganuzi linganifu (*comparative analysis*) kwa lengo la kuboresha masharti yanayopendekezwa na Muswada

#### 2.2 Upembuzi wa Maudhui

**Mheshimiwa Spika**, Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya Mwaka 2004, imekuwa ndio nyenzo kuu ya kimkakati katika suala la usimamizi wa maafa kwa kuwa inaweka mkazo wa umuhimu wa usalama wa maisha ya watu na mali zao. Sera hiyo imebainisha mambo muhimu mbalimbali katika mkakati wa kusimamia maafa ambayo kwa ujumla wake yamejikita katika vipengele vikuu vinne (4) vya usimamizi/menejimenti ya maafa ambavyo ni: -

- a) Kuzuia
- b) Kujiandaa



- c) Kukabili
- d) Kurejesha hali

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo, Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka, 2022 unakusudia kuanzisha **Mfumo wa Usimamizi na Uratibu wa Maafa** kwa lengo la kujiandaa kukabili majanga, kuchukua hatua za kupunguza madhara ya majanga, pamoja na kurejesha jamii katika hali ya awali au bora zaidi baada ya maafa.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada pia unakusudia kuifuta **Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Sura ya 242** iliyokuwa inatumika tangu Mwaka 2015. Katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kwamba Sheria inayofutwa ina mapungufu yanayosababisha utekelezaji wake kuwa na changamoto mbalimbali zikiwemo zifuatazo: -

a) Sheria inayofutwa kukinzana na **Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa, Sura ya 61** kwa sababu sheria zote mbili kwa pamoja kuwa na masharti ambayo yanaweka jukumu la usimamizi wa maafa kwa Kamati mbili tofauti bila kuainisha mipaka ya majukumu. Kamati hizo ni **Kamati ya Ulinzi na Usalama (KUU)** ya Mkoa na Wilaya kwa mujibu wa **Sura ya 61** kwa upande mmoja, na **Kamati ya Usimamizi wa Maafa** ya Mkoa na Wilaya kwa mujibu wa **Sura ya 242** ambayo inafutwa na Muswada huu.

b) Sheria inayofutwa ilianzisha **Wakala wa Usimamizi wa Maafa** ambao ulipewa mamlaka ya kuwa chombo kikuu cha usimamizi na uratibu wa maafa. Hata hivyo, tangu kutungwa kwa sheria hiyo, Wakala haukuwahi kuundwa. Aidha, Kamati imebaini kwamba, pamoja na Wakala huo kuwepo Kisheria, muundo wa sasa umeweka usimamizi wa maafa katika Idara ya Menejimenti ya Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, Sheria inayopendekezwa inaakisi **Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020** ambayo, pamoja na mambo mengine, iliweka ahadi kwamba itahakikisha Serikali inasimamia vyombo vinavyoshughulika na maafa kuwa na mpango wa utayari wa kuzuia, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali haraka pindi maafa yanapotokea kwa kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo zifuatazo: -

- a) Kujenga na kuimarisha uwezo wa kitaifa wa uokozi katika maafa makubwa
- b) Kuzijengea uwezo wizara, taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa

- c) Kuweka mikakati ya kushirikiana na sekta nyingine katika kuzuia na kukabiliana na maafa katika ngazi zote hususan ngazi za chini
- d) Kuainisha maeneo hatarishi na kuweka mfumo wa tahadhari ya mapema

**Mheshimiwa Spika**, Sheria inayopendekezwa pia ina lengo la kuendana na mabadiliko ya mfumo ya kikanda na kimataifa katika kushugulikia hatari za majanga yanayovuka mipaka ya nchi, ikiwemo **Mkakati wa Sendai wa Malengo ya Kupunguza Athari za Maafa 2015 – 2030** ulioandaliwa na Umoja wa Mataifa kwa kushirikiana na nchi wanachama, na kuridhiwa tarehe 18 machi, 2015 nchini Japan.

**Mheshimiwa Spika**, hivyo basi, Sheria inayopendekezwa, sasa inaanzisha **Mfumo wa Kitaasisi wa Usimamizi wa Maafa** katika sekta mtambuka na ngazi mbalimbali za Uongozi wa Nchi. Mfumo unaopendekezwa umezingatia muundo wa kitaasisi uliopo katika Serikali katika usimamizi wa maafa, na hivyo basi, mfumo huo utajumuisha mambo muhimu yafuatayo: -

- a) kuanzisha Kamati Elekezi ya Kitaifa ya Usimamizi wa Maafa, inayoundwa na Mawaziri wenye dhamana na sekta mbalimbali itakayoongozwa na Waziri Mkuu;
- b) kuzitambua Kamati za Ulinzi na Usalama za Mkoa na Wilaya kuwa Kamati Elekezi za Usimamizi wa Maafa katika ngazi hizo pamoja na Wabunge wengine ambao wameinishwa katika Muswada;
- c) kuanzisha Kamati za Wataalam za Usimamizi wa Maafa katika ngazi mbalimbali za uongozi wa nchi kuanzia ngazi ya Taifa hadi ngazi ya Kijiji au Mtaa;
- d) kuanzisha Jukwaa la Taifa la Wadau wa Usimamizi wa Maafa; na
- e) kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa

## 2.3 Uchambuzi Kuhusu Ibara za Muswada

### 2.3.1 Sehemu ya Kwanza ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, **Sehemu ya Kwanza** ya Muswada inaweka Masharti ya Utangulizi na inajumuisha Jina la Sheria, Tarehe ya Kuanza Kutumika, Mipaka ya Matumizi, pamoja na kutoa Tafsiri ya Maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 1** ya Muswada inalitaja jina la Sheria inayopendekezwa kuwa ni **Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2022**. Jina hili fupi la Muswada linatolewa ufafanuzi wa ziada na Jina Refu kwamba Sheria inayopendekezwa ni '*...Sheria ya kuweka mfumo wa **usimamizi** na uratibu (chombo au mamlaka) wa maafa kwa ajili (malengo ya hicho chombo) ya **hatua za kuzuia** na kupunguza madhara ya majanga, **kujiandaa kukabili** na kurejesha hali pindi maafa yanapotokea pamoja na kuanzisha na kusimamia Mfuko wa Usimamizi wa Maafa na mambo yanayohusiana nayo.*'<sup>1</sup> Msisitizo ni wetu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia maelezo yanayopatikana katika Jina Refu, Kamati ilifanya tathmini ili kuona uwezekano wa Jina Fupi la Muswada kuakisi na kujumuisha maudhui muhimu na mahsusi yanayopatikana katika Jina Refu la Muswada ambayo ni suala la kuzuia majanga, na hatua za kukabili maafa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilidadisi na kulinganisha tafsiri za Usimamizi wa Maafa kwa kutumia kamusi na kubaini kwamba, kwa lugha ya Kiingereza maneno hayo yanatafsirika kama '*Disaster Management*' ambayo pia imetumika katika Sheria za nchi nyingine kadhaa zenye sheria zinazofanana na ya kwetu. Hata hivyo, kwa mujibu wa **Kamusi ya Kiingereza – Kiswahili**, Toleo la Tatu, neno '*management*' kwa Kiswahili ni '*menejimenti*'. Aidha, Sera ya Maafa ya 2004, inatumia neno '*menejimenti*' badala ya neno '*usimamizi*'. Hii ni kwa sababu, neno '*usimamizi*' kwa mujibu wa Kamusi Kuu ya Kiswahili, Toleo la 2 ni '*tendo la kusimamia au kuongoza watu ili watimize wajibu fulani kwa namna inavyotakiwa*'.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba, tafsiri za kisheria zinatolewa na Sheria, na kwa muktadha huo, **Ibara ya 3** inatoa tafsiri ya maneno "Usimamizi wa Maafa" kuwa ni '*...utekelezaji wa sera na mikakati ya kupunguza hatari za maafa ili kuzuia hatari mpya, kupunguza hatari zilizopo na kudhibiti hatari zilizobaki kwa lengo la kuimarisha ustahimilivu na kupunguza hasara za maafa.*'

Kwa kuzingatia uchambuzi huo, Kamati ilishauri Serikali kwamba, Jina Fupi la Sheria inayopendekezwa kuwa **Sheria ya Kuzuia Majanga na Kukabiliana na Maafa, 2022**. Baada ya majadiliano ya kina, Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali kwamba Jina Fupi la Sheria hii libaki kama Muswada unavyopendekeza.

### 2.3.2 Sehemu ya Pili ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inahusu Uanzishwaji wa Mfumo wa Usimamizi na Uratibu wa Maafa Nchini, ambapo pamoja na mambo mengine inaanzisha

---

<sup>1</sup> Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa, 2022 UK. 4

Kamati Elekezi ya Kitaifa ya Usimamizi wa Maafa inayoongozwa na Waziri Mkuu, pamoja na Kamati nyingine mbalimbali na kuainisha Muundo na Majukumu ya kamati hizo. Aidha, katika Sehemu hii, Muswada unaanzisha Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura ambacho kitakuwa na jukumu la kufuatilia mwenendo wa majanga, pamoja na kupokea na kuchambua taarifa za tahadhari kwa ajili ya usimamizi wa Maafa.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6** inazungumzia Mamlaka ya Waziri; Ibara Ndogo ya 6 (c) inaweka masharti kwamba Waziri atakuwa na mamlaka ya kuamuru matumizi ya rasilimali za mtu yeyote, idara au taasisi, wakati wa usimamizi wa maafa. Kwa tathmini ya Kamati, na kwa kuzingatia ulinzi wa haki za msingi za raia kumiliki na kuhifadhi mali kwa mujibu wa Ibara ya 24 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, mamlaka hii inaweza ikaleta changamoto katika utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya majadiliano kuhusu Ibara hiyo ya Muswada, Serikali imeboresha masharti hayo kwa kuondoa sharti la Waziri kuamuru kutumia mali za watu na taasisi binafsi katika kukabiliana na maafa na badala yake Waziri atakuwa na mamlaka ya kuamuru matumizi ya mali za taasisi za umma pekee.

**Mheshimiwa Spika**, aidha napenda kulitaarifu Bunge lako kwamba, tathmini na uchambuzi wa Kamati uliofanywa katika Ibara ya 6, pia umefanywa katika Ibara ya 21 ya Muswada ambayo nayo inaweka masharti yanayoshabihiana kwa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya mtawalia, kutumia rasilimali za mtu yeyote, idara au taasisi, wakati wa usimamizi wa maafa. Serikali imeboresha masharti hayo pia kwa kuondoa sharti la Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kuamuru kutumia mali za watu na taasisi binafsi katika kukabiliana na maafa na badala yake watakuwa na mamlaka ya kuamuru matumizi ya mali za taasisi za umma pekee.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 7** ya Muswada inaanzisha Kamati Elekezi ya Kitaifa ya Usimamizi wa Maafa. Moja kati ya hoja kubwa zilizoibuliwa wakati wa uchambuzi ni idadi kubwa ya wajumbe wa Kamati hiyo, ambayo ilikuwa inajumuisha Mawaziri wenye dhamana katika sekta karibu zote. Aidha, kwa kuzingatia kwamba suala la usimamizi wa maafa ni jambo ambalo linapaswa kufanyika kwa haraka, uchache au wingi wa wajumbe una uhusiano wa moja kwa moja na ufanisi wa kufanya maamuzi ya haraka. Kamati pia ilizingatia uzoefu unaopatikana katika nchi nyingine, ikiwemo India ambapo Kamati inayofanana na hii ina Wajumbe wasiozidi tisa (9). Baada ya majadiliano ya kina na Kamati, Serikali imeboresha ibara hii kwa kupunguza idadi ya wajumbe wanaounda Kamati Elekezi ya Kitaifa ya Usimamizi wa Maafa.

**Mheshimiwa Spika**, tathmini ya idadi ya Wajumbe iliyofanywa na Kamati katika **Ibara ya 7**, pia imefanyika katika **Ibara ya 9** inayoanzisha Kamati ya Wataalam ya Kitaifa, **Ibara ya 15** inayoanzisha Kamati ya Wataalam ya Mkoa ya Usimamizi wa Maafa, pamoja na **Ibara ya 19** inayoanzisha Kamati ya Wataalam ya Jiji, Manispaa, Mji na Wilaya ya Usimamizi wa Maafa kwa muktadha wa kupunguza idadi ya Wajumbe wa Kamati hizo. Serikali pia imefanya maboresho katika Ibara hizo kwa kuondoa wawakilishi na kutambua wajumbe kutokana na nafasi zao. Aidha, maboresho yamefanyika kwa kupunguza idadi ya wajumbe wa Kamati za Wataalam katika ngazi husika.

### 2.3.3 **Sehemu ya Tatu ya Muswada**

**Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu** inahusu Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa na Operesheni Wakati wa Maafa. Kimsingi, sehemu hii inaainisha wajibu kwa Serikali kuandaa mipango, bajeti na mikakati inayolenga kuainisha hatari za majanga yanayoweza kutokea, na hatimaye kuzuia na kupunguza madhara ya majanga na kujiandaa na kukabiliana na maafa.

**Mheshimiwa Spika**, katika **Ibara ya 31** ambayo inabainisha Wajibu wa Jumla, Kamati ilifanya tathmini na kubaini kwamba kuna ombwe la kukosekana masharti ya uwajibikaji kwa Sheria inayopendekezwa kutoweka adhabu. Pamoja na kwamba Sehemu ya Tano ya Muswada imeweka Masharti ya Jumla na kuweka makosa na adhabu, bado kuna umuhimu wa Sehemu hii inayobainisha wajibu pia kuwa na masharti ya adhabu. Baada ya majadiliano ya kina, Serikali imezingatia maoni ya Kamati kwamba itaongeza ibara mpya itakayoweza masharti ya adhabu za jumla kwa makosa yote yanayohusiana na ukiukwaji wa masharti ya Muswada.

### 2.3.4 **Sehemu ya Nne ya Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya hii inaanza Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa, kuainisha vyanzo vya fedha vya Mfuko huo, na kuweka masharti yanayohusu matumizi ya fedha za Mfuko ikiwemo kumtambua Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana na maafa kuwa Afisa Masuuli. Moja kati ya mambo ya msingi ambayo kwa uchambuzi wa Kamati yanapaswa kuwekwa utaratibu mzuri wa kisheria, ni namna bora ambayo Mfuko huu utatumika ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba fedha za Mfuko zinalindwa ili zitumike kwa matumizi ya Kuzuia Majanga na Kukabiliana na Maafa tu na si kwa matumizi mengine.

### 2.3.5 **Sehemu ya Tano ya Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tano inahusu Masharti ya Jumla, ikiwemo makosa na adhabu ambayo yanatokana na utekelezaji wa usimamizi wa

maafa. Aidha, katika Sehemu hii ya Muswada, Waziri Mwenye Dhamana na maafa amepewa mamlaka ya kutengeneza Kanuni kuhusu suala lolote ambalo ni la lazima kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria inayopendekezwa.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 36** inabainisha Makosa na Adhabu. Makosa yanayoainishwa ni pamoja na mtu kukataa kutoa ushirikiano kwa afisa anayetokeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria hii, au kwa makusudi kutoa taarifa za uongo au za kupotosha wakati akijibu maswali anayoulizwa na afisa kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii. Moja ya adhabu inayopendekezwa ni faini isiyopungua shilingi milioni moja au kifungu kisichoziidi mwaka mmoja au vyote. Kwa tathmini ya Kamati, adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni moja haina ukomo na inaweza kutumika vibaya. Baada ya majadiliano ya kina, Serikali imezingatia tathmini ya Kamati na hivyo kupunguza adhabu hiyo na pia kuweka ukomo.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 Maoni na Mapendekezo ya Kamati

#### 3.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022 kwa Lugha ya Kiswahili. Pamoja na kwamba nia ya Bunge inabaki kuona Sheria zetu zinatungwa katika lugha inayoeleweka, hatuwezi kukwepa ukweli kwamba, matumizi ya lugha ya Kiswahili pekee katika uandishi wa Sheria unaleta changamoto hasa katika matumizi ya maneno na tafsiri. Changamoto kama hizi zinapaswa kuwa kichocheo chenye lengo la kuongeza ufanisi wa matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika Uandishi wa Sheria mbalimbali nchini ili lugha yetu iendelee kukua.

#### 3.2 Maoni na Mapendekezo Mahsus

##### Elimu kwa Umma

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Serikali kutoa elimu ya mara kwa mara kwa umma, kuhusu hatua za kuchukua panapotokea majanga ili kupunguza athari za maafa. Elimu hii itolewe katika shule za msingi na awali, maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu na yenye shughuli nyingi, pamoja na kwenye vyombo mbalimbali vya habari.

##### Maboresho ya Sera

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kwamba Sera ya Menejimenti ya Maafa ya Mwaka 2004 imekuwa ndio nyenzo kuu inayoweka dira ya suala zima la

usimamizi wa maafa, ni vyema Sera hiyo ikahuishwa ili iendane na wakati. Aidha, Sera hiyo iweke mkazo kuhusu suala la ushirikishwaji, na ushiriki wa sekta zote katika kukabiliana na maafa.

### **Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuandaa haraka Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa. Katika maandalizi ya Mkakati huo, kwa kadri itavyowezekana, Serikali ishirikishe makundi na wadau wote muhimu ili kuboresha mawanda ya utekelezaji wa Mkakati huo.

## **SEHEMU YA NNE**

### **4.0 HITIMISHO**

#### **4.1 Shukrani**

1.	Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb.	Makamu
2.	Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.	Mjumbe
3.	Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb.	Mjumbe
4.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.	Mjumbe
5.	Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.	Mjumbe
6.	Mhe. Zainab Athman Katimba, Mb.	Mjumbe
7.	Mhe. Lemburis Saputu Mollel Noah, Mb.	Mjumbe
8.	Mhe. Asha Abdullah Juma, Mb.	Mjumbe
9.	Mhe. Omar Ali Omar, Mb.	Mjumbe
10.	Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb.	Mjumbe
11.	Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.	Mjumbe
12.	Mhe. Ahmed Juma Ngwali Dedi, Mb.	Mjumbe
13.	Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb.	Mjumbe
14.	Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb.	Mjumbe
15.	Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mb.	Mjumbe
16.	Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb.	Mjumbe
17.	Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb.	Mjumbe
18.	Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb.	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru kwa dhiti Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, ambao katika kutekeleza majukumu yao kikatiba, walichambua, kujadili, na kutoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya Muswada huu. Kwa kutambua mchango wao, naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ifuatavyo: -

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kwamba baadhi ya Wabunge ambao walikuwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria wakati wa Uchambuzi wa Muswada huu, sasa ni Wajumbe wa Kamati nyingine, sina

budi kuwashukuru sana kwa mchango wao ambao ni sehemu ya Taarifa hii. Wajumbe hao ni: -

1. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb.
2. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb.
3. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb.
4. Mhe. Elibariki Immanuel Kingu, Mb.

Aidha nichukue fursa hii kuwakaribisha Wabunge walioteuliwa hivi karibuni kuwa Wajumbe wapya wa Kamati hii ambao ni: -

1. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb.
2. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb.
3. Mhe. Rashid Abdalla Rashid, Mb.
4. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb.
5. Mhe. Mohamed Lujuo Monni, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb.) akisaidiwa na Naibu Waziri wa Nchi katika Ofisi hiyo, Mhe. Umy Hamisi Nderiananga (Mb.), kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada. Aidha, nawashukuru Watendaji wote chini ya Ofisi hiyo, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. John Anthony Jingu, Naibu Katibu Mkuu, Ndg. Kaspar Kaspar Mmuya kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee niwashukuru Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelewa J. Mwihambi, *ndc*, kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. Namshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Ndg. Athuman Hussein, *ndc*, akisaidiwa na Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Gerald Magili, kwa kusimamia utendaji wa Kamati mbalimbali za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wa Bunge ambao wanaunda Sekretarieti ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria iliyohusika na uratibu wa vikao vya Kamati na kutoa ushauri wa kitaalam wakati wa Uchambuzi wa Muswada hadi kukamilika kwa taarifa hii. Watumishi hao ni Ndg. Elihaika Mtui, Ndg. Yona Kirumbi, Ndg. Evelyne Shibandiko, Ndg. Rebecca Balisidya, na Ndg. Daniel Zephaniah wakisaidiwa na Ndg. Theresia Jacob.



13 SEPTEMBER, 2022

#### 4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, inalishauri Bunge kuujadili, kuukubali na kuupitisha **Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 1 wa Mwaka 2022** pamoja na Marekebisho yake kama ulivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb.

**MWENYEKITI**

**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria**

13 Septemba, 2022

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa mawasilisho hayo.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha hapa ya Wabunge ambao wameomba kwa ajili ya kuchangia kwenye Muswada huu, tutaanza na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kama mchangiaji wa kwanza, awali ya yote niishukuru sana Serikali kwa kuleta Muswada huu katika kipindi hiki. Kutokana na changamoto za kimazingira na kadhalika masuala haya ya maafa yamekuwa ni *issue* kubwa sana sasa hivi, hasa katika baadhi ya nchi zetu hizi ambazo huduma za bima hazijawafikia watu wote, watu wamekuwa wakiachwa maskini kwa sababu ya matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, sheria hii imekuja kwa ajili ya kutekeleza, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, sera ile ya mwaka 2004 ambayo imejikita zaidi katika mambo manne, ya kuzuia, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali baada ya maafa kutokea.

Mheshimiwa Spika, sheria ya sasa imezingatia sana kuingiza suala la maafa katika mfumo rasmi wa uongozi, ndio maana kuna kuwa na Kamati za Maafa kuanzia ngazi ya Vijiji, Kata na kupanda juu tofauti na hapo awali ambapo maafa yakitokea tunaanza kutazama Waziri Mkuu yuko wapi au *Red Cross* wako wapi, lakini sasa imeingia katika mfumo, kwa hiyo yakitokea maafa tunaanza kutazamana wenyewe kwa wenyewe pale kijijini kwamba tumefanya nini ili kudhibiti hali hiyo ambayo imetokea.

Mheshimiwa Spika, sasa ili basi tuweze kufanikiwa, sheria hii nayo ifanye kazi isije ikawa kama ile Sura ya 242 tunayoifuta leo, yako mambo makubwa mawili nafikiri ya kuzingatia. La kwanza, ni suala zima la elimu juu ya kusimamia haya maafa yanapotokea. Hii iko kwenye ngazi mbili; ngazi ya kwanza ni mashuleni na mashuleni isifanyike tu kwa kutumia chaki na ubao, lakini iwe ni halisia katika maana kwamba watumie hasa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuja mashuleni na kufanya zile *drills* kuwaonyesha kabisa watoto nini cha kufanya janga linapotokea.

Mheshimiwa Spika, kwenye Jimbo langu la Mwanga yaliwahi kutokea majanga ya moto shuleni mara tatu mfululizo ndani ya kipindi cha wiki moja. Hii ilidhihirisha kabisa kwamba vijana wale hawakuwa na elimu yoyote ya kukabiliiana na maafa haya, kwa sababu kama wangekuwa na elimu hiyo basi, lilipotokea shule ya Jirani, *actual* moja lilitokea kwenye shule moja kwanza katika bweni la wasichana na baadaye likatokea katika bweni la wavulana. Wangekuwa na elimu kidogo basi ingewasaidia hata katika kukabiliiana na lile lisingejirudia kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo la kwanza ni elimu huko kwenye shule watoto wanapokwenda, lakini la pili ni kwenye hizi kamati ambazo tunaziunda, haitasaidia chochote kama tukiunda Kamati ya Maafa pale Kijijini au kwenye Kata lakini tusipowapa mafunzo ya kutosha, maafa yatakuwa yanatokea lakini wanakuwa hawana uwezo wa kufanya chochote, kwa hiyo lazima tuzingatie sana mafunzo kwa hawa.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni uwekezaji katika maana ya vifaa vya kushughulika na mambo kama hayo. Utakuta wilaya nzima au hata wilaya mbili, tatu zinazopakana hazina hata gari moja la zimamoto. Napendekeza kabisa kwamba, Serikali ihakikishe kwamba kwa kuanza tu angalau kila wilaya iwe na gari la zimamoto lililoko kwenye hali nzuri na linalofanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba suala hili la maafa ni suala mtambuka, linahitaji ushirikiano na linahitaji uwekezaji kwenye kila sekta. Kwa mfano sasa hivi, Serikali imepeleka fedha nyingi sana kwenye maeneo mbalimbali ya ujenzi, lakini fedha hizi hazitazuia mafuriko mvua nyingi kunyesha. Sasa wataalam wetu wanapotumia fedha hizi kujenga kama ni barabara au majengo ni lazima wazingatie kwamba haya maafa yanaweza yakatokea wakati wowote ule.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni vizuri tuhakikishe kwa mfano katika halmashauri zetu tusitegemee kuwa na *engineers* peke yao wanaweza wakafanya kitu ambacho kinaweza kuwa kikamilifu, lazima tuhakikishe tuna wale wasanifu majengo (*architect*), tuhakikishe tuna *quantity surveyors*, halafu

ndio na mainjia wawepo ili ile kazi inapofanyika asitokee mtu wa kuja kumlaumu mwenzake kwamba ramani ilisema hivi lakini *quantity* hazikuwa zimezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuwawajibisha pia hawa ambao wanajenga miundombinu ambayo haiwezi kukabiliana na majanga. Inabidi uwajibikaji uwepo, fedha zile za *retention* kwenye miradi ya barabara zitumike ipasavyo, zibakie kukarabati ile miundombinu baada ya kujengwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la utafiti. Ni vema utafiti ukafanyika kwa mfano, kuna maeneo mengi tunapata maafa yanayotokana na majanga ya ukame na utakuta kwamba eneo lile lingeweza kustawi mazao yanayostahimili ukame, lakini hakuna utafiti uliofanyika, wale wakulima wakashauriwa, wakalima kitu ambacho kinaweza kikabiliana na hali ambazo tunazo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa kumaliza tu, niseme kwamba Muswada huu umekuja wakati muafaka, tunahitaji sana haya yaliyoko ndani ya sheria hii, lakini la muhimu ni kuzingatia masharti ya utekelezaji wa yale yaliyosemwa humu, vinginevyo tunaweza tukajikuta baada ya muda tunaifuta tena kama tunavyofuta hii Sura ya 242.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka atafuatiwa na Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko ajiandae.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia huu Muswada wa Sheria ya Maafa. Naipongeza sana Serikali kwa kuona kwamba kuna umuhimu wa kuboresha hii Sheria ya Maafa hasa baada ya kufuta ile Sura 242 ambayo ndio tulikuwa tunaitumia kabla ya hii mpya. Hata hivyo, nina mchango mdogo kwamba tunapofuta ile sura 242, je, kwenye hii mpya tutakuwa na kitu gani kipyamba ambacho kinaweza kuboresha hii Sheria yetu ya Maafa.

Mheshimiwa Spika, maafa ambayo yanaleta majanga ni kitu cha ghafla, ni kitu cha dharura, mara nyingi huwezi kujua kinatokea wakati gani. Bado nasema ni muhimu sana kuzuia kabla ya jambo lenyewe halijatokea. Kwa mfano, kuna majanga ambayo tunayaona kabisa kwa macho na watu wanapita, kama vile mtu kuchimba kwenye daraja mchanga na tunajua kabisa, watu wa mamlaka mbalimbali wanapita pale kwa mfano madaraja ambayo na treni inapita, inachimbwa michanga pale.

Mheshimiwa Spika, sasa treni itakapokuja kuanguka kwa bahati mbaya katika maeneo yale, yale ni majanga ambayo tungeweza kuyazuia kabisa. Sasa kitengo hiki ambacho kiko chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hii *Division* ya Maafa ni vizuri sana wakawa wanaangalia kwanza kuzuia kuliko kuangalia namna gani watahughulikia hayo maafa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napitia *best practice* kwenye nchi za wenzetu, sana kwenye kamati tuliangalia nchi karibu mbili; tuliangalia ya India kama alivyosema Mwenyekiti wetu wa Kamati kwenye ripoti, lakini pia na Afrika Kusini. Kwa mfano wenzetu wa Afrika Kusini wana kitu kinaitwa *Disaster Management Act* ya mwaka 2005, ndani yake kuna Mpango wa Taifa wa namna ya kushughulikia mikakati maalum ambayo mingine kama itampendezesha Mheshimiwa Waziri, kuna sehemu ambazo ni muhimu sana kwa mfano chapter 12 kwenye hizo *guidelines* zao, kuna *minimum standards* za *relief* kunapotokea majanga.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, yale majanga ambayo yako kwenye ile *magnitude* kubwa kabisa, kuna watu wanakuwa wamekopa fedha benki kwa mfano na kipindi kile cha majanga hawa hawawezi kulipa tena benki, lakini wakati huo benki zinaendelea kuwachaji *interest* na vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, sasa wao wana-*relief standards* za kuangalia *magnitude* ya ile *disaster* yenyewe watawasaidia watu namna gani, lakini ukiangalia hiyohiyo ya wenzetu wana *special provisions* kwa watu ambao ni wajane, lakini pia na kwa *orphans*. Wanaangalia kwamba sasa watu hawa tutawasaidiaje katika kipindi kama hiki cha majanga makubwa kwamba hawa yatima pamoja na wajane wanasaidiwa kuna *special unit* kwa ajili ya kuwasaidia hawa. Kwa hiyo na sisi ni vizuri pamoja na kutunga vizuri hii sheria yetu tuangalie na wengine wanafanikiwa namna gani ikiwemo hiyo ya wenzetu wa Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kuondoa mlolongo wa Mheshimiwa Waziri kwenye ile Sura Na.6 kipengele (c) kuondoa yale mamlaka ya Mheshimiwa Waziri ya kukamata mali ya mtu yeyote ambayo ingeweza kutumika wakati wa majanga. Kulikuwa na shida na hasa majanga yanapokuwa yamepita au yamepungua kwa kuwa na shida kubwa inatokea namna ya kuwa-*compensate*, kuwalipa fidia hawa ambao mali zao zilikuwa zimechukuliwa kwa ajili ya kutumika kwenye majanga. Sasa kwa kuwa pia na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wameondolewa madaraka hayo zimebaki taasisi peke yake, naishukuru sana Serikali kwa kukubali ushauri wetu Wanakamati na kuondoa vipengele vya namna ile.

Mheshimiwa Spika, lingine limeongelewa hata kwenye ripoti yetu kulikuwa na mlolongo wa kamati watu ni wengi mno, inatokea janga inianza

mikutano ya wale wanakamati ni wengi kweli, mpaka watu wanakwenda kwenye tukio mambo yalishaharibika zamani kwa sababu ya wingi wake na kwa kadri watu mnavyokuwa mko wengi mnaangalia na akidi nayo vilevile inakuwa shida, lakini kwa kukubaliana na ushauri wa Kamati kupunguza idadi ya hawa ambao wanashughulikia maafa, naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, hii Sera ya mwaka 2004 ambayo tunaitumia ya mambo ya Sera ya Taifa ya Maafa, sera ile ni nzuri ingawa tumependekeza iboreshwe, sasa shida ya sera ni moja hata ingekuwa nzuri sana mara nyingi sera kwenye sheria *not enforceable* yani ile sera yenyewe uwezi ukaifanyia kazi moja kwa moja kisheria hata ingekuwa ni nzuri kiasi gani. Sasa waangalie katika kuendelea kuboresha hizi sheria zetu za maafa yale mambo ambayo ni mazuri sana kwenye sera zetu tuweze kuyaingiza kwenye sheria kamili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya machache, naunga mkono hoja na ahsante kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko na Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, ajiandae.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii nami kusema machache juu ya Muswada huu ambao ni wa muhimu na umeletwa kwa wakati muafaka kabisa. Awali ya yote, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima na kutujalia kufika hii leo na kusema machache mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mwanzo kabisa ningependa kuchukua fursa hii kutoa salamu zetu za rambirambi kwa familia ya Malkia Elizabeth wa pili aliyefariki, yeye ni kama Rais, Malkia ni *head of state* wa United Kingdom kwa familia yake na Serikali ya Uingereza kwa wananchi wa Jumuiya za Madola na wote wale ambao wameguswa na msiba huo. Tunapenda kusema poleni sana, Mwenyezi Mungu awajalie subira wote waliofikwa na huo msiba mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pili, ningependa vilevile kuzungumzia Muswada huu kwa ujumla wake. Maafa ni jambo ambao linaweza kutokea wakati wowote na suala mtambuka. Mara nyingi tukizungumza tunafikiria nini kinaweza kuleta maafa, lakini kuna maeneo mengi tu. Maeneo ambayo yanaweza yakasabishwa na sisi na maeneo ambayo yanaweza yakatokea tu kwa kudra za Mwenyezi Mungu, lakini maafa yanatabirika, siyo yote lakini sehemu kubwa ya maafa yanatabirika.

Mheshimiwa Spika, sasa wenzetu wa nchi za kimataifa wana mifumo ambayo inawasaidia kuwa na *early warning mechanisms*. Sasa sijui tutatafsiri

vipi hiyo lakini ni taarifa za awali za mapema ambavyo ni viashiria pengine maafa yanaweza yakatokea. *Climate change* tunajua mnaweza mkawa hampati mvua, mkaanza kuona wanyama wanafariki, ukame na athari zake. Migogoro ya kivita inaweza ikawa sio nchini kwenu lakini vita ikitokea jirani mauaji ya kimbari jirani hapa sisi kama Tanzania tumeyaona yote hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa yote haya yanahitaji mambo makuu manne; mipango, uhakika wa utekelezaji, fedha, *resource mobilization* yaani jinsi mbadala na mtambuka wa kuzitafuta hizo fedha kutusaidia katika hayo maafa na wakati mwingine utaalim ambao pengine sisi tusiokuwa nao katika sekta fulani au katika maafa fulani.

Mheshimiwa Spika, sasa yote haya yanahitaji mambo makuu manne; mipango, uhakika wa utekelezaji, fedha, *resource mobilization*, yaani jinsi mbadala na mtambuka wa kuzitafuta hizo fedha kutusaidia katika hayo maafa. Wakati mwingine utaalim ambao pengine sisi tusiokuwa nao katika sekta fulani au katika maafa fulani. Ukiangalia hii sheria inagusia mambo yote hayo. Inaweka mfumo ambao tutakuwa tuna mpango yakitokea maafa tunajipanga vipi. Pili, nani anahusika kutekeleza na kukabili yale maafa ambayo yametokea. *Resource mobilization* kuna watu, ukiangalia Wizara ya Fedha - *Treasury* ipo lakini haizuii taasisi za nje ambazo zipo tayari kusaidia vilevile kwa sababu mfumo huo upo.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hii sheria katika ngazi zote, kuanzia ngazi ya juu kabisa Kitaifa, Mkoa, Wilaya mpaka chini, inatoa fursa ya kuleta wataalam wa sehemu mbalimbali au wa sekta mbalimbali kuja kuleta mchango wao ili kutusaidia katika tatizo au janga ambalo limetukuta.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi, Muswada huu umekuja kwa wakati, tunawashukuru Serikali kwa kuwa wazi kwa kuchukua maoni tofauti, kwa sehemu kubwa Kamati imeweza kutoa maoni sehemu kubwa ya haya maoni yamepokelewa na Serikali na yamefanyiwa kazi hadi kupata Muswada huu ambao sina shaka yoyote unakidhi vigezo kwa Karne hii ya 21.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuchangia hoja na kuiunga mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka ajiandae.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, ambaye kiukweli ndiye anayejaribu kuleta furaha kwa Watanzania na kutufuta machozi kupitia Wizara hii kupitia kwa Kiongozi wetu Mheshimiwa George Simbachawene, kwa sababu unapofanyia kazi maafa maana yake unataka kuleta furaha na kuondoa huzuni kwa Watanzania, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Mwinyi anamalizia, amesema maafa yanakuja kwa dharura lakini maafa yanatokana na majanga mbalimbali. Yapo majanga ambayo yanasababishwa na shughuli za binadamu, lakini yapo majanga ambayo yanakuja kwa kadri ya Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Muswada huu, hasa katika dhumuni, malengo na sababu ya Muswada inalenga katika kuzuia majanga. Ninawapongeza sana Wizara pamoja na Kamati ya Katiba na Sheria, wamefanya kazi nzuri ya kujikita zaidi katika kuzuia majanga na siyo kupambana na changamoto za majanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongezee tu jambo kwamba ili kuzuia haya majanga, kuna maeneo mengi ya kufanyiakazi, eneo kubwa na muhimu ambalo ninapenda Wizara walichukue ni matumizi mazuri ya Jeshi letu la Zimamoto, hasa kupitia mipango miji katika Majiji na Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, tumeona changamoto kubwa ya maafa yanayotokana na moto kushindwa kuzimwa ama kudhibitiwa kwa wakati ni kutokana na magari yale kushindwa kuingia katika eneo la matukio kwa sababu ya kukosa njia au barabara ya kufika huko. Kwa hiyo wakati tunapambana na njia za kuzuia, wakati tunapambana namna ya kuelimisha jamii mara kwa mara, tuangalie namna ambavyo Kamati zote hizi ambazo zimetajwa kwenye Muswada huu zitasaidiwa katika kupanga vizuri Miji na kutoa nafasi ya vikosi vyetu vya zimamoto kuweza kufanya kazi kwa ufanisi mara majanga hayo yanapotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majanga yanatokea kwa dharura, lakini majanga yanaweza kukingwa kama tutatoa elimu ya kutosha. Katika majukumu ya Kamati elekezi za Wilaya, Kamati za Mikoa mpaka kwenye Mitaa na Vijiji, pamoja na majukumu mazuri mengi ambayo yameainishwa pale, sijaliona jukumu la Kamati hizi kutoa elimu za kila siku namna ya kukabiliana na majanga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaishauri Serikali kwamba wakati wanajumuisha watusaidie namna ya kuingiza litamkwe kisheria kwamba Kamati hizo zisisubiri janga litokee ili wadhibiti, ziendeele kutoa elimu kadri muda

unavyokwenda, kadri hali ya hewa na majanga mbalimbali yanavyotokea ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu kutokupoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, nimesoma Ibara ya 17, kipengele kile cha Kwanza kinatamka kwamba Kamati ya Usalama ya Wilaya itageuzwa tu kuwa Kamati Elekezi ya Maafa ya Wilaya. Lakini katika Kamati ile elekezi, haijamtaja Mkurugenzi wa Halmashauri, imemtaja Mwenyekiti wa Halmashauri au Meya wa Jiji, imemtaja Mbunge mwenye Jimbo katika Wilaya ile lakini Mkurugenzi wa Halmashauri hajatajwa, pengine ni kwa sababu kuna Kamati elekezi ya maafa kwenye ngazi ya Jiji au Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, nini faida ya kumtaja Mkurugenzi kwenye Kamati ya Wilaya; Kamati ya Wilaya kwa maana ya Kamati ya Usalama itatoa maelekezo, Namna nzuri zaidi ya kufikisha katika utekelezaji kwenye Majiji au Halmashauri ni Mkurugenzi Mtendaji kuwa mule ndani, yeye hajatajwa kwenye ile Sheria ya Baraza la Usalama kama Mjumbe kwenye Kamati ya Usalama, lakini hata katika Wajumbe walioongezwa na kwenyewe hajatajwa. Kwa hiyo, akiunganishwa hapo Kamati hiyo itakuwa na namna nzuri zaidi ya utekelezaji hasa kwa kuwa na yeye ni Afisa Masuuli kwenye ngazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Ibara ya 17, naomba pia nitoe ushauri katika Ibara ya 34 ambapo amesema kutakuwa na Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa. Tunazungumzia ile dhana ya ugatuaji wa madaraka. Kama tunataka kwa dhati kabisa kudhibiti maafa kwenye ngazi za chini kabisa, ni vizuri huu mfuko ukapelekwa kwenye ngazi ya Mkoa, huu mfuko uonekane pia kwenye ngazi ya Wilaya, ngazi za Kata na kadhalika huko chini.(Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa nini? Tunazungumzia majanga ambayo ni *natural*, lakini yapo majanga ambayo yanasababishwa na binadamu. Tuna majanga madogomadogo pia, kwa mfano juzi katika Wilaya ya Handeni wananchi kadhaa wamejeruhiwa na tembo pale. Maeneo mengine unakuta upepo tu unaezua nyumba, nyingine ni nyumba za nyasi, nyingine za bati, lakini watu wanapata shida, wanajeruhiwa, wanahitaji msaada. Sasa namna ya Wilaya au Kata kusubiri mfuko ambao upo Wizarani kuja kusaidia wale wananchi pale inakuwa ni shida. Wakati mwingine kukusanya michango kwa maana ya usimamizi wa rasilimali inakuwa ni mtihani mpaka mtu aridhie atoe, lakini inaweza kumchukua muda kutoa chochote kwa ajili ya kwenda kusaidia.

Mheshimiwa Spika, ili kulinda hiyo hali ninashauri sana, kwanza huu Mfuko ionekane ni namna gani utakwenda kwenye ngazi za chini, wawe na uhakika wa matumizi ya dharura panapotokea jambo hili. Pili, sheria itamke kwamba ikiwezekana kwenye Halmashauri zetu kama ambavyo tunatenga asilimia fulani ya mapato ya ndani kwa ajili ya majukumu mengine, hata ikiwa ni



asilimia moja tu, itengwe kwa ajili ya kuratibu majanga kwenye *Councils* zetu. Hii itatusaidia kufanya *action* ya haraka pale ambapo janga linatokea. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, naunga mkono hoja na sheria hii imekuja wakati muafaka kabisa, ninapenda kuishauri Serikali kwamba utekelezaji wake ufanyike kwa haraka kwa ajili ya kuendeleza au kulinda furaha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Sekiboko. Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu kwamba michango hii inahusu utungaji wa sheria na tuko kwenye huu Muswada ambao umeshasomwa mara ya pili, tumesikia mawazo ya Kamati kuhusu Muswada huo na tumesikia yale ambayo Serikali imekwisha kuyachukua.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hivyo kwenye ngazi hii ukiwa unapendekeza mabadiliko kwenye ule Muswada maana yake hapa mbele niwe tayari na marekebisho yako, yaani kwamba unayatetea, unataka Waheshimiwa Wabunge wakuunge mkono itakapofika ngazi ya kuanza kupitia kifungu kimoja baada ya kingine, tusipofanya hivyo tutakuwa sasa hatutungi tena sheria.

Waheshimiwa Wabunge, mawazo ya ziada unayoyatoa labda uyatoe na wewe kwa kuashiria kwamba ni ya ziada ili Kanuni ambazo Sheria inayotungwa leo inaruhusu Waziri kwenda kutunga Kanuni, wakayatazame kwenye ngazi ya Kanuni. Lakini ukizungumzia Vifungu vya Sheria na mabadiliko, kama hujaleta hapa hayo mabadiliko, hayo mawazo hata Waziri wala hatarajiwi kwamba atatoa majibu hapa mbele, kwa sababu tuko kwenye ngazi ya kutunga sheria.

Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi na mimi nitoe mawazo yangu kwa Muswada huu wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 1 wa mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Katiba na Sheria kwa kuwasilisha vizuri sana mada hii. Vilevile niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa michango mizuri, na walitoa mawazo mazuri sana wakati tunajadili Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali vilevile wakati wa mijadala na Kamati, kwa kweli wamechukua mawazo karibu yote ambayo yalikuwa yanasemwa na Kamati, hili ni jambo jema sana. Ninawashukuru pia wale ambao tuliwaalika waje watoe maoni yao na walikuja *Tanganyika Law Society* na wengine wengi, tulibahatika kama Kamati, tulinufaika sana na michango yao.

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema Wabunge wengine, Muswada huu umekuja wakati muafaka kabisa, tayari sheria tuliyokuwa nayo, *The Management Act 2015*, ilikuwa inaleta mkanganyiko mkubwa wa namna Serikali inavyojiandaa kukabiliana na maafa. Niwapongeze Serikali kwa kujaribu kufanya *case studies* nyingi. Wameangalia Sheria ya Afrika Kusini, sheria ya India na maeneo mengine kwa ajili ya kuboresha Pamoja na *international standards by the way*.

Mheshimiwa Spika, *concept* moja nzuri sana kwenye Muswada huu ni *concept* inaitwa Afya Moja (*One Health Concept*). Ni *concept* ambayo ni jumuisi, kwa kuwa majanga ni mambo ambayo ni *complicated* kidogo inagusa karibu kila mahali, walivyokuja na *approach* hii ya *One Health Concept* (Afya Moja) imesaidia Muswada huu kutengeneza a *holistic approach* kwenye namna ya kukabiliana na maafa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Kamati yetu ya *January/February 2022* kulikuwa na wazo la Bunge la kuiomba Serikali kwamba wakati wa kuleta Muswada huu wahakikishe kwamba Waheshimiwa Wabunge na wao wanakuwa sehemu ya hizi Kamati za maafa. Nafarijika sana kwamba Serikali imelisikia hili katika Ibara ya 11(2) utakuta uwakilishi. Tena tuliwaambia uwakilishi kwa ngazi za wilaya na mikoa, lakini wao walivyotengeneza ile *structure* kutoka Taifa wamewaweka Wabunge hata kwenye *level* ya Kitaifa, *big up*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 11(2), Ibara ya 13, Ibara ya 17 na Ibara ya 22 ya Muswada huu, kwa hiyo utaona kabisa kuanzia ngazi ya Taifa, mkoa, wilaya mpaka na Madiwani wapo. Kwa sababu wakati wa mijadala ilikuwa ni kitu cha ajabu kidogo kwamba, maafa yanatoka halafu kuna watu wanakaa kujadili halafu Mbunge ambaye ni Mwakilishi wa wananchi yuko nje. Akiulizwa na wananchi nini kinaendelea anasema tsubiri Kamati na vikao vitoke. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri, *this is a very good initiative*, itatufanya na sisi sasa tuanze kushiriki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tena mmefanya vizuri kwa sababu mnajua kazi ya Bunge ni *oversight*, kwa hiyo hamjawaweka kwenye zile Kamati zinazofanya kazi, ni zile Kamati elekezi ili waweze kuendeleza lile jukumu lao la *oversight*. *Big up*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kingine ambacho ni *innovation* nzuri sana, kuanzisha Mfuko huu wa Usimamizi wa Taifa, lakini kubwa kuliko yote ni kuruhusu sasa sheria iseme kwamba ni lazima Serikali itaweka pesa inayopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ni *initiative* nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Sheria ambayo sasa itafutwa baada ya Sheria hii kupita, ilikuwa inazungumza habari ya kutafuta hela za misaada, *donations* na vitu kama hivyo, lakini sasa ni jukumu la nchi kuweka sehemu ya bajeti yake kwenye Mfuko huu. Hii ni *innovation* nzuri sana. Unajua hata kabla hujaongea na wengine wanaokuchangia lakini umeshaweka *commitment* ya kwako ya fedha inayopitishwa na Bunge, nadhani ni *initiative* nzuri sana. *Big up. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kimsingi hata nchi nyingine – tutaangalia baadaye – *in fact* wamefika mahali wana-*dictate* kuweka *percent* fulani ya *National Budget*. Hiyo ni *stage* ya juu sana lakini ninyi mmeanza vizuri kwa kuruhusu Bunge hili lipitishwe bajeti ya kuweka pesa kwenye Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu vilevile kilichonifurahisha sana ni kwamba imetajwa *Red Cross* hapa. *Red Cross* kwa kweli Wabunge wengi hapa ni mashahidi – wamekwenda kila Jimbo. Kiteto, Manyara, kila mahali, kuweza kutambua mchango wa *Red Cross* nchi hii na kuwajumuisha kwenye Kamati hizi ni *innovation* nzuri sana. Tunawaomba tu muendeleo kuwapa *support* nzuri wanayohitaji ili waweze kusaidiana na Serikali katika jukumu hili.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Muswada huu vilevile utakutana na *volunteers* (watu wanaojitolea), kwa sheria kuthamini na kutaja *role* ya *volunteers* vilevile ni kitu kizuri sana, ita-*encourage* watu waendeleo kujitolea kwenye masuala haya ya majanga. Tunachoomba tu Serikali, pamoja na kwamba maafa ni jambo ambalo kuna Kamati nyingi na kuna watu wengi wanaohusika, sisi tunachoomba tu ni kuangalia suala la urasimu, isije ikawa ile *complication* ya watu wengi kuwepo ikaleta urasimu katika kufanya vikao na *of course budget wise*, isije ika-*inflate budgets unnecessarily* kwa sababu tunavutana kutafuta pesa kwa ajili ya majanga haya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nashukuru na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Mheshimiwa Elibariki Emmanuel Kingu ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia Muswada ulio mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme mimi siyo Mwanasheria lakini yapo mambo ambayo nimeyaona kwenye Muswada huu, naomba niyazungumze, Mheshimiwa Spika utatuongoza tutayaweka wapi ili tujue tunayaweka kwenye nafasi ipi.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Serikali kwa kuleta Muswada huu kwa sababu sasa hivi kutokana na maendeleo ya kibinadamu, teknolojia na shughuli mbalimbali za kibinadamu, huu Muswada ni mahali pake.

Mheshimiwa Spika, nianze na tafsiri ya neno maafa kwa mujibu wa nilivyoiona aya hii. Wameeleza kuwa maafa ni madhara yanayotokana na majanga ambayo yanajumuisha uharibifu wa mifumo ya kawaida katika jamii ambao unaweza ukasababisha vifo, majeruhi, madhara ya kisaikolojia, upotevu au uharibifu wa mali na kuendelea. Lakini mwisho wa tafsiri hiyo wakasema ni yale ambayo jamii au yule aliyepata madhara hawezi ku-recover, ndiyo yanakuwa sasa yale ni majanga.

Mheshimiwa Spika, sasa shida yangu ni kujua ni nani huyu sasa atakayesema kwamba janga hili haliwezi kuingia kwenye maafa kwa sababu jamii husika inaweza ika-cover, hapa ndipo napata shaka kidogo kwenye hii. Kwamba ni nani sasa huyo ambaye atakuja kusema kwamba kwa extent ya madhara haya yanafaa kuitwa maafa au haya hayafai kuitwa maafa.

Mheshimiwa Spika, hapa niende mbali zaidi, kuna maafa ambayo naomba ni-declare interest, mimi ni mmoja wa wahanga wa maafa yaliyotokana na Uchaguzi wa 2020. Nilichomewa nyumba zangu mbili, nikachomewa na magari matatu. Sisi kwenye ngazi ya Wilaya tukaunda hiyo Kamati ya Maafa ambayo ilikwenda mbali zaidi ikaleta valuer akafanya valuation. Ile ripoti ikapelekwa Mkoani, lakini kwa mujibu wa Sheria hii wakasema maafa hayo hayamo kwenye Sheria ina maana kwamba mimi siyo mnufaika wa maafa hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa maana yangu ni nini? Je, mbona hapa kwenye sheria hapajatajwa? Kwamba yakaainishwa hayo maafa halafu wakayaondoa maafa hayo; kwamba maafa yanayotokana na uchaguzi hayatakuwa considered.

Mheshimiwa Spika, na nilikwenda mbali, nilifika mpaka kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi majibu yakawa hayo hayo. Ile ripoti ya evaluation ilifika Ofisi ya Waziri Mkuu majibu yakawa yanafanana na hayo. Lakini vilevile hata kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Spika nilifika kuomba msaada lakini ikaonekana kwamba si miongoni mwa hayo maafa. Sasa wasiwasi wangu unarejea pale pale.

Kwamba, hivi ni nani atakayeweza kusema kuwa maafa haya huyu mtu anahitaji kusaidiwa?

Mheshimiwa Spika, kwenye sheria hapa nimeona kumeundwa Kamati kuanzia ngazi ya vijiji mpaka ngazi ya Wizara au tusema Taifa, kwenye hizo Kamati za Maafa. Sasa kwenye hizi kamati kwa mfano kama ngazi ya kijiji ni nani kule kwenye ngazi ya kijiji atasema maafa ya *extent* hii yanafaa kushughulikiwa na ngazi ya wilaya na si ngazi ya Kijiji? Kwamba, huyu mtu inafaa kusaidiwa na ngazi ya mkoa na si ngazi ya wilaya? Wapi panaainishwa kwenye sheria hii ili kujua kwamba kwenye maafa haya yanakwenda kuhudumiwa na nani?

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kwamba mimi si mwanasheria. hivyo mimi nitaomba Mheshimiwa Waziri aweze kunifafanulia kwenye baadhi ya sehemu.

(a) Je, ni sura gani kwenye sheria hii inakataza kwamba madhara yote yanayotokana na uchaguzi siyo maafa?

(b) Ni kipimo gani kitakachotumika kujua kiwango cha maafa?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika Taarifa. (Kicheko)

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

## T A A R I F A

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nimeona nimpe taarifa Mheshimiwa Kuchauka. Wakati anachangia na ana-*narrate* aina ya maafa kwake yaliyompata yeye wakati wa uchaguzi kuchomewa nyumba na gari zake, nimekaa nimetafakari kwa kina nilitaka nimpe taarifa tu kama ni hayo tu ya kuchomewa nyumba na gari kama angekuwa amezikatia bima nadhani ingekuwa *taken and care off*. (Makofi/Kicheko)

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka hiyo ni ngazi ya kwanza lakini ngazi ya pili hilo jambo linakuhusu wewe mwenyewe, na Kanuni zetu zilitakiwa sasa uwe umeshasema; hayo ndiyo mazingira ya kusema natoa mchango huu lakini naeleza maslahi binafsi; yaani ndio mchango kama huu. Kwa hiyo maslahi binafsi, tena ya kifedha kiasi gani? ndiyo inavyosema sheria yetu lakini malizia mchango wako maana ulianza kwa kujitetea kwanza. Lakini hili jambo unalochangia linakuhusu wewe mwenyewe, na ni hoja yako wewe mwenyewe kwa hiyo mazingira yapo namna hiyo. Malizia mchango wako. (Kicheko)

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nafikiri pengine hukunisikia *nili-declare interest* kwenye jambo hili, nilisema kwamba mimi ni mlengwa wa moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, lakini nakubaliana na taarifa yake; pengine ni kwa sababu ile niliyoitaja kwamba mimi si mwanasheria; lakini anapozungumzia masuala ya bima na hapo bado kwenye hii sheria sijaona mahali pametajwa kwamba yaani kama ni nyumba, kama ni mali yenye bima haitashughulikiwa na sheria hii, sijaona. Kwa hiyo, bado hata kama mimi nilikuwa na bima ya magari pamoja na ya nyumba bado, kwa mujibu wa sheria hii, ninavyoona mimi kwa uelewa wangu, ni kwamba bado nilikuwa nahitaji kupata msaada kwenye mfuko wa maafa pamoja na kwamba hizi ni mali zangu zilikuwa na bima. Hii ni kwa sababu hapa kwenye sheria haijatajwa, kwamba mali ambayo itakuwa ni bima haitashughulikiwa na mfuko wa maafa.

Mheshimiwa Spika, sasa swali lingine ambalo nilikuwa nataka niombe Mheshimiwa Waziri atakapokuja anitajie ni kujua ile *level* niliyoisema. Kwamba maafa haya yanashughulikiwa na nani kwa *level* ipi? Na ni nani anayeweza kujua kwamba kwa madhara haya hii jamii inaweza ikamudu au haiwezi kumudu? Kwa mfano imetokea madhara kwenye Kijiji, labda shule ikaungua moto; nani atajua kwamba kwa kuungua ile shule kijiji hakina uwezo wa kurudishia ile shule, na kwa hiyo Serikali inahitaji kuingiza nguvu yake pale, au kuiachia kijiji au kumuachia mtu binafsi? Nataka nipate hiyo mipaka ipo sehemu gani kwenye sheria hii?

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba ianishwe mamlaka za zile kamati. Kwamba, kamati ya kijiji inaishia hapa, kamati ya mtaa inaishia hapa, kamati ya wilaya inaishia hapa; ili kuondoa mkanganyiko huu ambao mimi nimeusema. Kwamba, ukishapata yale madhara wewe *personally* unatakiwa ufuatae ngazi ipi; ujue ni ngazi ipi inapaswa ikuhudumie? Na unapokosa huduma uone kwamba sheria haijakutendea haki.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naomba niunge mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Najma Murtaza Giga atafuatiwa na Mheshimiwa Elibariki immanuel Kingu, Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba ajiandae.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Nami nitumie fursa hii kwanza kabisa kuipongeza na kuishukuru Serikali kwa kuleta Muswada huu kwa lugha ya Kiswahili kama ambavyo tulivyokubaliana katika Bunge la Kumi na Moja. Naamini kwamba sasa changamoto ambayo tunaipata sisi hapa katika kuzichakata hizi sheria kwa

luga ya Kiswahili ni zetu sisi kama Wabunge, lakini wananchi huko watapokwenda kutekeleza hizi sheria au kuzifuata hizi sheria watapata urahisi na unafuu kama ambao tumekuwa tumekusudia.

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba ni kweli kutoka kwenye Kiingereza kuja kwenye Kiswahili ni kazi yetu sisi na ngumu, hata Mheshimiwa Waziri Mwenyewe Ofisi ya Waziri Mkuu atakiri hilo. Pia ni washukuru sana Serikali kwa kukubaliana mambo mengi ambayo tumeyachakata kwenye Kamati; lakini hata na sisi pia upande wa Kamati tumekubali mambo mengine ambayo yaliletwa na Serikali. Kwa mfano kuweka jina hilo hilo kubaki kuwa ni *disaster management*, kwa maana ya kwamba tukija kwenye Kiswahili *disaster* ni majanga na maafa. Kwa hiyo, kwa uandishi bora wa kisheria tulikubaliana na Serikali na jina likabaki kuwa hivyo nasi tunaona ni jambo zuri.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo wametangulia wenzangu, kwamba, kufutwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Sura ya 242 ni jambo zuri kwa sababu tumeona kwamba utekelezaji wake ulikuwa unakinzana na Sheria ya Baraza la Usalama wa Taifa. Vilevile pia tulishindwa kwa maana ya kutekeleza Sheria au takwa la Sheria la kuanzisha Wakala wa Usimamizi wa Maafa. Kwa hiyo, hayo ni mapungufu makubwa ambayo nafikiri yamesababisha kuleta sheria hii mpya.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu wa Sheria umelenga sasa kuweka usimamizi au mfumo bora wa usimamizi wa maafa nchini. Kwa namna ambavyo ulivyokaa na baada ya uchambuzi wa Kamati na baada ya kukubaliana na Serikali, kwa kweli kama tutaweza Kwenda kutekeleza sheria na kama Kanuni zitakwenda kuwekwa vizuri katika utekelezaji wa sheria hii; basi mfumo huu utakuwa ni bora na utasaidia katika nchi yetu jinsi ya kuweza kukabiliana na maafa hayo. Hii ni kwa sababu tunakuzuia, tunakupunguza madhara lakini pia tunakabiliana nayo pale tayari yametokea lakini pia kurejesha hali baada ya hayo maafa kutokea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kubwa ambalo nimelifurahia zaidi ni kwamba pale ambapo Serikali kwanza imekubali kwenye Ibara ya Nne, nafikiri Ibara ndogo ya 2(f), kushirikiana na upande wa Zanzibar. Tunaelewa kwamba Zanzibar wana sheria zao za maafa kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Lakini Sheria hii imeweka mwanya wa fursa ya ushirikiano mwema baina ya Zanzibar na Tanzania Bara pale ambapo majanga ya maradhi ya mlipuko, kwa mfano pamoja na majanga ya kiasili yanapotokea yakaikumba Tanzania nzima ikiwemo na Zanzibar, kuweza Sheria hii kuchukua hatua kwa mujibu ambao tumeona. Kwa hiyo, tunawashukuru sana Serikali kufikiria pande zote mbili za Muungano. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini pia wakati tunazungumzia uzuri wa Sheria hii na kushauri namna Kanuni ambavyo zitakwenda kuwekwa, ushauri mkubwa

ningeomba niuelekeze katika uundaji wa hizo Kanuni kufikiria namna sasa ya kuweza kuweka elimu iliyokuwa sahihi na bora kwa pande zote; kwa watumiaji wa Sheria na wasimamizi wenyewe wa Sheria. Kwa sababu kwenye Sheria hii kuna Kamati nyingi ambazo Serikali wamepunguza idadi na kuweka kwa namna iliyobora zaidi. Kwa hili ninaipongeza sana Serikali. Kwa hiyo, wale wanaokuwa wanasimamia hizo Kamati za Wataalam na Kamati za Uelekeza kuanzia ngazi ya Taifa mpaka huku kwenye vijiji ni muhimu sana wakawa na uelewa mzuri kabisa wa utekelezaji wa Sheria hii; ikiwa na dhana ya suala la kukabiliana na maafa. Kwa hiyo, watu watakapokuwa hayo wameelewa vizuri utekelezaji wa sheria utakuwa upo vizuri. (Makofi)

Mheshimia Spika, lakini pia tukiacha upande wa hawa watu wanaosomea sheria, kuna wananchi sasa kwa ujumla; kwa sababu tunaelewa kuna maafa ya kiasilia lakini kuna maafa ambayo yanatokana na binadamu mwenyewe. Kwa hiyo, bado tunahitaji sana Serikali kuishusha elimu kuanzia shule za msingi mpaka na vyo. Vilevile wananchi wa kawaida nao pia waelewe madhara yanayotokana na kuharibu miundombinu na kuharibu maeneo yetu; kwa maana ya mazingira, ili kuepukana na maafa ambayo yanatokana na binadamu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa ufupi ni hayo; lakini nashukuru sana Serikali. Ninaamini kwamba, endapo tutakwenda kutengeneza kanuni zilizo bora basi kutokana na yale maoni na michango ya Kamati, na makubaliano tuliyofikia suala hili litarekebishika na kufanyika vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani ajiandae.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana sana kwa kunipa heshima hii kubwa ya ku-second huu Muswada ambao umeletwa na Serikali. Kwa kweli kwa kifupi sana nitumie fursa hii kumpongeza sana Waziri na Naibu.

Mheshimiwa Spika, mimi ulinipa nafasi na heshima ya kuhudumia Kamati hii ya Katiba na Sheria. Nimeshiriki katika kuujadili Muswada huu. Kwa kweli nitumie nafasi hii kumpongeza sana kaka yangu Simbachawene na Ummy kwa usikivu wao mkubwa kwa maoni ambayo sisi Wanakamati tuliwapa kwa lengo la kuboresha Muswada huu na kufanya *harmony* katika *implementation* ya Muswada huu mzima. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri. (Makofi)



Mheshimiwa Spika, mimi niseme kitu kimoja. Ibara alizozitaja kaka yangu Olelekaita, Ibara hizi zimekwenda mbali zaidi. Ibara ya 13 ya Muswada huu imewataja Wabunge wa Viti Maalum wote nchini, kwamba wamepewa fursa ya kushiriki katika zile *Oversite Committee* tunazozitaja katika mikoa yao. Jambo hili limeonesha namna gani Muswada huu umeamua kuwa *inclusive* katika kuwafanya Wabunge katika kushiriki katika *level* za mikoa. Kwa maana Wabunge wa Viti Maalum ukija kwenye majimbo wanaweza wasionekane, lakini Muswada umeweza ku-*reflect*. Kwa hiyo, hili Mheshimiwa Simbachawene nafikiri darasa langu la kuwashirikisha kinamama katika uongozi na maamuzi ulilielewa vizuri. Ninakupongeza sana Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo nataka niipongeze sana Serikali; tulipata fedheha sana tulipopata maafa mwaka 2017 pale Bukoba. Tuliona namna gani Serikali ilivyokuwa ikihangaika kuwaita wadau ku-*mobilize fund* kwa ajili ya kwenda kutatua na kurudisha hali iliyokuwa imetokana na madhara ya *earthquake* ambayo ilikuwa imewapata watu wetu wa kule Bukoba. Kitendo cha Serikali kuja na Muswada unaoipa Ibara ya 34 Mamlaka ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzisha *fund* maalum ambayo itakuwa inatibu matatizo na majanga yakitokea katika nchi hii imeipa Serikali heshima na kuepuka Serikali kukimbia majukumu yake ya Kisheria na Kikatiba katika kupambana na majanga katika Taifa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Simbachawene tunakupongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na *fund* hii itakayoanzishwa itawekewa utaratibu wa namna itakavyotumika.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa namsikiliza sana kaka yangu Kuchauka. Kama angekuwa amepata nafasi, huenda ameusoma Muswada labda kwa sababu pia alishapata matatizo, lakini akipata nafasi kuusoma Muswada hivyo vitu vyote alivyokuwa anauliza kwamba nani ata-*determine* janga hili ni la *level* gani na lichukuliwe na nani; Muswada huu umejitosheleza kueleza kila kitu, Mheshimiwa Waziri tunakupongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo machache ninaomba, na ninawashawishi Waheshimiwa Wabunge, kwamba tuunge mkono Muswada huu kwa sababu umekuja wakati muafaka ili sasa tuweze kuipa Serikali *forum* ya kukabiliana na majanga katika Taifa letu kwa namna ya ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana ninaomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

**13 SEPTEMBER, 2022**

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba atafuatiwa na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma ajiandae.

**MHE. SALOME WYCLIFFE MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 1 ya Mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kwa kunukuu kauli ya aliyekuwa Rais wa 16 wa Marekeni, Abraham Lincoln. Alipopewa nafasi ya kutafsiri nini maana ya demokrasia akasema demokrasia ni kutekengeneza Serikali ya watu inayotokana na watu wenyewe kwa ajili ya kuwahudumia watu hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemnukuu Abraham Lincoln kwa sababu Serikali ya Chama cha Mapinduzi iko madarakani tunaamini kazi yake kubwa ya kwanza ni kuwahudumia watu; na katika Maisha yote mtu huhitaji huduma pale anapokuwa amepatwa na shida. Kwa hiyo, Sheria hii inayohusiana na maafa ni sheria ambayo itaonesha dhamira ya dhati ya namna gani mnaweza kuwahudumia watu wanapokuwa wamepatwa na shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utangulizi wangu huo unakwenda sawasawa na mabadiliko ambayo yameletwa kwenye sheria hii, Ibara ya 6, Ibara Ndogo ya 1(c) ambayo ilikuwa inaelekeza kwamba Serikali au Waziri ana uwezo wa kuchukua mali ya mtu yeyote pale ambapo ataona inafaa kwa ajili ya kwenda kuhudumia maafa.

Mheshimiwa Spika, wananchi ni mabosi zetu; na mimi naishukuru sana Kamati ya Katiba na Sheria kwa kuomba kifungu hiki kifutwe na nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kuridhia kukifuta. Kuchukua mali ya mtu yeyote eti kwa sababu tena kwa namna Serikali au Waziri anavyoona inafaa huko ni kinyume na Katiba, ni uporaji wa mali za watu, ni jambo ambalo kiukweli lingetuweka pabaya sisi wawakilishi wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye Sehemu ya Nne ya Marekebisho ya Muswada huu, ambayo kiukweli wameweka kipengele kinachohusiana na makusanyo ya pesa au fedha ambazo zitatumika kwa ajili ya kushughulikia watu ambao wamepatwa na maafa. Natamani sana, na ni kwa sababu ya muda, natamani sana tungekuwa na kifungu kidogo ambacho kinaruhusu fedha hizo zitakazokusanywa zitumike *specific* kwa kazi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi natoka Kahama. Miaka kama mitano saba iliyopita watu wangu wa eneo la Mwakata walipatwa na madhira makubwa sana ya kupata mvua ya mawe. Nyumba zao nyingi zilibomoka, watu walifariki

na mifugo pia ilikufa. Fedha zilitolewa, wadau wakachangia, lakini mpaka leo kuna watu wanaishi ndani ya maturubai; zilipokwenda fedha zile hakuna anayefahamu. Vivyo hivyo, limewahi kutokea janga Nyangalata eneo la Kakola kule nyuma; watu walikaa chini ya ardhi kwa kufukiwa kwenye maeneo ya machimbo ya dhahabu kwa siku zaidi ya 40; na mimi nilikwenda kuwaona mwaka 2015. Fedha zilichangwa kwaajili ya watu wale akini *re-allocation* ya bajeti inafanyika pakubwa sana kwenye fedha za maafa. Wote tunakumbuka tulikuwa Bungeni tuliokuwepo kisa cha Kagera, wananchi walichangia tena kwa huruma kwa ajili ya kuwasaidia watu waliopata maafa, waliokufa na waliopoteza mali, mifugo na ndugu zao. Lakini fedha zile tuliambiwa zitatumia kwaajili ya kujenga shule, sijui barabara, sijui nini; na sasa watu wale mpaka leo wako kwenye simanzi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ikimpendeza Mheshimiwa Waziri, fedha zitakazokusanywa kwa ajili ya maafa zifanye kazi ya kuwahudumia wananchi wanaopatwa na maafa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala hili hatujachelewa; liwekwe kwenye Kanuni, kwamba fedha ikikusanywa kwenye ngazi za kijiji, wilaya na mkoa zitumike kwa ajili ya wakati wa matatizo. Hapo tutakuwa tumekubaliana, kwamba Serikali ipo imewekwa na watu kwa ajili ya maslahi ya watu wale.

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu kwamba tunapofikwa na maafa ni jambo la dharura; na tuseme tu katika hali ya kawaida Serikali inawahudumia wananchi karibu kila siku. Lakini kwa vile tumeona suala la maafa ni la dharura tumetengeneza timu maalum. Lakini hivi kweli kamati ya kitaifa, sijui kamati ya wilaya, mara ya wataalam; jukwaa la wadau, watu zaidi ya 113 wanatakiwa wakutane ili waweze kupanga jambo la dharura. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, umuhimu wake ni nini? Kama Serikali ipo, tutengeneze Kamati ya Dharura ambayo inaweza ikakutana kwa dharura na kufanya maamuzi ya dharura kwa ajili ya maslahi ya dharura. Hii ya kusema sijui na nani ameingia, hii siyo fursa. Hatuendi kutengeneza taasisi ili watu waweze kunufaika; huyu amekuwa Mwenyekiti, Mkurugenzi wa Maafa, huyu sijui ni Makamu Mwenyekiti, hapana. Tutengeneze *task force* ambayo inaweza ikakutana kwa dharura, ikafanya maamuzi kwa dharura na watu waweze kupata huduma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwenye Muswada huu Ibara ya 8 mpaka ya 11 naona ni ibara ambazo zinataka kutengeneza ukiritimba (*bureaucracy*) ambao hauna maana yoyote wala umuhimu wowote na mwisho wa siku unaweza ukashangaa Kamati ya Wataalam inakwama kwa sababu huku Kamati ya Mawaziri haijaka. Mara jukwaa la wadau linakwama kwa sababu kuna Chama fulani sijui hakijaingia, hakijasikiliza au hakijafanya nini. Naomba suala hili

lisichukuliwe kama fursa, lichukuliwe kama lilivyo kwenye sheria. Ni suala la maafa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwenye Ibara ya 39, eti inasema: “Waziri atatengeneza Kanuni kuhusu suala lolote ambalo ni lazima kwa madhumuni ya utekelezaji wa sheria hii. Uzuri, Wanasheria wako wengi humu ndani. Hatuwezi kutengeneza sheria ya jumla namna hii. Yaani Waziri atengeneze Kanuni kuhusu suala lolote ambalo anaona yeye linafaa! Ni lipi hilo ambalo sisi Wabunge 400 na kitu humu ndani hatuwezi kuliona? Kama kunatokea ulazima wa kuleta suala hilo, liletwe Bungeni. Wanaotunga Sheria ni Wabunge, sio Waziri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hatuwezi kutengeneza kifungu cha jumla na ndiyo maana kule kwenye Kanuni imewekwa pale Ibara ndogo inasema: “Waziri atatengeneza Kanuni ili kuweza kutekeleza kifungu cha juu. Sasa hiki kifungu kimesimama chenyewe, kinampa mwanya Waziri. Sisemi Mawaziri wetu ni wabaya, lakini anaweza kukaa hapo kwenye kiti mtu ambaye hana nia nzuri akatengeneza sheria yoyote ambayo itasaidia lolote kuhusiana na maafa. Hiyo sheria ni ipi ambayo ipo *general* kiasi hicho? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ikikupendeza, naamini busara yako, ya Kiti, kifungu hiki kimekuwa *too generous* na kinakwenda kinyume hata na Kanuni na taratibu za utungaji wa sheria. Kwa maana hiyo, kifungu hiki kinaweza kikafutwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 38 ya Muswada inasema hivi: “Mtu yeyote ambaye kwa mujibu wa sheria hii au kanuni ameruhusiwa kushiriki katika utekelezaji wa masharti ya sheria hii, hatashitakiwa binafsi kwa jambo lolote alilolitenda au kuacha kutenda kwa nia njema wakati akitekeleza shughuli hiyo ya usimamizi wa maafa.” Hivi tunapimaje nia njema ya mtu? Ni mara ngapi tumeona viongozi wa Serikali tena Waandamizi wanafanya maamuzi ya kizembe yanayopelekea ulemavu kwa Watanzania, yanayopelekea upotevu wa mali kwa Watanzania, yanayopelekea dhuluma na ukatili kwa Watanzania? Ni mara ngapi? Leo tunakwenda kutengeneza kifungu kingine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, huu umekuwa ni utaratibu. Nadhani viongozi wa Serikali wameshagundua kwamba kuna wakati wanafanya mambo kwa uzembe, na kwa sababu *principle* ya kukiri makosa na kujiuzulu hawataki kwenda nayo, wanatengeneza vifungu vya sheria ambavyo vinawalinda kwa maamuzi ambayo ni ya uzembe wanayoweza kufanya. Hili suala halikubaliki. Kama kosa limefanyika, kama maafa yametokea, itatengenezwa timu maalum ya kufanya *evaluation* ya namna Serikali, Waziri na Mkuu wa Mkoa alivyotekeleza majukumu yake katika kushughulikia suala hilo. Ikionekana kuna uzembe wowote ambao umefanyika, kila mtu atabeba mzigo wake. Kila mtu abebe mzigo wake. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani mtu anafukiwa kwenye shimo siku 40 lakini Serikali ipo. Halafu leo unasema eti hatashitakiwa kwa sababu alikuwa anashughulikia maafa. Ashitakiwe, awajibishwe na ikibidi yule aliyehusika na hayo maafa alipwe fidia. Kwa hiyo, sikubaliani kabisa na hii *trend* ya Serikali ya kuleta vifungu vya kuweka kinga dhidi ya uwajibikaji au uzembe unaoweza kujitokeza kutokana na wao kushindwa kutekeleza majukumu yao. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi niseme, sheria inaweza ikawepo na tukatunga nzuri, lakini lazima tukubaliane, Sheria Sura 242 inayofutwa ilielekeza kwamba lazima kuwe na fungu kwa ajili ya maafa. Ilielekeza *clear*, lakini fedha zilikuwa hazipelekwi. Kwa hiyo, ni kuhusu utashi wa kisiasa wa kuona kwamba wananchi ni mabosi wetu, ni lazima tuwasaidie, nasi kama viongozi lazima tuwe na moyo wa kibinadamu. Tunaweza tukaweka sheria nzuri, bajeti itengwe, ikatengwa na isipelekwe. Tukaweka sheria nzuri, fedha ziwe *ringfenced*, wakatokea viongozi ambao wanajiona kwamba wao wako juu ya sheria, wakatumia vibaya fedha hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, laiti kama, na ninajua wengi humu tumewahi kulalamika hata tunaleta hoja za dharura; ukiona watu wanavyoteseka wanapopatwa na majanga, sisi Wabunge tunaweza kuwa *tuna-privilege*, lakini fedha zinazotengwa ziende kwenye mfuko. Tusizichungulie zile fedha kutaka kuzidokoa dokoa hatuwezi kujua ni jambo gani linaweza likatupata muda gani ili tuweze kulishughulikia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru. Naomba kuwasilisha. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salome Kifungu kinachotoa mamlaka ya jumla kwa Mheshimiwa Waziri kutunga Kanuni, umeshaleta marekebisha hapa mbele au Hapana!

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, Hapana, sijaleta.

**SPIKA:** Sawa. Ahsante sana. Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, ajiandae.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nami nafasi ya kuchangia katika Muswada huu wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 1 wa mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kuipongeza Wizara, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwanza kabisa kwa kutuletea Muswada huu

kwa lugha ya Kiswahili ikiwa ni namna mojawapo ya kutekeleza matakwa ya Sheria iliyotungwa na Bunge hili Tukufu. Pia niweze kusema kwamba maafa ni jambo linalotokea kwa dharura, tunakuwa hatuja-foresee mambo haya na Muswada huu kama walivyotangulia Wabunge wenzangu umekuja kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kwa sababu ya *issue* muhimu sana ya mabadiliko ya tabianchi na maafa nayo yamekuwa mengi. Kwa hiyo, sheria hii kwa utungaji wake na tukienda kutekeleza vizuri hasa ukizingatia sheria hii imekuja kuangalia, namna ya kuwasaidia wananchi moja kwa moja kuanzia ngazi ya chini, naamini tunaweza kupunguza majanga makubwa sana yanayowapata wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa *kuli-convince* Bunge hili Tukufu kuipitisha sheria hii kwa hoja zifuatazo: Kwanza, ni juu ya *issue* ya urasimu wa kamati zilizoundwa katika sheria hii. Katika sheria iliyofutwa kamati hizi zilikuwepo baadhi na baadhi sasa zimeundwa, lakini bado urasimu ulikuwa mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Serikali imepokea maoni ya Kamati, imepunguza urasimu kwa maana ya wingi wa Wajumbe na utaratibu unaotumika kuunda Kamati hizi. Pia, kwa namna ya pekee namwomba Mheshimiwa Waziri kwa kutumia Ibara ya 39 ambayo inampa nguvu ya kwenda kutengeneza Kanuni, basi aangalie namna ambayo Kamati moja haitazuia Kamati nyingine kutekeleza majukumu yake pale ambapo maafa yanatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hilo tutakuwa tumesaidia sana kupunguza *bureaucracy* kwa sababu tusipoweka kifungu hiki italazimisha kama hizi kamati fulani haijaka, nyingine haiwezi kukaa. Hii italeti madhara makubwa ukizingatia majanga yanaongelea *right to life* (haki ya kuishi) ambayo ndiyo haki ya msingi zaidi ya mwanadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili naomba niongelee suala la kuheshimu haki za binadamu za Mtanzania hasa Ibara ya 24(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mapendekezo ya kwanza kabisa ya sheria iliyokuwa imeletwa na Serikali katika Kamati ya Bunge hili Tukufu ilikuwa inampa nguvu Waziri, Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kutumia mali za mwananchi wa kawaida (*private/individual*) mali yoyote ile wakati wa majanga bila kuwa imeongelea suala zima la fidia. Nashukuru sana Serikali imepokea maoni yetu na imeondoa mali za watu binafsi na sasa Serikali itatumia mali za Umma pekee katika majanga ili kuokoa wananchi kwa wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, naipongeza sana Serikali kwa sababu katika sheria hii imeweka *inclusion* ya Wizara zote ukizingatia kwamba suala la

majanga hatuchagui *whether* litatokea kwenye maji, litaathiri chakula, litahusu moto, litaathiri miundombinu; kwa hiyo, imeweka Wlzara zote ili kuhakikisha kwamba majanga yanapotokea kila Wizara kwa namna yake na kwa nafasi yake inahusika kutoa nafuu kwa wananchi kwa namna inavyowezekana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nigusie tu pia suala la mfuko. Mchangiaji aliyepita amezungumza kwamba katika sheria iliyopita kulikuwa kuna ulazima wa Bunge hili kutenga fedha kwa ajili ya mfuko huu wa maafa. Naweza kusema kwamba *section 29* ya sheria inayopendekeza kufutwa ilikuwa ndiyo imeongelea mfuko huu, lakini *sources of funds* za mfuko huu ilikuwa *based on pure donations*. Maana yake ni kwamba ilikuwa ni pale ambapo watu watachanga kwa upendeleo wao, ndiyo watu waweze kuhudumiwa kwa fedha zile katika mambo ya maafa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa sababu katika sheria hii mpya iliyoletwa imeweka ulazima katika kila mwaka wa bajeti Serikali kupitia Bunge hili Tukufu kutenga fedha kwenda katika mfuko huu na fedha hizi zitumike siyo tu katika kukinga maafa, lakini kupunguza madhara ya majanga na maafa pale yanapojitokeza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, namwomba sasa Mheshimiwa Waziri katika Kanuni zetu ambazo amepewa nguvu ya kutunga chini ya Ibara ya 39 ya Sheria hii, azingatie pia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, cha kwanza, nashauri sana katika Kanuni hizi ahusishe suala zima la *relief in loan repayment schemes*, kwa maana ya unafuu wa malipo ya mikopo ya wananchi wetu. Serikali yetu katika utungaji wa sheria hii imechukua *study* kutoka katika nchi kama ya India na *South Africa*; na wenzetu wameenda mbali sana, wame-*provide* kwenye sheria zao kwamba yanapotokea majanga inatambua kwamba wananchi ndio waathirika wakubwa na wananchi wengi wanatumia fedha kutoka katika taasisi mbalimbali ambazo wanazipata kwa njia ya mikopo kuwekeza katika maisha yao ya kawaida na hivyo majanga yanapojitokeza kunakuwa na *disturbance* kwenye namna yao kwanza ya kujipatia kipato na hivyo katika kurejesha mikopo hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali iangalie namna ya kuonesha katika kanuni ni namna gani wananchi hao wataangaliwa ikiwa ni pamoja na Serikali sasa kuona inawekaje kwa vile yenyewe kupitia Benki Kuu ndio wasimamizi wa taasisi za fedha, inaelekeza kwamba watu hao wapewe nafuu fulani fulani aidha ya muda au msamaha fulani ili tuweze kuwasaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, cha pili, nilikuwa nashauri kuwe na maboresho katika Shirika letu la Bima ya Taifa. Tumesema kwamba Bunge hili litatoa fedha au litatunga sheria au katika kupitisha bajeti litatoa fedha kwa ajili ya mfuko huu. Nachelea kusema kwamba, mfuko huu ni kwa ajili ya muda ule ambao majanga yanatokea, lakini baada ya majanga wale wanaachwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naweza kusema kwamba ni muhimu sasa Serikali kupitia Wizara zinazohusika kuangalia namna ya kuboresha Shirika letu la Bima ili kwanza, tuwape elimu wananchi kwa umuhimu wa kukata bima katika mali zao; pili, tuangalie namna, ikiwezekana kutoa ruzuku kwenye Shirika hili ili Bima za mali za wananchi hasa wa kipato cha chini ziweze kukatwa kwa bei ndogo. Hii itaipunguzia sana Serikali mzigo mkubwa pale ambapo majanga yanatokea kwa namna ya kuwahudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba Bunge hili Tukufu kupitisha Sheria hii kwa sababu inakwenda kutusaidia sana wakati wa majanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, atafuatiwa na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu na Mheshimiwa Ummy Nderiananga ajiandae.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nikiwa kama Mwanakamati kuweza kutoa mchango wangu katika Muswada wa Sheria hii ya Kukabiliana na Kudhibiti Maafa kama ilivyoletwa.

Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pongezi kwa Serikali kwa kuleta Muswada huu wakati muafaka kwa sababu tumeona matokeo huko nyuma yalivyokuwa yanatupata kukitokea maafa, watu wanavyohangaika na Serikali inavyohangaika, inakuwa mpata mpatae, kakamate kule, kashike kule. Sasa hivi unapokuja na sheria hii ambayo inashirikisha ngazi zote kuanzia chini mpaka hapa ilipofika, ni kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kusema kweli Serikali ilijiandaa vyema na kutuletea wadau, nao wenyewe kutuletea mabingwa waliobobea katika sheria hii, na Kamati yetu ilishirikiana na kushauriana kwa dhati kabisa. Kwa kweli huko hukuwepo lakini moto uliwaka wakati wa kujadili sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri kwa kuwa watu wote ni waelewa; wadau ni waelewa, wanasheria ni waelewa na sisi ni waelewa, tumeweza leo kusimama mbele yenu kuomba Bunge letu hili liweze kupitisha Muswada huu



uwe sheria kamili kuweza kutusaidia katika hayo. Kwa sababu ni jambo la hakika kwamba unapotaka kupigwa ukiwa unajua ngumi itakupiga kwa wapi itakuwa haikuumi sana. Kwa hiyo, tunapojiandaa kwa lolote ni jambo ambalo litaisaidia Serikali yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sheria hii kwa kweli inatekeleza mambo ya Jamhuri ya Muungano, lakini kwa vile maafa yanaweza kugusa pande zote za Jamhuri, tumeona umuhimu wa ushirikiano wa pande hizi mbili yanapotokea matatizo makubwa, kwa sababu huenda yakatokea hata maradhi au dhoruba huko baharini yakakumba Zanzibar. Kwa hiyo, ule ushirikiano utakaokuwepo wakati wa dharura ni jambo zuri sana. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iendelee na jambo hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo tumejadili na tumeliona lina umuhimu wake, kwa sababu bila fedha hakuna utakaloliweza. Kuanzishwa huu mfuko maalum wa maafa, tunashawishi upate udhibiti mzuri, utekelezaji wake na uendeshaji wake uwe na uwazi zaidi ili tuweze kufikia yale ambayo tumedhamiria. Kwa sababu, bila kuwa na fedha hakuna kitu utakachoweza kukifanya na tunajua inapotokea maafa, basi fedha nyingi kweli huhitajika. Kwa hiyo, vile Serikali ilivyoona kwamba iweke kama ni sheria kwamba Serikali itie fedha kiasi fulani katika mfuko huu, ni jambo ambalo tunasema lilikuwa la maana sana.

Mheshimiwa Spika, sasa suala la majanga kama tunavyosema linaweza likatokea na maafa. Kitu cha muhimu ni kuhakikisha kwamba hii elimu inatolewa hasa shuleni, kwa wananchi kwa ujumla, kila mtu afahamu inapotokea dhoruba niiname chini. Kama vile tunavyoambiwa, ukisikia risasi zinalialia, basi wewe inama chini ili isije ikachukua sikio lako. Kwa hiyo, watu watakuwa wanajua mapema namna gani wafanye. Kwa hiyo, tunashauri Serikali iendelee kutoa elimu hii kwa ngazi zote tena kwa namna ya hali ya juu, kwa sababu kama alivyosema mwenzetu mmoja hapa Mheshimiwa Abdallah kwamba *early warning* inatusaidia sana; yaani tahadhari ya mapema ni jambo la muhimu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali pia iimarisha kitengo hiki cha kuweza kuhabarisha wananchi; *tuna-expect* hiki kwa hiyo, ni lazima tujiandae kwa namna hii ili kupunguza yale madhila au madhara yatakayotokea, kwa sababu, ukijua namna gani ukimbie, yale maafa yatakuwa yamepunguza ukali wake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kuliongelea hapa ni hili ambalo tulishauriana kwenye Kamati la kwamba siyo Waziri aamue tu kukamata mali za watu halafu afanye vile anavyofanya, ni kwamba ikitokea shida kutaka kutumia zitumike mali za Serikali, lakini kama itatokea mtu

mwenyewe atataka kujitolea, kwa sababu wakati wa maafa kuna watu wana moyo wa imani wanapenda kujitolea. Tumefurahishwa sana na Serikali kukitengeneza kifungu hiki cha Ibara ya 6(C) ambacho kilikuwa kinakwenda kinyume na Katiba yetu ya kutaka kuchukua mali za watu kwa lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunashukuru kwamba Serikali imekubali kupunguza ule msururu mkubwa wa Kamati zile za Maafa. Kwa hiyo, yale yote ambayo tumeshirikiana tukashauriana na kuweka utaratibu maalum ambao utakuwa rahisi katika utekelezaji, kwa sababu ukiweka kundi kubwa mara nyingine kama walivyosema wenzangu, wengine; huyu atakuwa hapatikani, huyu hapatikani, kwa hiyo jambo linapotaka dharura, kwa hiyo, mmoja Mwanakamati hakupatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa nampongeza sana Waziri Simbachawene na Mheshimiwa Ummu, kwa kweli wamekuwa maridhawa sana mpaka wakatuletea CBD ndani, kila mtu kaletwa pale ili pande zote zipate kushirikishwa. Kwa hiyo, hawa ndugu zetu wamefanya kazi kubwa sana nasi tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lililopo tuiunge mkono Serikali sheria hii ipite ikatusaidie wakati tunajiandaa vizuri ili yakitokea maafa, tuwe na namna ya kukabiliana nayo na kupunguza machungu kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, yangu yalikuwa ni hayo tu. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ummu Nderiananga na Mtoa hoja ajiandae.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Muswada huu wa Maafa. Katika Kamati yetu ya Katiba na Sheria tumejadiliana masuala mbalimbali kwa kutazama sheria hii ambayo ni muhimu na nyeti kwa wananchi wetu kwa maana ya Taifa letu katika kuzuia maafa. Mambo ambayo yaliibuka zaidi ambayo tulikuwa kwenye mjadala mrefu na mpana zaidi ilikuwa ni suala la jina la Muswada.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipoleta Muswada huu tulikuwa tumejadiliana kwa kina sana kwamba kwa nini Muswada huu uitwe Sheria ya Usimamizi wa Maafa? Tukawa tunajaribu kujadiliana kwamba kwa nini sheria hii isiitwe Sheria ya Kuzuia Majanga na Kukabiliana na Maafa?

Mheshimiwa Spika, baadaye tulikaa vizuri sana na Serikali na kueleweshana vizuri na tukaona kwamba kutokana na uandishi wa sheria, jina sahihi na muhimu kuwa ni iwe ni Sheria ya Usimamizi wa Maafa. Mambo haya yote kwenye Kamati yetu tulikuwa tumeona kwamba msingi wa sheria hii ni

kuhakikisha kwamba ni kuzuia, kujiandaa, kukabiliana na kurejesha hali pale ambapo panatokea maafa.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine haya yote ambayo tumejadiliana kwenye Kamati yetu ni kuhusu pia ukubwa wa Kamati kama Waheshimiwa Wabunge wanavyozungumza hapa. Tuliona hili na tukazungumza kwa kirefu sana na tunashukuru Serikali kwa sababu wamekuja na wakaeleza vizuri na wamerekebisha ukubwa wa kamati, hivyo imekuwa ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, pia tulipokuwa tumejadiliana kuhusu ukubwa wa kamati, haimaanishi kwamba maafa yakitokea sasa ndio lazima hizi kamati zikae ili hilo jambo likashughulikiwe, hapana. Serikali ilitoa maelezo mazuri sana kwamba maafa yanapotokea kunakuwepo na timu ya haraka sana kushughulikia masuala ya maafa. Kwa hiyo niwaondoe Waheshimiwa Wabunge wasiwasi kwamba haimaanishi kwamba kamati zote zikae, halafu ndio maafa yakashughulikiwe wakati watu labda wanakufa, nyumba zinaungua, lazima mambo mengi yatakuwa yanachukuliwa kuhakikisha kwamba jambo lenyewe linakabiliwa ili wananchi waendeleo kuwa salama na mali zao.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua kuna majanga ambayo ni ya asili na majanga ambayo yanasababishwa na binadamu. Majanga kama ya *volcano* na ukame ni mambo ambayo yanakuja *automatically* sisi hatuyaelewi, lakini kuna mambo mengine ambayo yanaweza kusababishwa na binadamu. Kwa hiyo tukasema kwamba kwa mfano, Serikali ihakikishe kwamba inapokabiliana na maafa au kujiandaa kama ambavyo nimekwishatangulia kusema, Serikali imeweka mipango na mifumo kwenye sheria hii kuhakikisha kwamba maafa yanapotokea kunakuwepo na mkakati mahususi wa kushughulikia maafa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, katika Kamati yetu pia tulijadiliana masuala ambayo wenzangu walishasema kwamba uchukuaji wa mali. Serikali ilikuja na kifungu hiki lakini tunashukuru tena Serikali kwa mara nyingine kwa sababu baada ya mjadala mrefu kwenye Kamati yetu tulisema hili linakwenda kinyume na Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 24(1) kwamba uchukuaji wa mali za wananchi kwa maana Waziri awe na uwezo wa kuchukua mali...

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nimemsikiliza mzungumzaji kaka yangu pale akifafanua kuhusu majukumu ya Kamati za Maafa. Napenda kumpa taarifa kwamba ibara ya 20 ya Muswada inaeleza

majukumu nikiacha zile kamati zingine nakutolea tu mfano wa kamati moja, majukumu ya kamati za maafa itakuwa ni kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa maafa na huduma za dharura katika eneo husika kama itakavyoelekezwa na Kamati ya Utekelezaji ya Wilaya ya Usimamizi wa Maafa. Kwa hiyo namna taarifa kwamba kuna *bureaucracy*, hakuna kamati ya dharura nyingine itakayotengenezwa kamati ndizo hizi na zitakazoshughulika na suala la maafa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis unapokea taarifa hiyo.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri nimeshirikia sana kwenye mjadala huu na ulikuwa ni mjadala mkali sana, lakini nataka niseeme taarifa yake siipokei kwa jinsi alivyoelewa.

Mheshimiwa Spika, iko hivi, kwanza tukumbuke sio mara ya kwanza Tanzania kushughulikia maafa kwa sababu kwa mfano tu juzi Nzige walipovamia Tanzania hakuna kamati yoyote iliyokaa, ni Serikali yenyewe ilishughulikia, imetafuta ndege, imefanya mambo mbalimbali na baadaye wakaweza kudhibiti hawa nzige. Kwa hiyo nataka nimwondoe wasiwasi kwamba haimaanishi kuwepo kwa kamati hizi sasa ndio nyumba inaungua mpaka kamati ikae, hapana au mafuriko inachukua watu halafu ndio kamati zikae, hapana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuendelea kusema kwamba suala la uchukuaji wa mali za wananchi, Waziri au Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya tuliona ni kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo sisi kama kamati tuliweza kuishauri Serikali na kuishukuru Serikali kwa sababu imeondoa kifungu hicho na sasa hakuna mali ya mwananchi yeyote wa Tanzania itakayochukuliwa na Waziri, Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ina manufaa makubwa sana kwa wananchi wa Tanzania. Kwa mfano, wajibu wa Serikali kwa sheria ni kuhakikisha kwamba imeweka mifumo mizuri ya kukabiliana na maafa na kuzuia maafa mengine ambayo yanaweza kuzuiwa kama yale ya binadamu. Pia kuweka vitendea kazi kwenye maeneo mbalimbali ambayo inatakiwa kwa ajili ya kujiandaa kuzuia maafa. Sheria hii pia inakwenda kuipa Serikali mamlaka ya ujenzi wa kuhakikisha kwamba inajenga miundombinu kwenye maeneo mbalimbali. Kwa mfano, kwenye maeneo ambayo mafuriko yanaweza yakaingia au labda kuhakikisha kwamba majengo yote ya Serikali yana vizimia moto na kadhalika. Vile vile usimamizi wa ujenzi wa majengo imara ili maghorofa yasije yakaanguka, pia suala la kuhakikisha kwamba mifumo mizima kwenye nyumba zote ambazo kuna vitu vingi ambavyo vinaweza vikaleta vihatarishi, iko vizuri.

Mheshimiwa Spika, naliomba Bunge lako liweze kupitisha sheria hii kwa sababu ni kwa manufaa ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kama tunavyojua, tunapotunga sheria tunatunga kwa sababu ya kuhakikiisha kwamba ina manufaa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge kanuni yetu ya 34 inaniruhusu kuongeza muda na si lazima niwahoji. Mheshimiwa Ummu Nderiananga atafuatiwa na Mheshimiwa mtoa hoja, halafu tutaendelea na utaratibu mwingine. Mheshimiwa Ummu Nderiananga, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, karibu kwa mchango wako.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMU H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Niungane na Mheshimiwa Waziri na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliompongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia tutele Muswada huu wa Sheria katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niwashukuru na kuwapongeza sana Wajumbe wa Kamati yetu ya Katiba na Sheria wakiongozwa na Mwenyekiti Dkt. Mhagama kwa kazi nzuri na kubwa waliyofanya ya kutushauri sisi Serikali mpaka tukafika hapa tulipofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze kipekee Mheshimiwa Waziri wetu wa Nchi, Mheshimiwa George Simbachawene kwa uongozi mahiri alioonesha na kuweza kutusadia kufika katika hatua hii pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watushi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wametoa maoni yao na sisi kama Serikali tunawashukuru sana na tunawapongeza kwa michango mizuri yenye kuleta mwelekeo wa kuboresha shughuli tuliyoifanya. Hata hivyo, niseme katika baadhi ya maeneo tumeshauriwa kuendelea kutoa elimu ya usimamizi wa maafa. Tunalichukua jambo hili, tutaendelea kutoa elimu ya usimamizi wa maafa na niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuungane mkono tupitische sheria hii ili kazi iweze kuanza mara moja.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili tutaendelea kutumia vyombo vya habari na majukwaa mbalimbali kuendelea kutoa elimu hii, lakini ushauri wa kupeleka elimu katika shule, vyuo na maeneo mbalimbali tumezingatia.

Mheshimiwa Spika, tunatambua suala la maafa ni suala mtambuka kama lilivyoielezwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliozungumza hapa, linahitaji ushirikiano wa kila mmoja na nilipokuwa naandika maoni hapa nilikuwa nafurahi kwamba kwa pamoja sisi wawakilishi wa wananchi tumeonesha mweitikio, kila mtu amelichangia na hata tulipokuwa tunaendelea kuchangia Muswada huu tumeendelea kutoa elimu kwa umma. Watanzania waliotuona wamesikia na wamefahamu kuhusu suala la maafa.

Mheshimiwa Spika, ipo hoja hapa ya kuwa na mlolongo wa kamati, kamati hizi ni kubwa na kuna posho. Nataka niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, hakuna posho yoyote kamati hizi zitaketi kwa mujibu wa majukumu yao. Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya anapoenda kwenye kamati yupo kazini, Mkurugenzi yupo kazini, kwa hiyo hakuna namna ambayo kutakuwa kuna posho au fedha nyingi zitatumika kwa ajili ya kuketi tu vikao, fedha nyingi zitaenda kwa ajili ya kushughulikia kazi ya maafa.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo hapa kidogo kama linatatiza hivi kwenye suala hili la maafa. Katika kujenga uelewa wa pamoja tunaposema usimamizi wa maafa inajumuisha kujiandaa kukabiliana na maafa kabla hayajatokea, wakati maafa yametokea na kurejesha hali baada ya maafa kutokea. Kwa hiyo huu mzingo mzima wa usimamizi wa maafa, hapa ndio sheria hii inatupa namna nzuri zaidi ya kusimamia eneo hili la maafa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, tutaendelea kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi katika kukabiliana na maafa na nilipe taarifa Bunge lako Tukufu kipindi ambako bado hatujakutana hapa wenzetu wa Shirika la WFP wameendelea kutu-*support* Serikali na walitupatia vifaa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tunavyo vifaa ambavyo ni *drowns*, pakitokea maafa pengine Dodoma Mjini tuna uwezo wa kurusha *drown* dakika 45 imeshatambua kwamba maafa haya yamesambaa kwa kiasi gani. Kwa hiyo na sisi tunaenda kwenye usasa, hatukai tena kizamani. Tutaendelea kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi lakini na ukanda wetu wa SADC, Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa pamoja tushirikiane kwenye suala hili.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kwa unyenyekevu mkubwa niwaombe Waheshimiwa Wabunge watuunge mkono, tupitische Sheria hii ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niseme kwamba naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

**13 SEPTEMBER, 2022**

Waheshimiwa Wabunge sasa namwite Mheshimiwa George Boniphace Simbachawene, mtoa hoja, aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU):**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba nichukue nafasi hii kwanza kabisa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, najua wapo waliochangia kwa kusema, lakini wapo ambao hawakuweza kuchangia, lakini wameshirikia na sisi katika mjadala wa hoja iliyokuwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati. Kama ulivyoona hapa uelewa unasumbua juu ya Muswada huu basi hata huko kwenye Kamati tulikuwa na sisi tunapata shida lakini hatimaye baadaye tulianza kuelewana. Kama pia ulivyoona hapa namna michango ilivyokuwa inaendelea kila mtu anazidi kuwa mbunifu zaidi na hasa katika kujua tofauti ya maafa na majanga ni nini. Wapo wengine wanachanganya majanga na maafa wanajua ni kitu kimoja.

Mheshimiwa Spika, majanga ni yale ya asili au yale yanayotokana na sababu za binadamu, yanapotokea ndio yanasababisha maafa. Maafa ni matokeo ya majanga. Sasa huwezi kutunga sheria ya majanga, yaani wewe unaweza ukatunga sheria ya kuzuia *tropical cycle* hapana ila *effect* yake ndio unaweza ukatunga sheria ya kuweza *kui-manage*. Kwa hiyo duniani kote *standard* sheria ziko hivyo, wanazungumzia sheria *Disaster Management Act*, kwa hiyo na sisi tumefuata utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni sheria yetu hii inahusika na matukio haya kabla, katika *level* hiyo hiyo kama ya majanga, lakini kabla je, njia gani tunaweza tukapunguza majanga kutokuweza kutokea, yale ambayo kibinadamu tunaweza. Baadaye, wakati yanapotokea majanga na wakati majanga haya yamekwishasababisha sasa madhara ambayo sasa yanaitwa sasa maafa, lakini na namna tutakavyorudisha madhara au kupunguza madhara ya maafa, hapa ndiko tunaweka sheria. Sheria kama sheria haiwezi ika-*exhaust everything* na ndio maana tuweka nafasi ya Waziri kutunga kanuni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kazi hii nzuri iliyofanyika ya marekebisho makubwa, sheria hii imekuwa na marekebisho makubwa, lakini kwa kweli sifa zote wapewe Kamati yetu, Kamati ya Katiba na Sheria. Wamekuwa walimu wetu wazuri, wametusaidia sana katika ushauri na kwa kuwa sisi Serikali ndio tulikuwa wenye hoja hata hili jedwali la marekebisho tuliloleta kwa kweli ni kazi kubwa iliyofanywa na Kamati. Kwa hivyo nawashukuru Kamati kwa kushirikiana na wataalam wetu wa Wizara tumeweza kufika hatua hii leo hapa.

Mheshimiwa Spika, wachangiaji walio wengi wamepongeza na nimeanza kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa sababu wamekuwa walimu humu wakielezea uzuri na maeneo mazuri ambayo yamewekwa katika sheria hii. Niwatoe mashaka kwa maeneo machache ambayo yameonyesha kwamba pengine watu hawakuweza kuyaona.

Mheshimiwa Spika, nianze na wote waliochangia ambao ni kama 12, lakini sio rahisi sasa kwa muda niliopewa kuweza kurejea kila mmoja alichokisema labda yale ambayo yalitia wasiwasi sana kwa ajili ya uelewa wa Wabunge pia na Watanzania wanaotusikiliza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kuchauka alizungumzia jambo lililokuwa lina-reflect tukio lililomkuta yeye, tukio halisi na ni kweli, tumpe pole sana lakini kimsingi lile lilikuwa ni kosa, watu walifanya uhalifu, haliwezi kuwa janga. Watu walikuja wakafanya uhalifu, wakaharibu mali, kwa hiyo wanashughulikiwa kwa mujibu wa sheria. Linapokuwa janga ni mpaka liwe linachukua sura ya ukubwa wake na haliwezi kurejesheka kwa namna nyepesi, lakini gari utaenda utanunua unakuwa na gari, nyumba utaenda utajenga utakuwa na nyumba, lakini ulikuwa kwa jirani alikusaidia pengine au ulihamia nyumba yako nyingine ya pili. Kwa hiyo halijawa janga. Kwa hivyo nijibu na lile la kusema nani anapanga kiwango kwamba hili ni janga au siyo janga.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria na utaratibu wa zile kamati tulizoziweka linapowazidi *level* ya mtaa au Kijiji wanaenda *level* ya juu kidogo kutoa taarifa. Kwa hiyo zile kamati zinawasiliana *level* zote wilaya, mkoa mpaka Taifa kulingana na uzito na ukubwa au pengine teknolojia au vifaa vinavyoweza kutumika.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limeguswaguswa ni maelezo aliyotoa Mheshimiwa Salome Makamba. Alijaribu kurejea baadhi ya maeneo, lakini yale yote mashaka yake yako covered na huu Muswada kwenye sura ya tano, masharti ya jumla. Kwa mfano, alisema fedha zikipatikana zinaweza zisifanyiwe shughuli nyingine. Kifungu cha 36(2) kinasema:

*“Mtu ambaye atakusanya michango au misaada kwa ajili ya jamii iliyoathirika na maafa na kutoiwasilisha katika kamati...”*, yaani fedha yoyote itakayokusanywa kwa ajili ya maafa itakwenda kushughulika na suala hilo tu na sasa tumeliweka kuwa kosa na mtu huyu atachukuliwa hatua. Kwa hiyo tume-improve tumetoka kwenye ile *level* ambayo ulikuwa na mashaka nayo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni lile ambalo alizungumzia suala la kinga ya kutokushtakiwa, kinga hii imewekwa kotekote, liko eneo hapa tumesema, kifungu 37:



“Endapo kosa limetendwa chini ya sheria hii na taasisi au kampuni, mtu yeyote ambaye wakati kosa hilo linatendwa alihusika na usimamizi wa taasisi au kampuni hiyo atachukuliwa kuwa yeye ndiye aliyetenda kosa...”

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, atashtakiwa yeye kama yeye kwa sababu hiyo. Pia tukaenda tukasema kuna *nature* na aina ya matatizo, gari inaungua, mtu yuko ndani, umeamua kuchukua chuma kigumu ukavunja kioo, ukamtoa katika nia yako hiyo njema umesababisha tatizo la mtu yule pengine kuumia zaidi kinyume na matarajio. Nia ilikuwa njema lakini limetokea vinginevyo, ndio tukasema lazima tuwape kinga. Hii ni *standard law* kwa mwanasheria yoyote anajua, katika sheria yoyote na hasa wale wataalam wa sheria zile za *Law of Torts, provisions* kama hizi ni lazima zinakuwepo nia njema yaani lazima iwe nia njema. Kwa hiyo tumewapa kinga hao, kwa sababu ya hiyo nia njema. Inapimwa kwa kuangalia vitu vingi sana, sasa *is a science*, tukienda sasa huko tunafika mbali, lakini kimsingi sheria nyingi tunaziandika hivyo kwa madhumuni hayo.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ni lile ambalo limesemwa na Waheshimiwa Wabunge hapa, juu ya maeneo yale ambayo yatagusa watu kupata uelewa na uwajibikaji. Tumeweka masuala ya majanga isiwe watu wanasema tu, Ofisi ya Waziri Mkuu au mtu fulani, ili watu wote waweze kushiriki. Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na wale waliosema kwamba, elimu izidi kutolewa watu wajue na zile angalau *standard equipment* katika hizi Kamati katika Mikoa na katika maeneo yetu kuwa na vifaa vya msingi hata vya kuweza kusaidia.

Mheshimiwa Spika, unakuta Wilaya nzima haina hata maturubai. Yaani likitokea tatizo ni Wilaya nzima na ni chombo cha utawala kabisa kiko pale kuna Mkuu wa Wilaya, kuna nani, lakini hawana maturubai ambapo hata watu wakipata matatizo ya mvua tu mnaanza kutafuta *Red Cross!* sasa tunaonesha kwamba, hatuna utayari. Kwa hiyo, utayari huu ni jukumu la kila mmoja na tumesema kwenye sheria hii kwamba, sasa itakuwa ni lazima kwamba, lazima hizi mamlaka zetu hizi za utawala ambazo zimewekewa mfumo huu wa sheria hii basi ziwe na wajibu wa kuwa na mazingira haya ya maandalizi.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimesema awali, siyo rahisi kuyajibu yote, lakini yale ambayo pengine yatahitajika ufafanuzi tunaweza tukafanya hivyo kwa maandishi, lakini kimsingi nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri ambayo imelenga kujenga. Kipekee nirudie tena kuwashukuru sana Kamati yetu chini ya viongozi wetu mahiri Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama pamoja na Mheshimiwa Najma Giga, wametusiambia vizuri na tumetoka na sheria nzuri. Mimi naamini changamoto yetu itakuwa ni utekelezaji tu. (Makofi)

**13 SEPTEMBER, 2022**

Mheshimiwa Spika, tutajitahidi sana Serikali katika kutunga kanuni, tutunge kanuni ambazo zitakuwa zinasaidia katika utekelezaji chanya wa sheria hizi. Wengi wamesisitiza kwamba, kwenye kanuni kwa kweli, tujaribu kutengeneza kanuni zitakazosaidia kupunguza changamoto za watu wetu ambazo ni ndogondogo katika misingi midogomidogo, lakini ndizo zinazowagusa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya ninaomba kutoa hoja.  
(Makofi)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Asanteni sana, tutaendelea na utaratibu wetu. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza Kifungu cha 1, Ukurasa wa 4.

Kifungu cha 1

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 3

Kifungu cha 4

Kifungu cha 5

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6  
Kifungu cha 7

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 8

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 9

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 10  
Kifungu cha 11  
Kifungu cha 12  
Kifungu cha 13  
Kifungu cha 14

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 15

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 16  
Kifungu cha 17  
Kifungu cha 18

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 19

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**13 SEPTEMBER, 2022**

Kifungu cha 20

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 21

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 22

Kifungu cha 23

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 24

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 25

Kifungu cha 26

Kifungu cha 27

Kifungu cha 28

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 29

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 30

Kifungu cha 31

*(Vifungu vilizotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 32

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**13 SEPTEMBER, 2022**

Kifungu cha 33  
Kifungu cha 34  
Kifungu cha 35

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 36

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 37  
Kifungu cha 38  
Kifungu Kipya cha 39  
Kifungu cha 40  
Kifungu cha 41

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge Linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja, taarifa.

## **T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria, Ibara kwa Ibara, Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2022, Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022, Ibara kwa Ibara na imekubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji.

**13 SEPTEMBER, 2022**

Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022 (*The Disaster Management Bill, 2022*) waseme ndiyo.

**WABUNGE:** Ndiyo.

**SPIKA:** Wasiofiki waseme siyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Watu wote wameafiki Muswada huu. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Muswada wa Sheria kwa lengo la kutunga sheria ili kuweka Mfumo wa Usimamizi na Uratibu wa Maafa kwa ajili ya hatua za kuzuwa na kupunguza madhara ya majanga, kujiandaa kukabiliana na kurejesha hali pindi maafa yanapotokea, kuanzisha na kusimamia Mfuko wa Usimamizi wa Maafa pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa mara ya tatu, na kwa muktadha huo sisi kama Bunge tumemaliza kwa hatua zote za kutengeneza sheria.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Katiba yetu, baada ya kupitisha Muswada huu wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa, sasa tutampeleka Mheshimiwa Rais ili nae afanye kwa sehemu yake, atakaposaini kwa mujibu wa Katiba basi itakuwa sheria na Waheshimiwa Wabunge mtapewa taarifa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nitangaze kwamba, Bunge tumepitisha rasmi Muswada huu wa Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kuipongeza sana Kamati yetu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuliwezesha Bunge letu kuweza kutunga sheria hii muhimu kabisa kwetu kama Taifa na namna ya kutuelekeza namna ambavyo tunaweza kushughulika na majanga ili tusipate maafa, pia pale ambapo yatatokea maafa basi namna ambavyo sisi kama Taifa tutakuwa tumejipanga vizuri. Hivyo, nimtakie kila la heri Mheshimiwa Waziri katika utekelezaji wa sheria hii Rais atakapomaliza kwa sehemu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri ninawapongeza na kuwashukuru pia kwa namna ambavyo mmekuwa wasikivu kwa kujua kwamba, kazi ya Bunge ni kutunga sheria ninyi mmeleta Muswada na sisi tumefanya kwa sehemu yetu, msingekuwa wasikivu ungekuwa mtihani. Kwa hiyo, tunawashukuru sana pia kwa ushirikiano wenu mlioutoa kwa Kamati hii kuweza kufikia hapa ambapo tumefikia leo. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunapoyasema haya maneno hapa mwishoni ni ya muhimu sana kwa sababu kuna watu ambao wengine hata wameshawahi kuwa Wabunge na hawaelewi utaratibu wa kutengeneza sheria. Kwa hiyo, mtu anafikiri Muswada ukiletwa na Serikali hapa Bungeni basi ni Serikali inayotunga sheria, eeh, hapana. Muswada unaletwa na Serikali, ndivyo Katiba yetu inavyosema kwa hiyo, watu wajielimishe. Muswada unaweza ukaletwa na Serikali, Muswada unaweza ukaletwa na Mbunge ambao utaitwa Muswada Binafsi. Sasa wewe ulitaka alete nani huo Muswada ili ujue ndiyo Bunge limetunga sheria?

Kwa hiyo, ni kazi ya Serikali kuangalia changamoto zilizoko kwenye jamii na kuzileta hapa Bungeni ili tutungie sheria hizo changamoto zilizopo. Tunaposema ni kazi yao kuzitazama ni kwa sababu, wao wamepewa mamlaka hayo na sisi Wabunge ni kazi yetu kusema humu Bungeni tukiwawakilisha wananchi wetu. Yale ambayo tunawawakilisha humu Bungeni ama tunayawasilisha humu Bungeni Serikali inapoyachukua yale yanayohitaji hatua za kawaida wanaendelea nayo, yale ambayo utekelezaji unahitaji sheria basi wanaleta Muswada. Kwa hiyo, ndio kazi yetu Bunge na ndivyo utaratibu ulivyo katika Mabunge yote ya Jumuiya ya Madola. Kwa hiyo, watu wasilete upotoshaji wa kuonesha kana kwamba, kulikuwa na namna tofauti ya kufanya tofauti na hayo ambayo tunayafanya.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya shukrani hizo na pongezi hizo na maelezo hayo mafupi, ninawapongeza pia upande wa Serikali kwa ujumla, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Waziri. Nikiipongeza Serikali tunaenda hadi kwa Mheshimiwa Rais kwa kuleta Muswada huu kwa lugha ya Kiswahili. *(Makofi)*

Tunawapongeza sana kwa sababu ni dhahiri, hata mmeona michango ya Wabunge wengi imekuwa ni michango mizito kutokana na kwamba, lugha ya Kiswahili inaeleweka na kila Mbunge na kwa hivyo, hata utekelezaji wake kwa zile Kamati mlizozianzisha katika ngazi mbalimbali za utawala itakuwa rahisi zaidi kwa sababu hata yule aliyeko kijijini, mtaani, ataweza kuisoma hii sheria, atajua mipaka yake, lakini pia atajua majukumu yake. Kwa hiyo, tunawapongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Baraza lake lote la Mawaziri kwa kutuletea sheria hii kwa lugha ya Kiswahili. *(Makofi)*

**13 SEPTEMBER, 2022**

Sasa Waheshimiwa Wabunge sheria hii kuletwa kwa Kiswahili inaashiria mambo mengi, yale mambo yetu ya kuchanganya lugha humu ndani, kama hii sheria imeweza kutengenezwa kuanzia Kifungu cha (1) mpaka cha mwisho na imeweka Kiswahili fasaha, hata sisi Waheshimiwa Wabunge tujifunze sasa kuzungumza Kiswahili fasaha, usichanganye na lugha nyingine ambazo zitakuwa hazipo hata kwenye sheria tulizotunga sisi wenyewe. Kwa hiyo, nawatakia kila la heri katika kujipanga kuzungumza lugha ya Kiswahili iliyo sanifu. Nawatakia kila la heri. *(Makofi)*

Wale wenzangu wa kuchanganya hata wakati wa kutunga sheria ndio tulikuwa tunachanganya sana kwa sababu, sheria itakuwa imeletwa Kiingereza. Sasa imeletwa Kiswahili, Mheshimiwa Mbunge huna sababu yoyote ya kuchanganya lugha unapochangia. Nawatakia kila la kheri katika mafunzo hayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 07.27 mchana Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano,  
Tarehe 15 Septemba, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*



**13 SEPTEMBER, 2022**